**3 APRILI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Pili – Tarehe 3 Aprili, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI MKUU:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:-**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa

Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. BAHATI K. NDINGO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhibiti wa UKIMWI) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsanteni sana.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 16

### Ajira za Wasaidizi wa Wanafunzi Wenye Ulemavu Uliozidi

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuajiri wasaidizi kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu uliozidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stela Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum kunahitaji kada ya wasaidizi wenye taaluma ya kutoa usaidizi kwa wanafunzi hao kulingana na changamoto zinazowakabili, ikiwa ni pamoja na kuwapa msaada wa awali pale inapohitajika. Kwa sasa Serikali imeendelea kuwatumia Walimu, wataalam waliosomea elimu maalum kuwafundisha na kuwahudumia wanafunzi hao.

Mheshimiwa Spika, pindi kada saidizi kitaalam kwa wanafunzi wenye ulemavu itakapotambulika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI iko tayari

kutoa ushauri wa kuajiri ili waweze kutoa usaidizi wa kitaalam kwa wanafunzi wenye changamoto kubwa zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, naomba muda wako kidogo; tarehe 6 Februari, 2024 *Mwananchi Digital* ilimwonesha mama ambaye amehamia shuleni, ameacha majukumu yake ya kiuchumi na kijamii ili kuweza kumsaidia mtoto wake awapo shuleni.

Swali la kwanza, je, hakuna kada inayofanana na kada hii ambayo nimeiulizia ambayo kwa sasa Serikali wakati inajiandaa kuipata kada husika inaweza ikaitumia ili kuwasaidia watoto hawa wawapo shuleni?

Swali la pili, je, ni nini mkakati wa Serikali kuipata sasa hii kada husika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli miongoni mwa wanafunzi wenye ulemavu wapo wanafunzi wenye ulemavu ambao umewaathiri kwa kiasi kikubwa na kushindwa kufanya baadhi ya majukumu ambayo kimsingi wanahitaji usaidizi wa karibu zaidi. Ndiyo maana Serikali imeweka utaratibu kuwa na vyuo vya Walimu, mafunzo maalum kwa wanafunzi wenye ulemavu, ambao kwa sasa wanatumika kuwasaidia wanafunzi hao katika mazingira hayo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunahitaji kuwa na kada maalum ambayo inaweza ikawasaidia kwa ukaribu zaidi wanafunzi wenye mahitaji makubwa ya usaidizi katika mazingira ya shule. Kwa hivyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalifanyia kazi hilo, inatambua umuhimu wao, lakini tuna mkakati wa kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwatumia pia Maafisa Ustawi wa Jamii katika maeneo hayo pamoja na Walimu wenye mafunzo

maalum ili wanafunzi wenye ulemavu waweze kupata huduma bora zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Patrobass Katambi, naona ulisimama.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, nikiongezea hapo ni kwamba, kwa kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu inayoshughulika na masuala ya watu wenye ulemavu sambamba na Wizara ya Elimu tumekwishaanza kufanyia kazi suala hilo la kuwa na kada maalum kwa ajili ya kutoa msaada kwa watu wenye ulemavu kwenye shule.

Mheshimiwa Spika, pia ukiangalia kwa upande wa vyuo vikuu *University of* Dar es Salaam wamekwishaanza. Kwa sasa tuko mbioni na tumeshapata bajeti maalum ya Mfuko wa Watu wenye Ulemavu ambao utasaidia katika kutekeleza jukumu hili. Kwa hiyo Serikali ipo katika hatua nzuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Mbarali, sasa aulize swali lake.

Na. 17

**Ukarabati wa Shule Kongwe za Msingi Mbarali**

**MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati shule kongwe za msingi zilizopo Mbarali ambazo zipo katika hali mbaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge Wa Jimbo la Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi wa madarasa mapya na ukarabati wa madarasa chakavu. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024, Serikali imetumia shilingi milioni 360 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa madarasa 18 mapya katika Shule Kongwe za Chimala, Igalako, Ujewa na Isitu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga shilingi milioni 180 kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za Ipwani, Ibumila na Mbuyuni. Aidha, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe kote nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nitakuomba mwongozo wako kwenye swali hili kwa sababu hizo milioni 360 zilifika katika Shule za Chimala, Igalako, Lujewa na Isitu kujenga madarasa mapya na siyo ukarabati wa shule kongwe. Kwa hiyo baadhi ya madarasa haya 18 yalijengwa kwenye shule hizi. Ninachokitaka mimi kwa Serikali lini wataanza ukarabati wa shule kongwe Mbarali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu hilo swali alilouliza kama swali la nyongeza ndiyo swali lake la msingi linavyosema. Kwa hiyo nadhani anahitaji majibu ya swali lake la msingi, haya yaliyoelezwa hapa ni ya ujenzi wa madarasa yeye anataka ukarabati wa shule kongwe zilizoko Mbarali ambazo zina hali mbaya. Kwa hiyo itabidi ajibiwe swali lake la msingi au unayo majibu ya mpango? Haya, karibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli, kama ambavyo Mheshimiwa Bahati Ndingo alivyosema kwamba swali lake la msingi ni ukarabati wa shule kongwe, lakini ukarabati unategemea na hali ya uchakavu wa madarasa, yapo madarasa

ambayo yamechakaa kiasi cha kutokarabatika *beyond repair*. Sasa Serikali inachofanya ni kujenga madarasa mengine katika shule hizo na kuvunja madarasa ambayo tayari yamechakaa kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili ndiyo lililofanyika katika shule hizi ikiwa ni sehemu ya ukarabati, lakini hatulazimiki kukarabati madarasa ambayo yana miaka sitini, yameshachokahayakabaratiki tena itakuwa ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kukarabati, kama tulivyofanya hivi katika shule hizi kwa namna ya kujenga madarasa mapya au kwa namna ya kukarabati madarasa ambayo yapo katika hali ambayo yanaweza kukarabatika. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tatizo hili liko maeneo mengi na shule hizi zinazoitwa kongwe, zingine siyo kongwe sana wala madarasa yake siyo makongwe sana; kwa sababu ni wale wanaotumia ni watoto yanaharibika haraka. Kwa hivyo ukarabati huu kwa sababu sasa hivi tunayo Wizara inayohusika na mipango, kwa kweli kuwe na mpango maalum wa kukarabati shule za sekondari zote na shule za msingi zote. Kwa sababu kule yalikojengwa haya madarasa mapya, kuna madarasa mapya watoto wanasoma humo na kuna madarasa yenye hali mbaya sana watoto wanasoma humo, kwa hiyo watoto wanajiona kama wale walioko huku na wao kuna utofauti huo.

Nadhani lazima kuwe na mpango huo maalum kwa ajili ya nchi nzima ili kuzileta hizi shule katika mazingira ambayo Mheshimiwa Rais amejenga hizi shule mpya na shule za zamani zifanane na hizi. Madarasa mapya yamejengwa kwenye shule mbalimbali yafanane na yale yaliyokuwepo pale shuleni.

Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, sasa aulize swali lake.

Na. 18

**Ukarabati wa Shule za Msingi Chakavu Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati shule chakavu za msingi katika Jimbo la Lushoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Jimbo la Lushoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kufanya ukarabati wa shule chakavu nchini ikiwemo zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ambapo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali imetoa shilingi milioni 796.5 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Shule ya Msingi Mshangai na Kwemshai katika Jimbo la Lushoto.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imetoa shilingi milioni 180 kwa ajili ya ukarabati wa Shule Kongwe nne za Nyankei, Mhelo, Hemtoye na Mbaramo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini kuna shule ambazo zina hali mbaya sana. Kwa mfano Shule ya Kwemashai, Shule ya Mshizii, Shule ya Msingi Kwai, Shule ya Msingi Matego, Kweboma pamoja na shule nyingine za Jimbo la Lushoto.

Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itapeleka fedha za dharura kwa ajili ya kukarabati shule hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pamoja na uchakavu wa shule lakini unaenda sambamba na ujenzi wa majengo na nyumba za Walimu. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za Walimu ili Walimu wetu hawa wasitembee umbali mrefu na vituo vyao vya kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge, amesema kwamba kuna baadhi ya shule ambazo zina uchakavu wa hali ya juu zaidi na kwa kweli zinahitaji bajeti maalum kwa ajili ya kuzikarabati. Kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua kwamba kuna shule ambazo zinahitaji maalum na tayari imeshaweka mkakati wa ukarabati wa shule hizo.

Mheshimiwa Spika, tumeanza na shule kongwe za sekondari baadhi ya shule zimekarabatiwa, bado nyingi zinahitaji ukarabati, lakini tuna shule nyingi za msingi ambazo tumeanza ukarabati na zoezi hili ni endelevu. Kwa hiyo naomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Lushoto kutuma wahandisi wa halmashauri hiyo ili kufanya tathmini ya mahitaji ya ukarabati kwa shule ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili fedha iweze kutafutwa, lakini pia kutafutwa mapato ya ndani kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali imeweka mkakati wa ujenzi wa nyumba za Walimu. Tumeanza kujenga nyumba za *three in one, two in one* lakini na zoezi hili linaendelea kila bajeti ya kila mwaka, tutahakikisha tunajenga nyumba za Walimu katika shule zetu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumain Bryceson Magessa, swali fupi la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Je, ni lini Serikali itakarabati Shule chakavu za Msingi katika Jimbo la Busanda ikiwemo Lubanda, Lulama na nyinginezo nyingi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua katika Jimbo la Busanda pia kuna shule chakavu. Tayari Serikali imeshaanza kuwaainisha shule chakavu zaidi katika majimbo yote kote nchini na fedha zinatafutwa kwa ajili ya kuanza ukarabati kwa awamu. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Jimbo la Busanda pia litapewa kipaumbele. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Kupandisha Walimu Madaraja kwa Mserereko**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kupandisha madaraja kwa mserereko Walimu wenye changamoto ya kupandishwa madaraja wakiwemo wa Ngara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 6(a) na (3) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 kikisomwa pamoja na Kanuni ya 17(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022; upandishaji vyeo watumishi wa umma pamoja na vigezo vingine huzingatia sifa za kielimu na kitaaluma zilizoainishwa katika miundo ya maendeleo ya utumishi, utendaji mzuri wa kazi, uwepo wa bajeti na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na ofisi yangu kuhusu utekelezaji wa ikama na bajeti kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia miongozo hiyo, ofisi yangu imeendelea kuhakiki taarifa na kuwapandisha vyeo watumishi wa kada ya ualimu waliobainishwa na waajiri kuwa na changamoto katika upandishwaji vyeo wakiwemo Walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Spika, naliahidi Bunge lako kuwa, zoezi hili litakapokamilika, watumishi wa kada ya ualimu waliobainishwa na waajiri wao, wakiwemo Walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara waliothibitishwa kuwa wametimiza sifa za kupanda madaraja watapandishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa kuna Walimu waliajiriwa 2013 na kumekuwa na upandishwaji wa madaraja kwa makundi huku Walimu walio wengi wakiachwa nyuma bila kupandishwa madaraja kutoka 2013. Ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha Walimu hawa wanapandishwa madaraja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa kuna kundi kubwa sana la Walimu wa Jimbo la Ngara ambao ni Walimu wa *grade A* ambao walitakiwa kuwa wamepandishwa mpaka kuwa *grade G* mpaka sasa hivi lakini wengi wameachwa nyuma na michakato hiyo. Ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha Walimu hawa wanapandishwa madaraja? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu ya msingi, kwa kuwa vipo vigezo vinavyotumika kwa ajili ya kupandisha madaraja Walimu, nataka kulihakikishia Bunge lako kwamba ule uchambuzi wa uhakiki uliokuwa unafanyika umekwishakamilika kwa upande mmoja ambapo katika Mwaka huu wa Fedha unaokwisha 2023/2024, Serikali inatarajia kupandisha Walimu 52,551 wakiwemo Walimu 148 wa Halmashauri ya Ngara ambao wamekwishatimiza vigezo vinavyotakiwa. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba, Walimu hawa tutawapandisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la Walimu ambao wamepandishwa katika *grade* nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Halmashauri ya Ngara kwamba, Serikali ilifanya uhakiki na uchambuzi wa walimu 283,193 wa halmashauri zote nchini. Katika uchambuzi huo tulibaini kwamba Walimu 54,242 wamekwishatimiza vigezo kwa wale ambao wanapandishwa madaraja na kati ya hao Walimu 540 wakiwemo wa Halmashauri ya Ngara na Halmashauri nyingine za Mkoa wa Kagera, ambao walikumbwa na changamoto hizo wamethibitika kwamba wamepata vigezo hivyo, wote kwa pamoja nao tutaweka katika mserereko ili waweze kufika katika madaraja wanayotakiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

Na. 20

**Kutoa Maeneo ya *EPZA* kwa Wananchi - Bagamoyo**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaachia maeneo yaliyotwaliwa na *EPZA* ambayo hayapo kwenye mipango ya matumizi ili wananchi wayatumie?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya *EPZA* imetwaa maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuanzisha Kanda Maalum za Kiuchumi. Maeneo hayo yapo katika hatua mbalimbali za utwaaji na uendelezaji. Katika kuendeleza maeneo hayo Mamlaka huandaa Mpango Kabambe ili kuainisha matumizi mbalimbali ya maeneo hayo. Hivyo, maeneo yaliyotwaliwa na *EPZA* bado yapo kwenye mpango wa matumizi yaliyokusudiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa ni mwaka wa 14 toka wananchi hawa wafanyiwe tathmini hawajalipwa, je, ni lini Serikali italipa wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Waziri yupo tayari kuongozana na Mheshimiwa Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo kwenda kuongea na hawa wananchi kujua hatma ya malipo yao? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, maeneo yote ambayo yametwaliwa yanayostahili kulipiwa fidia huwa tunaingiza kwenye bajeti na hata katika bajeti ambayo tutawalisha mwaka huu tutayapangia. Baadhi ya maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayataja yatakuwemo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwenda Bagamoyo Mheshimiwa Mkenge anafahamu kwamba hata mwaka jana tulikuwa naye na mwaka huu pia tumepanga kutembelea eneo la Bagamoyo. Kwa hiyo, wakati wowote tukimaliza vikao vya Bunge tutakwenda Bagamoyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mbunge wa Mpendae, sasa aulize swali lake.

Na. 21

**Mkakati wa Kuvutia Wawekezaji Wazawa**

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga majengo ya viwanda kuwapangishia wawekezaji wazawa ili kuongeza idadi kwani gharama za kuanzisha kiwanda ziko juu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Sera za Serikali katika uwekezaji ni kushirikiana kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika maendeleo ya viwanda. Serikali ina jukumu la msingi la kutwaa, kupima na kupanga matumizi ya ardhi, wakati sekta binafsi hukaribishwa na kuhamasishwa kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya viwanda. Utaratibu huu umeshaanza kuzaa

matunda ambapo hadi kufikia Desemba jumla ya kongani kubwa tatu za viwanda zimejengwa kwa ushirikiano kati ya sekta binafsi na Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, swali la nyongeza.

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali na naomba kuuliza swali la nyongeza, tukijua kuwa malighafi nyingi ndani ya nchi yetu inatoka katika vijiji. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha sekta binafsi waweze kuwekeza hizo *industrial pack* ili wananchi waweze kunufaika katika Taifa lao hususani kwenye vijiji? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji pamoja na Mamlaka ya *EPZA*, tumeendelea kuhamasisha wawekezaji kupitia njia za makongamano na *forum* mbalimbali. Hivi ninavyozungumza wiki iliyopita tu, tulikuwa na wawekezaji wa ndani 200 na wawekezaji kutoka China 100, walikutana pamoja na kuweka mikakati ya kuweza kushirikiana kwenye kuwekeza katika haya makongamano makubwa. Kwa hivyo, niwakaribishe hata Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Toufiq ambaye ni mfanyabiashara muhimu kabisa katika nchi yetu, aweze kuwekeza katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa, tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 22

**Bei ya Dizeli na Petroli kuwa moja Nchi Nzima**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka utaratibu ili bei ya mafuta ya dizeli na petroli iwe moja kwa nchi nzima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati. Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *EWURA* inafanya tathmini ya uwezekano wa kupanga bei moja ya bidhaa za petroli nchi nzima. Utaratibu huu uliokuwa ukitumika miaka ya nyuma, ulikwama kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo za kisera na kiusimamizi. Hivyo, wafanyabiashara wa mafuta waliruhusiwa kupanga bei za bidhaa za mafuta kuendana na ushindani wa soko. Tathmini hiyo itakapokamilika, Serikali itaweza kujiridhisha iwapo utaratibu huu una tija ikiwa ni pamoja na kujua namna bora ya kuusimamia ili kuhakikisha changamoto zilizojitokeza kipindi cha nyuma hazijirudii. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, ukizingatia kwamba Bandari ya Dar es Salaam ni bandari ya nchi nzima siyo Dar es Salaam peke yake, lakini tumeona kwamba mafuta kwa maana ya petroli na dizeli zimekuwa rahisi zaidi Dar es Salaam kuliko maeneo mengine ya pembezoni. Kwa mfano, kwa Taarifa ya *EWURA* ya jana petroli Dar es Salaam ni 3,257 na dizeli 3,210 lakini ukienda Songwe ni 3,374 na dizeli ni 3,227 na maeneo mengine hali kadhalika.

Mheshimiwa Spika, maswali yangu mawili ya nyongeza; la kwanza; je, Serikali inategemea kumaliza lini tathmini hiyo ili utekelezaji huu uanze mara moja na wananchi walioko nje ya Dar es Salaam waepuke hiyo changamoto? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba inatatua changamoto za nyuma kama ambavyo imezisema kwenye majibu yake ya leo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kumaliza tathmini yalikuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kufanya tathmini hii kwa haraka sana ili kuweza kujua kama tunaenda kwa mfumo huo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge suala hili ni la kipaumbele na tathmini itakamilika hivi karibuni na kisha tutaweza kufanya tathmini, ili kuweza kujua kama kweli tunaweza kwenda kwenye mfumo huo. Kwa hiyo, ni suala la kipaumbele kwa upande wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tathmini itatueleza namna ambavyo tulipata changamoto huko nyuma na kwa sasa tujipange vipi ili kuelekea kuwa na mfumo huu kama tathmini itatuelekeza hivyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. kwa kuwa wananchi wamehamasika kutumia nishati ya gesi kuendesha magari, je, ni upi mpango wa Serikali kuweza kuongeza vituo vya kuongeza nishati hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri swali hilo utaruhusiwa kulijibu kama swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 23

**Mradi wa maji kutoka Bwawa la Julius Nyerere kwenda Lindi na Mtwara**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha usanifu wa mradi wa maji ya Mto Rufiji yatokayo Bwawa la Julius Nyerere kupeleka Mikoa ya Lindi na Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na taratibu za tathmini ya awali ya usanifu wa Mradi wa Maji wa Mto Rufiji kutoka katika Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere, kupeleka kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa lengo la kuhakikisha inaongeza hali ya upatikanaji wa maji katika mikoa hiyo. Aidha, Serikali inaendelea na mapitio ya usanifu wa Mradi wa Kutoa Maji katika Mto Ruvuma kwenda kwenye Mikoa ya Mtwara na Lindi na maeneo ya pembezoni yatakayopitiwa na bomba kuu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ningependa kupata *commitment* ya Serikali kwamba usanifu huu wa awali utakuwa

umekamilika kufikia mwaka ujao wa fedha, ili tuweze kujua kwamba tatizo hili linaenda kutatuka kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali haioni haja ya kwenye miradi yote ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia maji, sasa Wizara ya Maji iweze kubeba yale maji yanayotumika baada ya kuzalisha umeme na kwenda kusambaza kwenye maeneo ya jirani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayofanya, lakini kubwa Wizara ya Maji mkakati wake mkubwa sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunatumia vyanzo toshelevu kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji. Moja ya mkakati ni kuhakikisha kwamba tunatumia maji haya ambayo yanazalishwa katika Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere. Pia tumeshaianza kazi ya kuyatoa maji ya Mto Ruvuma kuyapeleka katika Jimbo la Nanyumbu, lakini maji yale yatafika mpaka Jimbo la Masasi ili kuhakikisha wananchi wa Masasi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la haja ya kuyachukua na kuyasambaza maji yanayotoka katika maeneo ya uzalishaji wa umeme, Serikali inaona haja hiyo, maji yale baada ya kupotea tutayatumia katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha watu wanapata huduma ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itafanya mradi wa kuvuna maji na kuboresha Mto Lumemo ili kupunguza adha ya mafuriko kwa wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, uikizingatia nchi yetu haina umaskini kwa maana ya mvua na mvua badala ya kuwa fursa

imekuwa ikileta maafa mengi sana. Sasa maelekezo ya Mheshimiwa Rais kupitia Wizara yetu ya Maji na sekta zingine ni kuhakikisha kwamba, tunajenga mabwawa ya kimkakati na tumekwishaanza Bwawa la Kidunda na sasa hivi Bwawa la Farkwa, lakini pia tumepewa mitambo kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Mheshimiwa Asenga, Ifakara tutaipa kipaumbele hasa juu ya mitambo tuliyokuwa nayo ili kuondokana na adha hii ya mafuriko kwa wananchi wa Ifakara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 24

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kisasa Mtwara Vijijini**

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya zao la muhogo kuwa moja ya zao la kimkakati katika Mikoa ya Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara imeshatoa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 11,100 kwa ajili ya ujenzi wa

Kituo cha Polisi Daraja C eneo la Mkunwa. Ramani na mchoro wa kituo umeshakamilika na kiasi cha shilingi 300,265,723 zinahitajika kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Fedha hizo zinatarajiwa kutengwa kwenye bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Jimbo la Mtwara Vijijini kupakana na Nchi jirani ya Msumbiji; je, Serikali haioni haja sasa ya kujenga Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya ili kuleta tija kwa wananchi wa Jimbo langu la Mtwara Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchoro wa awali uliotayarishwa upo katika *level* hiyo niliyoitaja, wazo lake linachukuliwa na tutakwenda kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na.25

**Muhogo kuwa zao la kimkakati**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya zao la muhogo kuwa moja ya zao la kimkakati katika Mikoa ya Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuendeleza zao la muhogo nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na matumizi ya mbegu bora za muhogo zilizogunduliwa na *TARI* zenye uwezo wa kuzalisha tani 20 hadi 50 kwa ekari. Mbegu hizo zinapatikana kwenye Vituo vya Utafiti wa Kilimo *(TARI)* na kwa wazalishaji wa mbegu katika madaraja yote.

Mheshimiwa Spika, aidha, mbegu hizo zina sifa za mavuno yenye tija, wanga, kustahimili ukame, wadudu na ukinzani wa magonjwa. Kutokana na matumizi ya mbegu hizo, uzalishaji wa muhogo mkavu umeongezeka kutoka tani 2,486,000 Mwaka wa Fedha 2020/2021, hadi kufikia 2,575,453 Mwaka wa Fedha 2022/2023. Mkoa wa Mtwara upo katika nafasi ya tano ukitanguliwa na Tanga, Kigoma, Pwani na Kagera.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mkakati Mahsusi wa Kuendeleza Zao la Muhogo nchini ambao unalenga kuhamasisha uzalishaji wa zao hilo kwa tija, upatikanaji wa masoko ya uhakika ya bidhaa za muhogo, kuhamasisha wawekezaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za muhogo zenye thamani kubwa, kama vile viwanda vya kuzalisha wanga utokanao na zao la muhogo, bidhaa ambayo kwa sehemu kubwa huingizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kama sehemu ya utekelezaji wa mkakati huo, Wizara imepanga kufanya *Cassava Business Forum* ili kujadili biashara ya muhogo nchini utakaofanyika tarehe 15 Aprili, 2024. Kongamano hilo litawezesha kutangaza fursa zilizopo katika Mikoa ya Kusini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, changamoto kubwa ya wakulima wa zao la muhogo ni upatikanaji wa masoko. Nashukuru Mheshimiwa Waziri ameeleza, sasa je, katika hiyo *Business Forum* ambayo inategemea kufanyika mwezi huu, Waziri yupo tayari kuwaaalika wakulima wa muhogo kiutoka Jimbo la Nanyumbu ili washiriki, waje kueleza changamoto na matatizo yanayowakabili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tumeona wadau wengi ambao kule kusini walikuwa wanashirikiana na Serikali sasa hivi hawapo na wameondoka katika maeneo yao. Je, ni sababu zipi ambazo zimewasababisha wadau wale *VSO, TILED* wameondoka katika maeneo ya Wilaya ya Nanyumbu na hawajulikani wako wapi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika hiyo *Casava Business Forum* tutaalika wadau karibu wote ambao wanahusika na hii biashara ya muhogo wakiwemo wakulima wanaotoka eneo la Nanyumbu, kwa hiyo hilo naamini litafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, sababu kubwa ambayo wadau hawa walikuwa wameondoka katika Jimbo la Nanyumbu, ilikuwa ni changamoto kubwa ya soko kama ambavyo tumejadili hapo na ndiyo maana unaona tunaitisha hii ili tuweze kujua namna bora ambapo tutaondokana na hizi changamoto ikiwemo kutafuta soko la uhakika na kuhamasisha uwekezaji wa zao la muhogo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya yote tutayajibu zaidi kwenye hiyo *forum* na tutakuwa na mkakati madhubuti wa kuhakikisha sasa

hizi changamoto zinazotokana na zao hili ambazo tumeweka katika mazao 15 ambayo tunaendanayo kimkakati zinaondoka. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, sasa aulize swali lake.

Na. 26

**Barabara ya Murushaka hadi Murongo – Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali kwa Barabara ya Murushaka - Murongo ambayo Mkandarasi amepatikana zaidi ya mwaka mmoja bila Mkataba kusainiwa?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Murushaka – Murongo yenye urefu wa kilometa 125, sehemu ya Kyerwa – Omurushaka kilometa 50, kati ya *TANROADS* na Mkandarasi *Shandong Company Limited* umesainiwa tarehe 19 Februari, 2024. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Barabara hii imesainiwa tarehe 19, ni zaidi ya mwezi mzima tangu imesainiwa. Je, ni lini mkandarasi atakabidhiwa *site* ili aanze kazi rasmi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Barabara ya Omugakorongo – Kigarama mpaka Mrongo ilitangazwa kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini mpaka sasa hivi haijulikani ni hatua gani imefikia ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kyerwa kwamba, baada ya kusaini barabara hii kinachofuata sasa ni kumkabidhi mkandarasi ili aanze kazi. Tayari Meneja wa Mkoa wa Kagera ameshapewa maelekezo na *TANROADS* Makao Makuu kwamba kuanzia tarehe 5 mwezi huu, siku yoyote huyu mkandarasi aweze kukabidhiwa kazi na aanze kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Barabara ya Omugakorongo – Murongo, ilikuwa tayari imeshapata mkandarasi, lakini kwa taratibu za kimkataba, yuko mkandarasi ambaye ali-*appeal,* yaani alipinga mchakato wa manunuzi na hivyo imeamuliwa kazi hiyo itangazwe tena. Kwa hiyo, tuko kwenye hatua nyingine ya manunuzi baada ya ule mkataba wa kwanza kuonekana kwamba ulikuwa na changamoto za kisheria. Kwa hiyo, taratibu zinaendelea, tayari tuko kwenye manunuzi tena. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Barabara ya Masasi mpaka Liwale, kilometa 175, ni barabara ambayo imesainiwa tarehe 16 mwezi wa Sita mwaka uliopita 2023 kuwa itajengwa kwa *EPC+F,* lakini barabara hii usanifu wake …

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, uliza swali. Umeshaona wenzio wengi wamesimama hapa na tuna dakika chache tu. Hizo taarifa nyingine zote Waziri anazijua, wewe nenda kwenye barabara yako.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, wana-Liwale wamenituma niulize, barabara hii ujenzi wake unaanza lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara aliyoitaja itaanza kujengwa mwaka huu kama tulivyokuwa tumeahidi. Ahsante.

**SPIKA:** Mwaka huu ukimaanisha 2023/2024 au 2024/2025?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tunategemea kuanza ujenzi wa barabara hiyo mwaka huu wa fedha.

**SPIKA:** Mwaka huu wa fedha. Mheshimiwa Mbunge umesikia. Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya *Ruaha National Park* utasainiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Iringa – Msembe – *Ruaha National Park,* sasa hivi tuko kwenye *evaluation* na inafadhiliwa na *World Bank.* Baada ya kukamilisha taratibu hizo, barabara hiyo itaanza kujengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina kauli gani kwa barabara ya Iringa (MR) – Pawaga Road (Itunundu) ambayo mkandarasi ametelekeza vitu na haendelei na wakati alikuwa ameichimbachimba, hivyo wananchi kupata shida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge, baada ya hapa tuweze kukutana naye ili niweze kujua changamoto ya huyo mkandarasi na tuweze kuondoa hiyo changamoto ambayo mkandarasi anaileta kwa wananchi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, je, ni lini Barabara ya *bypass* inayoanzia Kata ya Kisaki mpaka Mtipa itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ilishasanifiwa na Serikali kwa kweli inaendelea kutafuta fedha ili kuweza kuijenga hiyo Barabara ya *Bypass* katika Mji wa Singida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, swali langu limeshajibiwa. Ni swali ambalo Mheshimiwa Kuchauka ameuliza. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ni lini ujenzi wa Barabara ya Mbagala Rangi Tatu mpaka Kongowe ambayo ipo katika bajeti ya mwaka huu utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo kilometa 3.8 imeshapata kibali cha kutangazwa ili ianze kujengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita Kisau, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kongwa – Kiteto – Simanjiro ni lini itaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, hiyo ni barabara ambayo iko kwenye *EPC+F*. Kama nilivyosema, tunategemea hizo barabara zianze kujengwa mwaka huu wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza?

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu, je, Serikali imefikia hatua gani kwenye maandalizi ya kujenga barabara ya Hydom – Mogitu kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ilishafanyiwa usanifu na tayari Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Barabara ya Iguguno – Nduguti, Wilaya ya Mkalama itaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo itaanza kujengwa mwaka huu, lakini imeshapata kibali cha kuitangaza. Kwa hiyo, bado tunatangaza, lakini tuko kwenye hatua ya kuitangaza mwaka huu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, ni lini barabara ya Utegi – Shirati – Kilongwe itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ndiyo kati ya zile barabara za kilometa 27 ambazo zimepewa kibali itangazwe kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Barabara ya Kongwa – Mpwapwa itaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tayari mkandarasi alishapatikana, kwa hiyo, kinachosubiriwa sasa hivi ni kumkabidhi *site*. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 27

**Kuanza kwa Bima ya Afya kwa Watu Wote**

**MHE. FURAHA N. MATONDO** aliuliza:-

Je, lini Bima ya Afya kwa watu wote itaanza kutumika?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ilipitishwa na Bunge tarehe 1 Novemba, 2023 na Mheshimiwa Rais ameidhinisha sheria hiyo tarehe 19 Novemba, 2023 na imechapishwa katika gazeti la Serikali la tarehe 1 Desemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza maandalizi ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambapo kwa mujibu wa Kifungu cha kwanza cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Waziri anaweza kuteua baadhi ya vifungu vya kuanza kutumika. Baadhi ya vifungu ambavyo vinaweka mifumo imara ya kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote vimeainishwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Sheria itatangazwa kuanza kutumika kabla ya mwisho wa mwezi wa Aprili, 2024 kwa tarehe itakayotajwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwanza naipongeza Serikali kwa majibu yake mazuri. Napenda kujua, katika utekelezaji wa Bima ya Afya, nini mkakati wa Serikali wa kuwasaidia akinamama wajane ambao hawatakuwa na uwezo wa kulipa Bima ya Afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; maeneo ya miji mikubwa kama Mkoa wa Mwanza kuna wimbi kubwa la watoto yatima na watoto wa mitaani. Nini mkakati wa Serikali wa kuwasaidia watoto hao kuweza kupata Bima ya Afya ili waweze kupata tiba bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri. Moja, anazungumzia kwamba ni nini Serikali itafanya kwa akinamama wajane ambao hawana uwezo, kwa sababu inategemeana, kuna mjane, lakini ana uwezo na kuna wale ambao hawana uwezo. Ninyi Wabunge mnakumbuka hapa mlisisitiza utaratibu wa kuwasaidia wasio na uwezo na utaratibu huo huo utatumika kulisaidia hilo kundi ambalo amelitaja.

Mheshimiwa Spika, pia, amezungumzia watoto wa mtaani, nao vile vile wanaangukia kwenye eneo lile lile, lakini wote kwa pamoja suala la watoto wa mtaani tusione kama ni kundi maalum, tuone ni kundi la sisi kuhamasishana kuliondoa mtaani na kuhakikisha liko nyumbani, liwe na utaratibu mzuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, ningewatangaza wageni sasa, lakini majina hayajanifikia hapa. Kwa hiyo, tutambue tu wageni walioko humu Bungeni, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Niongee kuhusu jambo moja, halafu nitamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aje awasilishe hoja yake hapa. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa *Chief Whip,* majibu ya Serikali yanapoanza kusomwa hapa mbele na Mawaziri na Naibu Mawaziri, waanzie jibu linapoanza badala ya kuanza kwa niaba au kwa nani. Nadhani hayo maelekezo nilishatoa huko mwanzo, lakini ni jambo linalojirudia.

Majibu yanapoletwa, yanasomwa yote vile. Ile "kwa niaba," mimi Mbunge nakuwa nimeshamtaja na swali lake ameshalitaja yeye, kwa hiyo, Waziri au Naibu Waziri hana haja tena kwenda huko. Yeye ameshaleta yale majibu yake aanzie majibu ya Serikali yanapoanzia ili tukomboe wakati, maana kipindi chetu cha Maswali na Majibu ni kifupi.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba yetu. Haya, kabla hatujaendelea, orodha ya majina imefika hapa na Waheshimiwa Wabunge, mnaotembea mketi.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotutembelea Bungeni asubuhi hii. Nitawatangaza kwenu, halafu tutaendelea na ratiba yetu.

Wabunge wanaotembea na wanaozungumza, naona wanasubiri kutajwa kidogo hapa mbele.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, kwanza ni wageni 26 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; hawa ni Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Wakurugenzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu; Dkt. Jim James Yonazi ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu; Ndugu Anderson Mtatembwa, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Said Mabiye, Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu; Ndugu Bengi Issa ambaye ni Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Dkt. Jerome Kamwela, Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS);* Dkt. Godwill Wanga, Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Biashara; Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama Vya Siasa; na Ndugu Aretas Lyimo, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Suleiman Mohamed, Mwenyekiti wa Bodi ya Mishahara Sekta Binafsi; Dkt. Samweli Nyantahe, Mwenyekiti Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii Ushauri *(RESCO);* yupo pia Ndugu Hadija Mwenda, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi *(OSHA);* Ndugu Suzana Mkangwa, Kamishna wa Kazi; Ndugu Zena Amour, Mwakilishi wa *UNICEF;* Ndugu Edmund Mushi, Mwakilishi Shirika la Kazi Duniani *(ILO);* Ndugu Tumaini Nyamhokya, Mwenyekiti *TUCTA;* Ndugu Oscar Mgaya, Mwenyekiti Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE);* na Ndugu Ernest Kimaya, Mwenyekiti Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA). *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Mariam Ngaeje, Mwakilishi Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani *(UNFPA);* Ndugu Mussa Mchola,

Mwenyekiti, huyu hajaandikwa ni Mwenyekiti wa nini, lakini ni Mwenyekiti; Dkt. Lucas Luhende, Mwenyekiti Baraza la Ushauri la Taifa kwa Watu Wenye Ulemavu; na Dkt. John Mduma, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF)*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa wameambatana na Wakurugenzi na Maafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na wote wasimame kwa pamoja. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Ighondo Ramadhan ambao ni Madiwani wa Kata, Katibu wa CCM Wilaya na Mwenyekiti wa Vijana Wilaya kutoka Mkoa wa Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Ester Bulaya ambao ni mdogo wake na mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu watoto wa kulea ni watoto wetu, kwa hiyo, hapa sasa ameandikwa mtoto wake na watu wanamjua mtoto wake na pale hawamwoni, sasa ndiyo nikawa najiuliza, sijui kama ameshaongeza mwingine, lakini tunamtakia kila la heri katika hiyo safari. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao. Tunaendelea na ratiba yetu. Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa

Kassim Majaliwa Majaliwa, aje awasilishe hoja ya ofisi yake kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2023/2024 na Mwelekeo wa Kazi zake kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa fadhila zake ambazo zimetuwezesha kukutana hapa leo, kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mwelekeo wake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 tukiwa wenye afya njema. Aidha, natumia fursa hii kuwapongeza Wakristo wote kwa kuhitimisha Kwaresma pamoja na kuadhimisha Sikukuu ya Pasaka kwa mwaka 2024. Vilevile nawatakia Waislam wote heri ya Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mwenyezi Mungu atujalie sote tukamilishe funga zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, salamu za pole; naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania kwa ujumla kwa kumpoteza kiongozi wetu

mpendwa, Hayati Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, naishukuru Kamati ya Kitaifa ya kuratibu mazishi kwa kujitoa kwao usiku na mchana kufanikisha taratibu zote muhimu za maziko, sambamba na kuhakikisha kuwa kiongozi wetu anapewa heshima zote za mwisho hadi alipopumzishwa katika Kijiji cha Mangapwani, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hakika tunaendelea kumuenzi kiongozi huyu mahiri aliyeleta mageuzi ya kisiasa kwa kurejesha mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vyingi mnamo mwaka 1992, kufungua nchi kiuchumi na kuruhusu uwekezaji wa sekta binafsi katika njia kuu za uchumi pamoja na hulka ya ustahimilivu, unyenyekevu na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile, hivi karibuni tumeondokewa na mwanasiasa nguli na mahiri, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowasa, aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Natumia nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa kumpoteza kiongozi huyo ambaye atakumbukwa kwa uthubutu wake, uwezo na ushawishi mkubwa wa kisiasa. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ampe Marehemu pumziko la amani. Amina.

Mheshimiwa Spika, tangu tulipohitimisha Mkutano wa 14 nchi yetu imekumbwa na maafa yaliyosababisha athari mbalimbali vikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanznaia wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao kutokana na maafa hayo. Mwenyezi Mungu awape marehemu pumziko la milele, Amina. Aidha, tunamwomba pia Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji wa haraka ndugu zetu walioumia na ambao bado hawajapona ili waweze kupona na kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, salamu za pongezi; nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu tangu ashike madaraka na kuendelea kutuongoza vyema, huku tukishuhudia mafanikio lukuki chini ya uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo yanaonekana dhahiri katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu na huduma za kiuchumi na kijamii, ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya, maji, elimu, nishati, uchukuzi na kuimarisha hali ya kisiasa nchini pamoja na mahusiano ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumsaidia majukumu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuongoza na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Serikali yenye kuleta manufaa kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake thabiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kunisaidia katika kuratibu na kufuatilia na kusimamia shughuli mbalimbali za Serikali kwa ufanisi. Hakika wote mtakubaliana na mimi kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ameonesha uwezo mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yake aliyopewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nawapongeze Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Mbunge wa Chamwino na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu. Pia, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais. Nawatakia kila la heri viongozi wote walioteuliwa katika utekelezaji wa majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na kuwatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya, napenda kutumia fursa hii kuwakumbusha kuendelea kusimamia kikamilifu mipango ya Serikali na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 ili kuhakikisha kwamba lengo na maendeleo tuliyojiwekea yanafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabaraza ya Kitaifa Duniani *(IPU)* na Baraza la Uongozi la *IPU* ambacho ni chombo kikuu cha kufanya maamuzi kinachojumuisha Wabunge kutoka duniani kote. Hakika unastahili pongezi za kipekee kwa kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo tangu historia ya kuanzishwa kwa chombo hicho. Vilevile, naendelea kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima na umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina shaka na Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana nami kuwa Mheshimiwa Spika ameendelea kuonesha ukomavu, ustahimilivu na weledi wa hali ya juu katika kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge. Hongera sana kwa kutekeleza majukumu yako kwa viwango vya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala na Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo kabla ya uteuzi, kwa kuendelea kukusaidia kikamilifu kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Nitoe wito kwetu sote tuendelee kuwapa ushirikiano ili waendelee kuliongoza vyema Bunge letu na kulifanya liendelee kuheshimika ndani na nje ya mipaka yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Vilevile, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Ustawi na Maendeleo

ya Jamii, vilevile, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Wajumbe wote wa Kamati hizo kwa michango yao iliyosaidia kuboresha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niwashukuru sana Wenyeviti, Makamu Wenyeviti wote pamoja na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge lako Tukufu kwa ushauri walioutoa wakati wa kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali Zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maoni na ushauri wao utazingatiwa vilivyo wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wake katika utendaji wa majukumu ya kila siku kati ya Serikali na Bunge. Nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Wakuu wa Mikoa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu na Wakuu wa Wilaya, Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano waliotupatia na wanaoendelea kunipa wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nawapongeza na kuwashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na taasisi zake kwa kufanya kazi kwa weledi, utaalam na umahiri mkubwa na hivyo kuwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Vilevile, Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi, Mbunge wa Shinyanga Mjini na Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu

kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumshukuru Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa ushirikiano mkubwa aliokuwa akiuonesha wakati wote alipokuwa akitekeleza majukumu yake ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Namtakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kumshukuru Dkt. Jim James Yonazi, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Bwana Anderson Mtatembwa, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu na wafanyakazi wote, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa wakati wote kwenye majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie fursa hii pia kumpongeza Bi. Mary Ngelela Mganga kwa uteuzi aliopata na kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Kipekee namshukuru Mhandisi Cyprian John Luhemeja, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa ushirikiano mkubwa aliouonesha wakati akitekeleza majukumu yake katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Namtakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yake mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo zikiwemo Taasisi Binafsi, Nchi Rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Madhehebu ya Dini kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kujenga uchumi shindani wa viwanda na kuiletea nchi yetu maendeleo. Serikali inathamini michango yao kwenye afua mbalimbali na utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kitendo hicho kimekuwa chachu ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee na umuhimu mkubwa, nataka nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la

Ruangwa kwa kuendelea kuniunga mkono na kuielewa vizuri dhamana ya Kitaifa niliyonayo ya kusimamia utendaji wa Serikali katika sekta zote na kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Vilevile, nawashukuru Watanzania wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inaendelea kutekeleza kwa dhati dhamira ya kuwaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa umuhimu wa kipekee, naishukuru familia yangu hususan mke wangu mpendwa Mary na watoto wetu kwa upendo, dua na kuendelea kunitia moyo ili nitekeleze kwa ufanisi zaidi majukumu ya Kitaifa niliyopewa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni Mkutano wa 15 wa Bunge la Kumi na Mbili ambao ni mahususi kwa ajili ya mjadala wa Bajeti ya Serikali. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuitumie vyema fursa hii kutoa maoni na ushauri ili kuisaidia Serikali kuimarisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2024/2025. Napenda kuwahakikishia kuwa, Serikali yenu sikivu iko tayari kupokea maoni na ushauri wenu na kufanyia kazi kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuwasilisha makadirio ya bajeti ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa vipaumbele vilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2023/2024, Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya 2050, Ajenda ya 2063 ya Maendeleo ya Afrika na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, nianze na utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; Serikali imeendelea kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Kielelezo hususan miradi ya miundombinu ya reli, barabara, viwanja vya ndege, huduma za jamii na nishati, yenye mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa letu. Hadi kufikia Februari 2024, utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa kilometa 1,219; Serikali yetu imeendelea kutoa fedha za utekelezaji wa mradi huu ambapo jumla ya shilingi trilioni 10.69 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa. Ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro kilometa 300 umefikia 98.84%, ujenzi wa kipande cha Morogoro – Makutopora kilometa 492 umefikia 96.35%, kipande cha Mwanza – Isaka kilometa 341 umefikia 52.69%, ujenzi wa Makutopora – Tabora kilometa 371 umefikia 13.86%, ujenzi wa Tabora – Isaka kilometa 165 umefikia 5.38% na ujenzi wa Tabora – Kigoma kilometa 506 umefikia 1.81%.

Mheshimiwa Spika, kama nyote mlivyoshuhudia majaribio ya treni hiyo ya mwendokasi yaliyofanyika kwa mafanikio makubwa mwezi Februari mwaka huu, ni matarajio yetu kuwa, huduma ya usafiri na usafirishaji itaanza ifikapo Julai, 2024, kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma. Reli hiyo ya Kisasa itakapoanza kufanya kazi itarahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa baina ya Bandari ya Dar es Salaam na sehemu za ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere, Megawati 2,115; mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere ambao utazalisha Megawati 2,115, utekelezaji wake umefikia 96.81%. Kama mlivyoshuhudia zoezi la kuwasha mtambo wa kuzalisha umeme lililofanyika kwa mafanikio na kuingiza kwenye Gridi ya Taifa Megawati 235, mtambo huo ni mmoja kati ya mitambo tisa itakayozalisha umeme katika mradi huo. Aidha, kazi zote katika mradi huu zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Disemba, 2024.

Mheshimiwa Spika, tatu, uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania; Serikali imekamilisha malipo ya shilingi bilioni 753 kwa ajili ya ndege tatu. *Boeing 787-A8* ndege moja na ndege mbili aina ya *Boeing 737-9MAX*, zilizowasili nchini Oktoba, 2023 na Machi, 2024 na nyingine moja inategemewa kuwasili Aprili, 2024. Hivyo, kulifanya shirika hilo kuwa na jumla ya ndege 16. Ndege hizo zitawezesha kuongeza safari za ndege za nje ya nchi na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi kama vile utalii, biashara, kilimo, mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, ni Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima Uganda hadi Tanga Tanzania lenye urefu wa kilometa 1,443. Serikali yetu imeendelea kutekeleza Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima Nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga. Hadi kufikia Machi, 2024, baadhi ya shughuli zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha ulipaji fidia kiasi cha shilingi bilioni 34.93 kwa wananchi 9,823 kati ya 9,904 wanaopisha eneo la mradi, kukamilika na kuzinduliwa kwa Kiwanda cha Kusimika Mifumo ya Kupasha Joto na Kuzuia Upotevu wa Joto kwenye bomba kilichopo Wilaya ya Nzega na kuanza ujenzi wa matanki manne yenye ujazo wa mapipa 500,000 kila moja na kuhifadhia mafuta ghafi kabla ya kupakiwa kwenda kwenye meli katika eneo la Chongoleni.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kwa ushiriki wake kwenye mradi tayari imechangia jumla ya Dola za Marekani milioni 268.77 sawa na 87.27 ya hisa zake.

Mheshimiwa Spika, tano, ni Mradi wa Kiwanda cha Sukari pale Mkulazi. Serikali imeendelea na ujenzi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi, Mkoani Morogoro ambapo ujenzi umefikia 99%, kwa gharama ya shilingi bilioni 320.05. Kiwanda hicho kimeanza uzalishaji Disemba, 2023 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024, jumla ya tani 1,851 za sukari zimezalishwa na kupelekwa sokoni. Kuanza kwa uzalishaji wa sukari katika Kiwanda cha Mkulazi kunaongeza kiwango cha upatikanaji wa sukari hapa nchini na kuchangia kuongezeka kwa ajira ambapo hadi sasa kiwanda kimetoa fursa za ajira 1,996. Matarajio ya kiwanda hiki ni kuzalisha tani 50,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, mradi wa sita, ni Mradi wa Daraja Kigongo – Busisi Mkoani Mwanza. Ujenzi wa Daraja Kingogo – Busisi lenye urefu wa kilometa 3.2 pamoja na barabara unganishi yenye urefu wa kilometa 1.66 kwa kiwango cha lami, umefikia asilimia 84.7%.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utagharimu shilingi bilioni 716.333 ambapo hadi sasa Mkandarasi ameshalipwa jumla ya shilingi bilioni 441.309 na Mhandisi Mshauri ameshalipwa jumla ya shilingi bilioni 6.260. Mradi huu ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2024

utasaidia kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii na kuongeza kasi ya maendeleo kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa saba, ni mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato hapa Jijini Dodoma. Ujenzi wa uwanja wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato umefikia asilimia 54.1 katika sehemu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua, barabara ya viungio, maegesho ya ndege pamoja na usimikaji wa taa za usalama na kuongozea ndege. Pia sehemu ya pili inayohusisha ujenzi wa jengo la abiria na majengo mengine utekelezaji wake umefikia asilimia 17.1. Hadi Februari mwaka huu 2024 jumla ya shilingi bilioni 107.647 zimeshatumika. Kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja hiki kutarahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa kutoka na kuingia nchini na hivyo kukuza utalii na uchumi na kuongeza fursa za ajira.

Mheshimiwa Spika, nane ni kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwenye Maziwa Makuu. Ujenzi wa meli ya *MV* Mwanza "Hapa Kazi Tu" umefikia asilimia 93 ambapo Serikali imetumia dola za Marekani milioni 44.823 sawa na asilimia 90.87 ya gharama zote za mradi huu ambao unatarajiwa kukamilika Mei, 2024. Kukamilika kwa mradi huu kutaboresha huduma za usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya meli katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Nchi jirani za Kenya, Uganda na kufungua nchi kiuchumi na kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii. Vilevile Ziwa Tanganyika lakini pia Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, hali ya Uchumi; uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika licha ya kukumbwa na changamoto kadhaa ambazo baadhi zinatokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa Serikali kama vile mabadiliko ya tabianchi, athari za vita na ushindani wa kisiasa, kiuchumi, mikingamo ya kisera ya mataifa makubwa. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2023 ukuaji wa uchumi wa Taifa ulikuwa asilimia 5.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imelenga kuongeza kasi ya ukuaji wa pato halisi la Taifa kufikia asilimia 5.4 kwa mwaka 2024 kutoka matarajio ya ukuaji wa asilimia 5.2 mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi wetu utachangiwa na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa ikiwemo kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kuwianisha, kufuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada vinavyoonekana kuwa kero. Maelezo ya kina kuhusu mwenendo mzuri wa ukuaji wa uchumi na matokeo yake yanapatikana katika aya ya 25 hadi ya 28 ya kitabu cha hotuba kilichopo pia kwenye vishikwambi vyenu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumuko wa bei; katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023 wastani wa mfumuko wa bei umepungua na kufikia asilimia 3.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi la wastani wa asilimia tatu hadi asilimia tano. Kupungua kwa kiwango cha mfumuko wa bei nchini kimechangiwa na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti pamoja na upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani. Mfumuko wa bei nchini unatarajiwa kuendelea kuwa tulivu na kubaki katika viwango na wigo wa tarakimu moja wa wastani wa asilimia tatu mpaka asilimia tano na ndani ya vigezo vya mtangamano vya kiuchumi vya kikanda kutokana na hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, ikiwemo kuchochea uzalishaji wa ndani na kupunguza nakisi ya urari wa biashara, usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti, utulivu wa thamani ya shilingi na kuimarisha upatikanaji wa umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa ukusanyaji wa mapato; katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Januari, 2024 mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 17,188.4 sawa na asilimia 95.9 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 17,929.8 na ukuaji wa asilimia 10 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka wa 2022/2023. Kati ya mapato hayo mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yalikuwa shilingi bilioni 15,159.8 sawa na asilimia 97.9 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 15,492.7. Mapato yaliyokusanywa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Taasisi za Serikali yalikuwa shilingi bilioni 1,374.5 sawa na asilimia 78.2 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 1,758.3. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa

yalifikia shilingi bilioni 654.1 ikiwa ni asilimia 96.4 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 678.8.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa wafanyabiashara wote kuhakikisha kuwa wanatoa risiti halali za kieletroniki za mauzo za bidhaa zao na huduma wanayoitoa. Vile vile niwakumbushe wananchi wote kudai risiti halali za kieletroniki kila wanapofanya ununuzi wa bidhaa na huduma ili kudhibiti upotevu wa mapato na hivyo kuimarisha uwezo wa Serikali katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi ikiwemo maji, elimu na afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itaendelea kuweka vipaumbele zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa bajeti kwa kuendelea kutekeleza hatua zifuatazo: Kuimarisha na kuboresha mazingira biashara na uwekezaji nchini, ikiwa ni pamoja na kuwianisha, kufuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada zinazoonekana kuwa ni kero; Kuboresha mazingira ya ulipaji kodi na kuongeza wigo wa kodi; Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi; na Kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato. Hatua hizi zitawezesha kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kukuza mapato ya ndani kufikia asilimia 15.7 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.3 ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya uwekezaji; Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imedhamiria kuifungua nchi katika uchumi wa dunia kupitia utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayolenga kuimarisha mazingira ya uwekezaji hapa nchini. Baadhi ya mikakati inayotekelezwa ni pamoja na Mheshimiwa Rais kuboresha miundombinu ya taasisi za Serikali, kuhamasisha baadhi ya majukumu ikiwa ni pamoja na kuhamishia masuala ya uwekezaji katika Ofisi ya Rais kutoka iliyokuwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Wizara hiyo imeanzishwa mahususi ili kuimarisha uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imeendelea kuboresha mifumo ya kujisajili na kusajili miradi ili kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024, jumla ya miradi 416 ilisajiliwa ambapo miradi ya Watanzania ni 153, wageni 175 na ubia ni 88 sawa na ongezeko la asilimia 205 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 ambapo jumla ya miradi 203 ilisajiliwa na miradi hiyo inatarajiwa kuwekeza jumla ya dola za Marekani milioni 4,490 na kuzalisha jumla ya ajira119,717. Uwekezaji huo utaimarisha uchumi wa Taifa letu pamoja na kuboresha maisha ya watu wetu kupitia fursa za ajira, ukusanyaji wa mapato na kunufaika na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kutunga sera, sheria, kanuni, mikakati na miongozo ili kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji hapa nchini. Katika kuhamasisha ushiriki wa Halmashauri na Serikali za Mikoa, sekta binafsi na wadau wa maendeleo katika uendelezaji wa maeneo ya uwekezaji na uendelezaji wa miundombinu ili kuvutia uwekezaji na kuimarisha upatikanaji wa huduma za uwekezaji katika ngazi zote kwa kuanzisha Benki ya Ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa kutoa maeneo kwa ajili ya uwekezaji mahsusi. Maelezo zaidi kuhusu uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara yanapatikana katika aya ya 37 na aya ya 38 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, utawala wa sheria; Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya utoaji wa haki na huduma zinazotolewa na Mahakama kwa kujenga na kukarabati majengo ya mahakama katika ngazi mbalimbali. Hadi Januari, 2024, Serikali inaendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama hapa Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia 97 na ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Korogwe, Ulanga na Ubungo unaendelea. Aidha, ujenzi wa Mahakama za Mwanzo tatu upo katika hatua mbalimbali katika maeneo ya Madale Dar es Salaam, Kinesi na Rorya Mkoani Mara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa haki kwa kuimarisha mifumo ya kieletroniki ya

usikilizaji wa mashauri, utunzaji wa kumbukumbu, ukusanyaji wa takwimu na utoaji wa taarifa za kimahakama unaofahamika kama *Judicial Statistical Dashboard System* pamoja na matumizi ya *video conference* katika kuendesha mashauri ya usuluhishi ya kimataifa na hata baadhi ya mashauri ya hapa ndani. Aidha, Mahakama imeanza majaribio ya matumizi ya teknolojia ya akili mnemba ya kunakili na kutafsiri lugha ya mawasiliano wakati wa mwenendo wa usikilizwaji wa mashauri Mahakamani. Mifumo hii imewezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake na kuendesha mashauri na utoaji haki kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka utaratibu na upatikanaji wa msaada wa kisheria hususani kwa wananchi ambao hawana uwezo wa kumudu gharama za wanasheria. Taarifa za wananchi walionufaika na kampeni za msaada wa kisheria na maboresho ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika huduma za kimahakama zinapatikana katika aya ya 42 hadi 43 ya kitabu cha hotuba ambacho kipo kwenye vishikwambi vyenu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali itaendelea kuimarisha utawala wa sheria kwa kuendelea kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki, lakini pia kuimarisha mahusiano na taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa; kuendelea kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro ambazo ni usuluhishi, upatanishi, maridhiano, majadiliano ili kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa haki; kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za sheria na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za uzalishaji; kwenye Sekta ya Kilimo Serikali imeendelea kutekeleza programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya pili *ASDP II* ya mwaka 2017/2018 hadi 2027/2028 katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imefanya mapitio ya kati ya programu hiyo ambapo tathmini ya utekelezaji wa kipindi cha miaka mitano ya awali imeonesha ufikiaji wa malengo kwa asilimia 66 ikijumuisha kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi. Aidha, matokeo hayo ya awali yanaonesha umuhimu wa kuongeza uwekezaji katika sekta ndogo za mazao na uvuvi ili kufikia malengo.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha mazao; Serikali imeendelea kuongeza tija na uzalishaji katika mazao na kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora na mbolea, kuwezesha upatikanaji wa dhana bora za kisasa za kilimo pamoja na teknolojia ya kisasa na rafiki kwa wakulima wetu. Vile vile kuhakikisha kilimo kinakuwa na faida kwa kuhamasisha uongezaji wa thamani kwenye mazao na upatikanaji wa masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa ulikuwa tani milioni 20.4 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani milioni 16.3 na uzalishaji huo umehakikisha nchi imekuwa na utoshelevu wa chakula kwa asilimia 124 kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Serikali imeendelea kuwezesha na kuwekeza katika ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji katika miradi mipya 28 na miradi 30 ya ukarabati yenye jumla ya hekari 95,000 ambayo imefika wastani wa asilimia 76. Aidha, ujenzi wa mabwawa 11 kati ya 14 umefikia wastani wa asilimia 65 kukamilika. Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hii kutaifanya nchi kuwa na hekta 728,223 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji sawa na asilimia 60.69 ya lengo la hekta 1,200,000 ifikapo mwaka 2025. Taarifa zaidi kuhusu jitihada za kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo biashara pamoja na uzalishaji wa sukari nchi zinabainishwa kuanzia aya ya 48 hadi aya ya 51 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya ushirika; katika sekta ya kilimo Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuimarisha ushirika kwa kuimarisha mifumo ya uendeshaji, kufanya kaguzi, kuhamasisha uwekezaji na kuendelea kutoa mikopo kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Taarifa za kina kuhusiana na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika maendeleo haya na maeneo haya zimeainishwa katika kitabu cha hotuba aya ya 52 hadi aya ya 55.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mifugo; Serikali kwa kutambua mchango wa sekta ya mifugo kiuchumi na kijamii imeendelea kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma za mifugo na kuimarisha huduma za ugani. Katika mwaka 2023/2024, Serikali

imenunua vifaatiba 1,100, pikipiki 1,200 na vifaa vya uhimilishaji 184. Vile vile imeendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa maji kwa mifugo, kukamilisha ujenzi wa mabwawa matatu ya vinyenze Mkoani Pwani, Kihumbu Wilayani Bunda na Kongwa Morogoro *DC*. Pamoja na kuendelea na ujenzi wa mabwawa saba katika Mikoa ya Arusha, Mara, Tanga, Katavi, Manyara, Simiyu, Singida na Songwe, pamoja na utoaji wa mafunzo kuhusu upandaji, uvunaji na uhifadhi wa malisho na mbegu za malisho kupitia mashamba darasa 150 yaliyoanzishwa katika Halmashauri za Wilaya 71.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirika wa vijana na wanawake katika programu ya *BBT* ambapo jumla ya vijana 165 wameendelea kupatiwa mafunzo ya kufuga kibiashara ambapo jumla ya ng'ombe 2,176 wamenenepeshwa na kuuzwa kwa thamani ya shilingi bilioni 1.22 na kupata faida ya shilingi milioni 153.64. Aidha Serikali imeendelea na itaendelea na taratibu za kuanzisha vituo nane vipya vya *BBT* katika Mikoa ya Tabora viwili, Arusha viwili, Morogoro viwili, Pwani kimoja na Mtwara kimoja ili kuwashirikisha vijana wengi zaidi kufuga kibiashara.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi; Serikali yetu imeendelea kuimarisha miundombinu ya sekta ya uvuvi pamoja na kuwapatia wavuvi dhana bora.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu subiri kidogo. Upande wangu wa kushoto kuna sauti inatoka mtu anaongea kwa nguvu sana, watu wote humu ndani wanaongea lakini yeye anaongea kwa nguvu sana. Sasa ninyi mnaozungumza huku kuna hiyo sauti inayotoka ni ya mwanaume, tafadhali utoke nje kidogo kama unaongea na simu ama vipi ili tuweze kumsikiliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali yetu inaendelea na Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Wilayani Kilwa eneo la Kilwa Masoko unaotarajiwa kukamilika ifikapo Februari, 2025. Vile vile Serikali imenunua na kusambaza boti 160 za kisasa za uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 11.5 kwa vyama vya ushirika vya

wavuvi, watu binafsi na vikundi vya wavuvi katika Halmashauri za Wilaya 58. Aidha, Serikali imejenga vizimba 222 katika Mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza, Kagera na Geita kwa ajili ya kuwawezesha wafugaji samaki 1,213 kufanya biashara zao katika mazingira bora kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali itaendelea na ujenzi wa mabwawa na majosho; kuhamasisha matumizi ya mbegu bora za mifugo; kukamilisha ujenzi wa bandari ya uvuvi; kuendelea na taratibu za ununuzi wa meli na uvuvi wa bahari kuu; na kununua boti 520 za kisasa na Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali itaendelea kutekeleza programu ya kuendeleza kilimo awamu ya pili ya *ASDP II* pamoja na mapendekezo yanayotokana na mapitio ya programu hiyo ikiwemo uzingativu wa mifumo ya chakula, kuimarisha ushirika, uwezeshaji kwa wakulima ili waweze kuongeza tija katika shughuli za kilimo, kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, kuratibu upatikanaji wa pembejeo, kuboresha huduma za ugani, upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi, pamoja na kuimarisha utoshelevu na usalama wa chakula hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Maliasili na Utalii; Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya sekta ndogo ya utalii, wanyamapori, misitu, ufugaji nyuki na mali kale na kuhamasisha uwekezaji ili kuhakikisha rasilimali za sekta hizo zinatumika kwa njia endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023, tumeshuhudia ongezeko la idadi kubwa ya watalii wa kimataifa kutoka 1,454,920 mwaka 2022 hadi kufikia watalii 1,808,205 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Aidha, mapato ya ndani ya utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.53 mwaka 2022 hadi kufikia Dola za Marekani Bilioni 3.37 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 33.5.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kutangaza utalii ndani ya nchi na nje ya nchi ili kuongeza mapato yatokanayo na utalii. Kutokana na mafanikio haya programu ya *Tanzania the Royal Tour* Serikali imetengeneza filamu

nyingine yenye hadhi ya Kimataifa ya kutangaza utalii ijulikanayo kama *Amazing Tanzania. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, filamu hii imerekodiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mchezaji filamu nguli kutoka Nchini China ajulikanaye kwa jina la Jin Dong. Filamu hiyo imeandaliwa kwa lengo la kuvutia watalii hususani katika soko la China na inatarajiwa kuzinduliwa Mei, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa zaidi kuhusu jitihada za Serikali katika kulinda baioanuai ya hifadhi ya kuboresha maisha ya wananchi wanaoishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, zimebainishwa vizuri katika aya ya 65 ya kitabu cha hotuba ambacho kinapatikana kwenye vishikwambi vyetu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali itaendelea kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati, ikiwemo utalii wa fukwe, meli, mikutano, matukio, michezo na utamaduni; kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi; kuimarisha matumizi ya hifadhi wa maeneo ya kale kwa kukarabati majenzi ya kale na kuyatangaza. Pia, kuendelea na mikakati ya uongezaji wa thamani ya mazao ya misitu na mazao nyuki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya madini; Serikali itaendelea kusimamia sekta ya madini kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kusimamia masoko ya madini na vituo vya ununuzi. Vile vile, kudhibiti matukio ya utoroshaji wa madini kwa kuimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, huko mipakani, viwanja vya ndege na bandarini. Tutawezesha na kusimamia sekta ya wachimbaji wadogo na uwekezaji katika viwanda vya kusafisha dhahabu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2024, Serikali imeanzisha jumla ya masoko 42, na vituo vya ununuzi wa madini 100 katika maeneo mbalimbali, ambapo thamani ya mauzo ya madini katika masoko ya vituo vilivyoainishwa yamefikia shilingi trilioni 1.74 na kuiwezesha Serikali kunufaika na kukusanya jumla ya shilingi bilioni

121.44. Aidha, Serikali imetoa jumla ya vibali 7,775 vya kuuza madini nje ya nchi vyenye thamani ya shilingi trilioni 5.82.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu mkakati wa manufaa ya uwezeshaji wachimbaji wadogo na wakubwa katika sekta ya madini yamebainishwa katika aya ya 69 hadi aya ya 70 ya kitabu cha hotuba kilichopo kwenye vishikwambi vyetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa kwa kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya madini, ikiwemo madini ya kimkakati; uwekezaji ikiwa kuongeza thamani madini; kufanya tafiti za kina za jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege na uendelezaji wa sekta ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya nishati; umeme, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa nishati ya umeme ili kuchochea shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza miradi mbalimbali. Hadi kufikia Februari, 2024 mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ilikuwa na uwezo wa kuzalisha jumla ya megawati 2,129.8.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na changamoto za upungufu wa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme iliyokuwepo kabla ya msimu ya mvua wa *El-Nino* kuanza, upungufu wa gesi asilia katika vituo vinavyozalisha umeme kwa kutumia gesi pamoja na hitilafu kwenye mitambo ya kuzalisha umeme. Umeme unaozalishwa ulikuwa pungufu kwa megawati 410.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utoaji wa huduma ya umeme nchini katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imekamilisha mradi wa kufua umeme wa *Kinyerezi One Extension* wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 185. Mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo ambao umewezesha nchi kupata megawati 27 na hivi karibuni Serikali imefanikisha kuanza uzalishaji wa umeme kutoka mradi wa Bwawa la Julius Nyerere kutoka katika mtambo wa kwanza kati ya mitambo tisa ambayo uzalishaji wake kiasi cha megawati 235.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na miradi ya umeme ya jua ya Shinyanga megawati 150, Mto Malagarasi megawati 49.5 na Kakono megawati 87. Maelezo zaidi kuhusu uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme na uendelezaji wa gesi asilia yanapatikana katika aya ya 74, 76 na aya ya 77 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kutimiza dhamira yake ya kupeleka umeme vijijini, imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme katika vijiji vyote Tanzania Bara; ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2024, jumla ya vijiji 11,837 sawa na silimia 96.1 ya vijiji vyote 12318 vya Tanzania Bara vimeshaunganishwa umeme, ambapo mtandao wa njia za kusambaza umeme nchini umefikia kilometa 176,334.14.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali itaendelea kupeleka umeme katika vitongoji, visiwa, vituo vya afya, pampu za maji, machimbo ya madini, viwanda, shule, mahakama za mwanzo vijijini na maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala la nishati safi ya kupikia; ikiwa ni hatua ya kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia Barani Afrika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa Mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabia ya Nchi *COP28,* alizindua programu ya nishati safi ya kupikia itakayowezesha wanawake Barani Afrika *(African Women Clean Cooking Support Program)* kutumia nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa programu hiyo mnamo tarehe 9 Februari, 2024, Serikali iliandaa Kongamano la Wanawake la Nishati safi ya kupikia Jijini Dodoma ambalo lilifunguliwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kongamano hilo lililenga kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na kugawa mitaji na vitendea kazi kwa wajasiriamali wadogo wadogo wanawake kutoka mikoa yote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, mnamo tarehe 24 Machi, 2023, kupitia notisi namba 1,790, Serikali ilitoa katazo la matumizi ya kuni kwa taasisi za umma na binafsi zinazotoa huduma ya kulisha watu zaidi ya 100 ziache kutumia kuni na mkaa ifikapo tarehe 31 Januari, 2024, na utekelezaji wa katazo hilo umeanza.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kuchukua hatua zinazolenga kuhakikisha kuwa wananchi wanawezeshwa kutumia nishati safi ya kupikia, ikiwa ni pamoja na kusambaza mitungi ya gesi ya *LPG* ambapo tayari mitungi 61,400 ya *LPG* ya kilo sita (6) imesambazwa kwa wananchi hadi Februari, 2024 kati ya mitungi 70,200 iliyotarajiwa kusambazwa, sawa na asilimia 87. Usambazaji wa gesi asilia majumbani pamoja na majiko banifu uliendelea.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mnamo tarehe 24 Machi, 2024, Serikali imeidhinisha Mkakati wa Miaka 10 ya Kuhamia katika Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa Mwaka 2024/2025 hadi 2033/2034. Hatua inayofuata ni utekelezaji wa mkakati huo kwa kuhakikisha kuwa wadau wote walioainishwa wanatekeleza majukumu yao katika muda uliopangwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na kumaliza tatizo la mgao wa umeme Serikali yetu itaendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme. Kupeleka nishati vijijini, kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia; ikiwa ni pamoja na Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(LNG project)* na ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima Uganda hadi Tanga Tanzania. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza shughuli za utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia; Usambazaji wa gesi asilia viwandani katika taasisi za majumbani na kuimarisha matumizi *CNG* katika magari.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, itaendelea kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini pamoja na upatikanaji wa nishati ya

mafuta vijijini kupitia uanzishaji wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo pamoja na kuhakikisha kuwa nchi inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli pamoja na ufanisi katika kushughulikia upatikanaji wa bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ardhi; sekta hii ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi, hasa ikizingatiwa kuwa Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na maendeleo ya makazi hapa nchini. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (2018/2019 hadi 2027/2028) imewezesha upimaji wa jumla ya viwanja 46,417 kwenye mikoa 17 nchini ikijumuisha maeneo yaliyo kwenye miradi ya kimkakati. Aidha, programu hii imewezesha kutatua migogoro ya mipaka ya kiutawala ikiwa ni pamoja na mpaka wa Wilaya za Kilindi na Kiteto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi nchini; Kuendeleza sekta ya makazi; Ukamilishaji wa mwongozo wa viwango vya ujenzi wa majengo; na Kukamilisha Muswada wa Sheria ya Ujenzi ambayo itasaidia udhibiti wa ujenzi holela katika miji yetu. Aidha, itaendelea kukamilisha kazi za uthamini kwa wananchi wote wanaopisha shughuli za maendeleo, kuweka alama zinazoonekana ardhini katika mipaka ya vijiji na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, taarifa za kina kuhusu utatuzi wa migogoro utoaji wa hati miliki za ardhi na mpango wa Serikali wa ujenzi wa nyumba za gharama ya kati na nafuu hususani kupitia Mradi wa *Samia Housing Scheme* zimeainishwa katika aya ya 83 na 84 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya viwanda na biashara; Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wastani wa viwanda vya biashara nchini kwa kuandaa na kutekeleza sera, sheria, mikakati na miongozo mbalimbali. Katika mwaka 2024, Serikali imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003 na kuandaa Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji Mkataba wa Soko Huru la

Afrika. Hali kadhalika Serikali imefanya maboresho ya Sheria ya Leseni za Biashara na Kanuni zake, Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara, Sheria ya Wakala wa Vipimo na kufanya maboresho ya mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao ili kurahisha usajili.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha malengo ya nchi yanafikiwa, Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, itaweka mkazo katika uendelezaji wa miradi ya kimkakati ya viwanda; Uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo na mifugo kwa kujenga Kongani ya viwanda katika mikoa; Urasimishaji wa biashara nchini ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara wasio rasmi kunufaika na fursa zilizopo katika soko la ndani, kikanda na kimataifa; na Kujenga mifumo ya masoko na utafutaji wa masoko ya bidhaa zinazowasilishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, maelezo yanayohusu kampuni zilizosajiliwa, maandalizi ya kongani za viwanda na kutumia fursa za masoko ya kikanda na kimataifa zimeainishwa vizuri sana katika aya ya 87 na 88 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri na usafirishaji; miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni msingi wa uchumi wa Taifa hili na inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuwezesha na kurahishisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Katika kuhakikisha huduma hiyo inaboreshwa, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 iliendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, viwanja vya ndege, vivuko pamoja na majengo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizofanywa na Serikali katika ujenzi wa barabara kuu, barabara za mikoa, barabara za mijini na vijijini, madaraja ya ngazi zote na makalvati zimebainishwa vizuri katika aya ya 91 na 92 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imeendelea kutekeleza miradi ya kupunguza msongamano wa magari katika miji na majiji hapa nchini. Jumla ya shilingi bilioni 9.14 fedha za ndani na shilingi bilioni 67.44 fedha za nje zimeshatumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mzunguko wa nje wa Jiji la Dodoma yenye urefu wa kilometa 112.3. Hadi kufikia Februari, 2024 ujenzi wa sehemu ya kwanza kutoka Nala

mpaka Veyula – Mtumba – Ihumwa Bandari Kavu yenye urefu wa kilometa 52.3 umefikia asilimia 74.17, na sehemu ya pili kutoka Ihumwa Bandari Kavu kupitia Matumbulu mpaka Nala yenye urefu wa kilometa 60 utekelezaji umefikia asilimia 60.62. Ujenzi wa barabara hii unatarajiwa kukamilika ifikapo Disemba, 2024 na Machi, 2025 kwa sehemu ya kwanza na ya pili mtawalia.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya pili Jijini Dar es Salaam unaohusisha *lot* ya kwanza na ya pili. *Lot* ya kwanza inahusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 20.3 kutoka Mbagala hadi Mzunguko wa Bandari uliopo eneo la Bendera Tatu hadi Kariakoo, Sokoine hadi Zanaki, Barabara ya Kawawa hadi Magomeni na Barabara ya Chang'ombe hadi Barabara ya Kilwa utekelezaji umefikia asilimia 98.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa *lot* ya pili inayohusisha ujenzi wa majengo ikiwemo vituo viwili, yadi moja na vituo mlisho vinne umekamilika. Vilevile awamu ya tatu ya ujenzi wa barabara inayoishia Gongolamboto yenye urefu wa kilometa 23.3 umefikia asilimia 22.2. Kukamilika kwa ujenzi huo kutapunguza sana msongamano na hatimaye kuchochea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanja vya ndege na usafiri wa anga; Serikali inaendelea na ukarabati, upanuzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Iringa, Musoma, Tabora, Shinyanga, Sumbawanga na Moshi ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya hali ya hewa nchini kwa kukamilisha ufungaji wa rada mbili za hali ya hewa katika Mikoa ya Mbeya na Kigoma, kuendelea na utengenezaji wa rada mbili zitakazofungwa katika Mikoa ya Kilimanjaro na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75 na kufunga mitambo mitano ya kutoa huduma za hali ya hewa katika Viwanja vya Ndege vya Songwe, Zanzibar, Mtwara, Arusha na Songea. Aidha, imekamilisha ununuzi wa mitambo mingine mitatu ya kutoa huduma za hali ya hewa katika Viwanja vya Ndege vya Musoma, Iringa na Mpanda pamoja na kukamilisha ununuzi wa seti 20 za mitambo ya kupima hali

ya hewa inayojiendesha yenyewe *(Automatic Weather Stations)* katika Vituo vya Hali ya Hewa vilivyopo katika Viwanja vya Ndege vya Mtwara, Songea na Arusha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya reli, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya reli ya kati kwa kukamilisha ukarabati wa mabehewa ya mizigo 254 na mabehewa ya abiria 25. Vilevile inaendelea na ukarabati wa kipande cha njia ya reli kutoka Kaliua hadi Mpanda chenye urefu wa kilometa 210 ambacho ukarabati wake umefikia asilimia 10.53. Mkakati wa eneo hili ni kuijenga reli kwenda mpaka Bandarini Karema ili iweze kutoa huduma kutoka Mpanda Mjini mpaka Karema kwa njia ya reli.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafiri kwa njia ya maji. Hadi Februari 2024 imekamilisha ukarabati wa meli ya *MV* Umoja yenye uwezo wa kubeba tani 1,200 ya mizigo kutoka Bandari ya Mwanza kwenda Bandari ya Port Bell Nchini Uganda na inaendelea na ukarabati wa MT. Sangara katika Ziwa Tanganyika ambao umefikia asilimia 92. Hatua hii itarahisisha usafiri na usafirishaji wa abiria na bidhaa katika maziwa makuu na nchi jirani ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Jumla ya shilingi bilioni 24.13 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya bandari nchini kwa kufanya maboresho mbalimbali ikiwemo kuongeza kina cha mita 15.5 na upana wa mita 200 katika lango la kuingia na kugeuza meli kwa ajili ya kupokea meli kubwa katika Bandari ya Dar es Salaam. Kuongeza kina kutoka mita tatu mpaka 13 pamoja na kuboresha gati namba moja mpaka namba mbili zenye urefu wa mita 450 katika bandari ya Tanga na kukamilisha ujenzi wa gati katika bandari mpya ya Kalema Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea na ujenzi wa yadi na sakafu ngumu yenye ukubwa wa hekta tano katika Bandari Kavu ya Kwala kwa ajili ya kuhifadhi shehena za mizigo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96 pamoja na kukamilisha ujenzi wa barabara ya zege yenye urefu wa kilomita 15.5 kutoka Barabara kuu ya Morogoro

hadi Bandari Kavu ya Kwala. Katika kufikia mafanikio hayo, jumla ya Shilingi Billioni 69.243 zimeshatumika.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali itaendelea ukamilishaji wa miradi inayoendelea ikiwemo ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege, miradi ya kupunguza msongamano katika miji mikubwa, madaraja, uimarishaji wa miundombinu ya reli ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa na uendelezaji wa bandari. Hatua hii itafungua fursa za kijamii na kiuchumi katika maeneo ya utalii, kilimo, mifugo, uvuvi, madini, bandari, viwanda, mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na teknolojia ya habari nchini kwa lengo la kuongeza chachu ya maendeleo ya jamii, siasa, usalama na uchumi kwa kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia hapa ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, taarifa za kina kuhusu Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Uchumi wa Kidijitali na Uwezeshaji wa Tanzania Safari *Channel* imeainishwa katika aya ya 100 na 104 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Anuani za Makazi, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi kwa kufanya uhakiki wa taarifa za watu na makazi zilizokusanywa wakati wa Operesheni Anwani za Makazi ya Mwaka 2022. Hadi kufikia Februari, 2024, jumla ya anwani milioni 2.24 zimehakikiwa na anwani mpya 498,975 zimesajiliwa katika halmashauri 25 na kufanya idadi ya anwani zilizohakikiwa na kusajiliwa kufikia milioni 12.84. Vilevile, Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi (*NaPA*) umeunganishwa na mifumo nane ya Taasisi za Serikali ya kutolea huduma ili kuwezesha mifumo hiyo kusomana.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza maelekezo niliyoyatoa hivi karibuni kuzitaka mamlaka za Serikali za Mitaa ziandae sheria ndogondogo kwa ajili ya kulinda matumizi ya vibao vya anwani za mitaa na kufanya kaguzi za mara kwa mara ya matumizi ya vibao vya anwani ya makazi; kuongeza juhudi katika kupima, kupanga na kutoa namba za nyumba za makazi na ofisi pamoja na kuweka majina ya

mitaa katika maeneo mapya; na kuhakikisha vibali vya ujenzi vinatolewa pamoja na namba za nyumba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025 Serikali itatoa kipaumbele kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano, kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara mtandao, kuimairisha miundombinu ya uchumi wa kidijitali, kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao na kuimarisha upatikanaji wa habari. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pamoja na utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi ikiwemo ukusanyaji na uhakiki wa taarifa za anwani za makazi.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Jamii, nianze na Sekta ya Elimu; katika kuimarisha utoaji wa elimu ya msingi na sekondari, hadi Machi, 2024, jumla ya shilingi bilioni 262.62 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa shule za msingi na sekondari, ukarabati wa vyumba vya madarasa, ujenzi na ukamilishaji wa mabweni, mabwalo na uzio wa shule za msingi. Hili limechangia ongezeko la wanafunzi katika mwaka wa masomo 2024 ambapo darasa la awali walioandikishwa ni 1,450,281 sawa na asilimia 77.4 ya lengo, darasa la kwanza ni 1,743,173 sawa na asilimia 92.7 ya lengo na kidato cha kwanza wanafunzi 973,440 sawa na asilimia 89.1 ya wanafunzi waliochaguliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza fursa za elimu ya juu nchini, ambapo udahili katika vyuo vikuu umeongezeka kufikia wanafunzi 133,617 mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na wanafunzi 113,383 mwaka 2022/2023. Udahili katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo umeongezeka kutoka 171,581 mwaka 2022/2023 hadi 235,804 mwaka wa fedha 2023/2024 na katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi udahili umeongezeka kutoka 380,748 mwaka 2022/2023 hadi wanafunzi 415,131 mwaka 2023/2024. Hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa vyuo 29 vya ufundi stadi, ukarabati wa vyuo 13 vya maendeleo ya wananchi na juhudi za kuendelea na ujenzi wa miundombinu katika kampasi 14 za vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza fedha za mikopo ya elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 654 kwa mwaka 2022/2023 hadi shilingi bilioni 738.7 mwaka 2023/2024. Wanufaika wa mikopo na ruzuku

wameongezeka kutoka wanafunzi 177,615 mwaka 2022/2023 hadi wanafunzi 220,278 mwaka 2023/2024. Vilevile, Serikali imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi wenye ufaulu uliojipambanua kupitia Samia *Scholarship* ambapo jumla ya shilingi bilioni 9.74 zilitolewa kwa wanafunzi 1,276 wanaoendelea na masomo katika fani za teknolojia, uhandisi, hisabati na tiba.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imedhamiria kuinua viwango vya elimu kwa kuongeza fursa na kuboresha mazingira ya upatikanaji wa elimu kwa kila mtoto wa Kitanzania. Vilevile, itaendelea kutekeleza mitaala ya elimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu pamoja na kuimarisha ufanyaji na matumizi ya tafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji; Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji na kujenga mabwawa katika maeneo kame ili kuongeza uwezo wa nchi kuhifadhi maji ya mvua na kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi. Lengo la Serikali ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini unafikia wastani wa asilimia 95 na 85 mtawalia kwa mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, hadi Februari 2024, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini imefikia asilimia 79.6 ikilinganishwa na asilimia 77 mwezi Februari, 2023. Vilevile, kwa upande wa mijini upatikanaji wa maji umefikia asilimia 90 ikilinganishwa na asilimia 88 mwezi Februari, 2023. Mafanikio hayo yamechangiwa na kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 374 inayonufaisha wananchi wapatao 2,274,193 wanaoishi vijijini pamoja na kukamilisha utekelezaji wa miradi 70 ya maji mjini.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa mabwawa, Serikali ilipanga kujenga mabwawa makubwa ya kimkakati ya Kidunda na Farkwa, mabwawa ya kati na mabwawa madogo. Aidha, hadi Februari, 2024 ujenzi wa Bwawa la Kidunda linalogharimu shilingi bilioni 329.46 umefikia asilimia 17 na umepangwa kukamilika Juni, 2026. Vilevile, Serikali imeendelea na hatua za maandalizi ya ujenzi wa Bwawa la

Farkwa ambapo Wataalam Washauri wa kufanya mapitio ya usanifu na usimamizi wamepatikana na wanatarajiwa kukamilisha mapitio mwezi Mei, 2024. Kukamilika kwa mabwawa haya kutawezesha maji kupatikana kipindi chote cha mwaka, kuwezesha kilimo cha umwagiliaji na shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, suala la usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; Serikali imeendelea na utekelezaji wa Programu Maalum ya Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji iliyoanza mwaka 2021 ambapo inatarajia kukamilika mwaka 2035. Kupitia programu hiyo, Serikali imetambua vyanzo vya maji 3,265 vinavyohitaji kuhifadhiwa ambapo vyanzo 316 vimewekewa mipaka na vyanzo 59 vimetangazwa kuwa maeneo lindwa ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya; Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya; upatikanaji na usambazaji wa chanjo, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika ngazi zote. Katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi, kuimarisha mfumo wa ugharamiaji wa huduma za afya nchini, kuimarisha utoaji wa mafunzo ya wataalam katika Sekta ya Afya, kuimarisha Mifumo ya TEHAMA na matumizi ya takwimu na kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika eneo la afya.

Mheshimiwa Spika, taarifa za kina kuhusu masuala ya bima ya afya, kuimarisha miundombinu ya afya na upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi nimeziainisha katika aya ya 117 hadi aya ya 121.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha  2023/2024, Serikali imejipanga kuendelea kuimarisha huduma za matibabu ya ubigwa na ubigwa bobezi, kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa na pamoja na kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote. Vilevile imedhamiria kuimarisha upatikanaji wa huduma bora zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote pamoja na kuimarisha upatikanaji na udhibiti wa dawa, vifaa tiba, vifaa vyenyewe na vitendanishi.

Mheshimiwa Spika, suala la huduma kwa makundi maalum; Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa makundi maalum ikijumuisha usawa wa kijinsia, huduma kwa watu wenye ulemavu, kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto na uratibu wa mashirika yasiyo ya Kiserikali kama ilivyoainishwa katika hotuba yangu aya ya 123 hadi 132.

Mheshimiwa Spika, Suala la hali ya Siasa na Demokrasia Nchini; katika mwaka 2023/2024, Serikali inayongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kutekeleza wajibu wake kwa Watanzania kwa kuzingatia vilivyo misingi ya maridhiano *(reconciliation),* ustahamilivu *(resilience),* mageuzi *(reform)* na ujenzi mpya *(rebuild)*. Misingi hiyo ndiyo nguzo kuu ya falsafa ya uongozi wake wenye kulenga kuimarisha misingi ya amani, utawala bora na demokrasia. Misingi hii imekuwa kielelezo cha dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais kuona Serikali anayoiongoza inajenga mazingira bora ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Utekelezaji wa falsafa hiyo, ndiyo unaoongoza utekelezaji wa mipango na mikakati yote ya Serikali katika kuwaletea na kuwashirikisha wananchi kwenye maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha demokrasia nchini inaimarishwa, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa. Chimbuko la mapendekezo ya kutunga Sheria Mpya ya Uchaguzi ni kuwepo kwa maudhui yanayofanana ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 zinazosimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Sheria hizo zinasimamia uchaguzi unaoendeshwa kwa wakati mmoja na kusimamiwa na mamlaka moja ya uchaguzi ambayo ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Vilevile, kutungwa kwa Sheria hiyo ni utekelezaji wa maoni ya wadau wa uchaguzi kwamba itungwe sheria itakayoimarisha usimamizi wa uchaguzi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia ya vyama vingi nchini, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeratibu shughuli za Vyama vya Siasa kwa kuhakikisha fursa sawa

zinatolewa katika shughuli za siasa nchini. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetoa ruzuku ya jumla ya shilingi bilioni 11.7 kwa vyama vya siasa vyenye sifa ya kupata ruzuku. Hatua hii, imesaidia kuendeleza na kuimarisha uendeshaji wa shughuli za vyama vya siasa na demokrasia nchini. Sambamba na hilo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imewezeshwa kwa kupatiwa vitendea kazi vipya na shilingi bilioni 77.91 kwa ajili ya maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na uendeshaji wa chaguzi ndogo nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, uchaguzi mdogo wa Ubunge uliendeshwa katika Jimbo la Mbarali na Udiwani katika kata 51 Tanzania Bara. Chaguzi hizo zimefanyika kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo vifo na baadhi ya Waheshimiwa Madiwani kukosa sifa za kuendelea na nyadhifa hizo. Nitumie fursa hii kuvipongeza vyama vilivyoonesha ukomavu wa kisiasa kwa kushiriki uchaguzi. Kipekee nikipongeze Chama Cha Mapinduzi kwa ushindi wa Jimbo la Mbarali pamoja na viti 51 vya udiwani katika chaguzi hizo. Pia nimpongeze Mheshimiwa Bahati Mbunge wa Mbarali kwa ushindi mnono alioupata katika uchaguzi huo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 yataendelea ikiwa ni pamoja na kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kuendelea na utoaji wa elimu ya mpiga kura; kuandaa nyaraka za uchaguzi mkuu na kujenga mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya chaguzi na utoaji wa huduma za Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, suala la uratibu wa Shughuli za Serikalini Bungeni, katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Bunge imeendesha mikutano mitatu ya Bunge yaani Mkutano wa Kumi na Mbili, Kumi na Tatu na Kumi na Nne. Katika kipindi hicho, jumla ya maswali ya kawaida 531 na maswali ya nyongeza 1,784 yaliulizwa Bungeni na kujibiwa na Serikali. Aidha, maswali 23 ya papo kwa papo yaliulizwa na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako pia lilijadili na kupitisha Miswada 10 ya sheria, Maazimio manne ya Mikataba na Itifaki za Kimataifa. Vilevile, Bunge lilijadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa

Maendeleo wa mwaka 2024/2025. Sambamba na hilo Kamati za Kudumu za Bunge zilifanya uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali na ufuatiliaji wa utekelezaji wa afua za UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Ofisi ya Bunge itaendelea kusimamia shughuli za Mikutano Minne ya Bunge na Mikutano Minne ya Kamati za Kudumu za Bunge na kuratibu ushiriki wa Wabunge katika Mikutano ya Kimataifa ikiwemo Bunge la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Umoja wa Afrika na Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Aidha, Ukumbi wa Bunge utaendelea kuboreshwa pamoja na jengo la kumbi za Bunge na majengo ya ofisi.

Mheshimiwa Spika, Suala la Ulinzi na Usalama; hali ya ulinzi na usalama katika mipaka ya nchi yetu inayohusisha eneo la nchi kavu, maji na anga imeendelea kuwa shwari bila kuwepo kwa matukio ya uhasama yaliyoripotiwa. Hali hii imechangiwa na ushirikiano uliopo baina ya wananchi na vyombo vya ulinzi na usalama katika kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama nchini inaendelea kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa. Jeshi letu limeendelea kuwa na vikosi vya ulinzi na Maafisa Wanadhimu na Makamanda kwenye operesheni za ulinzi wa amani katika Nchi mbalimbali duniani ikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan, Sudan Kusini, Lebanon na Jamhuri ya Afrika ya Kati. Aidha, katika kuimarisha mifumo ya utendaji kazi za ulinzi na usalama wa raia na mali zao nchini, Jeshi la Polisi limeimarisha mifumo ya utendaji kazi kwa kuifikia jamii katika ngazi za mitaa na vijiji kwa kuwapanga Askari Kata katika Kata 3,956 na Shehia 388.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kuviimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia zana bora, vitendea kazi vya kisasa, mafunzo pamoja na kuimarisha Mashirika na Taasisi za Utafiti wa masuala ya kijeshi. Vilevile, kuimarisha ushiriki wa

Majeshi yetu kwenye masuala ya ulinzi na usalama kwenye miamvuli ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya za Kikanda na nchi mbalimbali katika nyanja za kijeshi na kiulinzi na kuendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura.

Mheshimiwa Spika, taarifa zaidi kuhusu vitambulisho vya uraia na mpango wa Serikali wa usajili wa watoto wanaozaliwa zimeelezwa katika aya ya 143 na aya ya 144 iliyo katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Masuala ya Kazi na Wafanyakazi; Serikali imeendelea kuimarisha masuala ya kazi na wafanyakazi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikijumuisha usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kikazi, kuimarisha vyama vya wafanyakazi na waajiri wao, kuimarisha usalama na afya mahali pa kazi, haki na uwajibikaji wa wafanyakazi wa kina wa jamii na ukuzaji wa fursa za ajira na ujuzi. Maelezo ya kina kuhusu hatua zilizochukuliwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwenye sekta hii ya kazi na ajira kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 imeanishwa katika hotuba yangu kuanzia aya 146 hadi 166.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza kipindi cha pili cha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Awamu ya Tatu ya *TASAF* katika maeneo yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Mpango huu unaendelea kuwezesha kaya za walengwa kutumia fursa za kuongeza kipato, huduma za jamii na uchumi na kuwekeza katika kuendeleza na kulinda watoto katika kaya hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, jumla ya shilingi bilioni 164.31 zimehawilishwa kwa kaya za walengwa 1,336,600 katika halmashauri 184 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar. Aidha, jumla ya halmashauri 184 za Tanzania Bara na wilaya zote za Zanzibar zimeingizwa katika malipo ya njia ya kielektroniki ambayo yanawezesha walengwa kufikiwa kwa haraka sana kwa gharama nafuu na uendeshaji wake unakuwa rahisi.

Mheshimiwa Spika, taarifa zaidi kuhusu uhakiki wa kaya za walengwa zinazoimarika kiuchumi na vikundi vinavyowezeshwa vimeelezwa katika aya ya 169 – 170 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inatarajia kufanya tathmini ya mwisho ya kupima matokeo na manufaa ya mpango huo ili kuangalia namna ambavyo uwezekezaji wake wa Serikali umeleta tija katika kuwahudumia wananchi kuweza kuondokana na hali duni na kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na jitihada za uwezeshaji na uendelezaji vijana kiuchumi ili kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo, pia, kujipatia ajira na kujikwamua kiuchumi. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.27 ilitolewa kwa miradi 56 ya vijana, elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara na vijana 2,800 pia wameweza kushirikishwa. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 ambayo itawezesha masuala ya vijana kuratibiwa na kutekelezwa na wadau mbalimbali kwa lengo la kuinua ustawi wa vijana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kusimamia masuala ya malezi na makuzi kwa vijana wetu hapa nchini, kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kusimamia na kuratibu masuala ya maendeleo ya vijana, kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kutoa mikopo ili waweze kujiajiri na kutengeneza fursa za ajira kwa vijana wenzao.

Mheshimiwa Spika, pia, tunaratibu mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi wa biashara na stadi za maisha kwa makundi maalum ya vijana, kusimamia uundwaji wa vikundi vya vijana vya uzalishaji mali, na kuandaa mfumo thabiti wa utaratibu wa shughuli za maendeleo ya vijana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Masuala Mtambuka, naanza na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Ikumbukwe kwamba mnamo tarehe 9 Desemba, 2023, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua rasmi mchakato wa maandalizi ya Dira Mpya ya Maendeleo ya Taifa. Dira hiyo itatoa

mwongozo wa mwelekeo wa maendeleo ya nchi kwa kipindi cha miaka zaidi ya 25 ijayo.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa rai kwenu Waheshimiwa Wabunge na kwa Watanzania wote kushiriki kikamilifu katika zoezi la kutoa maoni ambayo yatatuwezesha kuchangia na kuweza kuwa na Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo itakayobeba maono ya muda mrefu na kujumuisha masuala yote muhimu kwa ajili ya kuwa na maendeleo endelevu yenye kuzingatia ustawi wa Jamii ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa mwaka 2024 kutakuwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Serikali inaendelea na maandalizi ya uchaguzi huo ambapo hadi Februari, 2024 imeshatoa shilingi bilioni 5.1 kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi huo ikiwemo uhakiki wa maeneo ya uchaguzi, kuandaa Tangazo la Serikali, kuandaa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na kuhakiki vituo na vifaa vya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na misingi ya kidemokrasia. Aidha, nitoe wito kwa wadau wote wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa kushiriki kikamilifu katika mchakato wote wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kuwezesha uchaguzi huo kuwa wa mafanikio.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mapambano Dhidi ya Rushwa; Serikali inaendelea kupambana na kudhibiti vitendo vya rushwa na ufisadi nchini ambapo hadi kufikia Februari, 2024 kesi 767 zimeendeshwa katika mahakama mbalimbali. Kati ya kesi hizo, kesi 254 ziliamuliwa mahakamani ambapo Jamhuri ilishinda kesi 169 na watuhumiwa kuhukumiwa kifungo na kulipa faini. Aidha, shilingi bilioni 14.45 ziliokolewa kutokana na operesheni za uchunguzi zilizofanyika katika maeneo mbalimbali nchini ambapo shilingi bilioni 13.79 ni fedha taslimu zilizorejeshwa Serikalini na shilingi milioni 789.78 zilidhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi kwa kuelimisha umma kuhusu madhara ya rushwa, kuchambua na kuimarisha mifumo ya utendaji kazi na utoaji huduma. Pia tutaendelea na uchunguzi na kuwafikisha

mahakamani wale wote watakaokuwa wamepatikana na tuhuma za rushwa na ufisadi na kuendelea kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuongeza ufanisi katika kukabiliana na rushwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, maelezo zaidi kuhusu juhudi za TAKUKURU na kupambana na rushwa pamoja na matokeo ya taarifa ya *Transparency International* yameelezwa katika aya ya 179 na 180 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuratibu na kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI nchini. Katika mwaka 2023/2024, Serikali imezindua Taarifa za Matokeo ya Utafiti wa Athari za UKIMWI Tanzania kwa mwaka 2022/2023. Utafiti huu umeonesha matokeo chanya yaliyofikiwa na nchi yetu katika mwitikio dhidi ya UKIMWI ikiwemo kupungua kwa kiwango cha ushamiri wa VVU kutoka asilimia 4.7 mwaka 2016/2017 hadi asilimia 4.4 mwaka 2022/2023 pamoja na kupungua kwa maambukizi mapya kutoka watu 87,013 mwaka 2016/2017 hadi watu 60,000 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ipo kwenye mwelekeo mzuri wa kufikia shabaha ya kitaifa na kimataifa za 95, 95, 95 ifikapo 2026. Utafiti huo umebainisha kuwa asilimia 95 ya kwanza inayohusu watu wote wanaoishi na VVU kupima na kujua hali zao na maambukizi imefikia asilimia 82. Asilimia 95 ya pili inayohusu tiba za WAVIU waliotambua hali zao na utambuzi huu umefikia asilimia 97 na asilimilia 95 ya tatu inayohusu Ufubavu wa Virusi kwa WAVIU wanaoendelea na tiba na yenyewe imefikia asilimia 94.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2024/2025, Serikali itaendeleza jitihada za mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo kutoa fedha za mitaji kwa wasichana balehe na wanawake vijana, kutekeleza programu za kuhamasisha upimaji wa hiari, kufanya Mapitio ya Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2001, kuwezesha shughuli za uendeshaji wa Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI, kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI na kutoa elimu kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi ya kupata VVU na kujenga uwezo wa vijana viongozi wa kisiasa, dini, kimila na mitandao ya makundi maalum yaliyo katika mazingira ya

hatarishi ya kupata maambukizi ili kushughulikia mila na desturi zinazosababisha unyanyapaa na ubaguzi wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mafanikio makubwa katika udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya ambapo hadi Desemba 2023, jumla ya kilogramu milioni 1.96 za dawa za kulevya zilikamatwa kutoka kwa watuhumiwa 10,522. Aidha, dawa tiba zenye asili ya kulevya kilogramu 1.59 na lita 61.67 zilikamatwa. Kiasi hicho kilichokamatwa ni zaidi ya jumla ya dawa za kulevya zilizokamatwa nchini katika kipindi cha miaka 11 kuanzia mwaka 2012 hadi 2022 ambazo ni kilogramu 660,465.4. Mafanikio haya yameipa heshima nchi yetu kimataifa kwa kupewa tuzo mbalimbali kutokana na udhibiti ulioonyesha ufanisi mkubwa wa ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanikiwa kuteketeza ekari 2,389 za mashamba ya bangi katika Mikoa ya Arusha, ekari 1,093 ya bangi maarufu ijulikanayo kama "Cha Arusha", Morogoro ekari 489, Mara ekari 807 na ekari 535 za mashamba ya mirungi katika Mkoa wa Kilimanjaro. Vilevile, ulifanyika ukaguzi kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa biashara ya kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Ukaguzi huo ulifanyika katika maeneo mbalimbali 734 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Songwe, Shinyanga, Dodoma, Kilimanjaro na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kupitia mifumo ya kielektroniki, Serikali ilifanikiwa kuzuia kemikali bashirifu kilogramu 157,738.55 na lita 1,000 zilizokuwa zikiingizwa kinyume cha sheria ambazo kama zingechepushwa zingeweza kutumika kutengenezea dawa za kulevya. Pia, juhudi hizi zimekwenda sambamba na uzinduzi wa Mwongozo wa Uelimishaji kuhusu Rushwa na Dawa za Kulevya utakaotumika kwenye klabu za kupinga rushwa na dawa za kulevya shuleni na vyuoni, kukamilisha Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2023 na kuanzisha Maabara ya Uchunguzi na Sayansi Jinai.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kutekeleza afua za

kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya nchini, kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya, kupunguza madhara yanayosababishwa na utumiaji wa dawa za kulevya na kuboresha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Uratibu wa Maafa; Serikali imeendelea kuhakikisha shughuli za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga na kujiandaa kwa ajili ya maafa yanayoweza kutokea zinatekelezwa kikamilifu. Kufuatia taarifa za tahadhari zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kuhusu kutokea kwa mvua za *El-Nino*, Serikali iliandaa Mpango wa Taifa wa Dharura wa Kukabiliana na Madhara ya *El-Nino* kwa kipindi cha Septemba, 2023 mpaka Juni, 2024. Kupitia mpango huo, Kamati za Usimamizi wa Maafa za Mikoa 18 na timu za utayari zilijengewa uwezo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Januari, 2024 zikijumuisha Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Mara, Geita, Kagera, Kigoma, Lindi, Mtwara, Ruvuma na Tanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuratibu na kutoa huduma za kibinadamu wakati wa maafa ikiwemo makazi ya muda, chakula, vifaa vya ujenzi, vifaa vya malazi, vifaa vya usafi, matibabu na huduma za kisaikolojia katika maeneo mbalimbali yaliyokumbwa na maafa hapa nchini. Katika mwaka 2023/2024, ufuatiliaji wote wa hali ya majanga na uratibu wa misaada ya kibinadamu umefanyika katika Wilaya za Ilala, Kinondoni, Temeke, Kigamboni, Ubungo, Kilosa, Same, Moshi, Hai, Muleba, Bukoba, Mbarali, Nyang'wale, Mbogwe, Chato, Liwale, Shinyanga, Hanang, Masasi, Mbarali, Nachingwea, Ruangwa na Kakonko. Vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa maghala mawili ya kuhifadhi vifaa vya misaada ya kibinadamu na kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia 37.

Mheshimiwa Spika, sote tumeshuhudia uratibu madhubuti wa Serikali katika maafa yaliyotokea tarehe 3 Desemba, 2023 Wilayani Hanang, Mkoa wa Manyara kufuatia maporomoko ya udongo ulioambatana na mawe, miti, magogo na matope. Maafa hayo yalisababisha madhara mbalimbali ikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa miundombinu, makazi na mazingira. Serikali ilichukua hatua

mbalimbali za kukabiliana na kurejesha hali ikiwemo kufanya uokoaji, kuanzisha kambi za muda kwa ajili ya waathirika, kugawa misaada ya kibinadamu na vyakula, kutoa huduma bure kwa majeruhi, kutoa msaada wa kisaikolojia kwa waathirika, kugharamia mazishi ya watu wote waliopoteza maisha pamoja na kutoa rambirambi kwa wafiwa.

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali imefanya uratibu wa urejeshaji hali kwa wafanyabiashara waliokuwa na mikopo kupitia taasisi za kifedha walizokopa ambapo baadhi yao mikopo imelipwa na wengine waliongezewa muda wa urejeshaji wa mkopo hiyo kwenye maeneo haya ambayo yamepata madhara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa maafa nchini ili kuongeza ustahimilivu wa jamii dhidi ya majanga kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya uokoaji na huduma za kibinadamu ili kuongeza utayari wa kukabiliana na maafa hapa nchini. Vilevile Serikali itaendelea kuzijengea uwezo Timu na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi za mikoa na wilaya, kutoa elimu kwa umma na kukiwezesha Kituo cha Taifa cha Mawasiliano na Dharura kufanya ufuatiliaji wa hali ya maafa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa masuala mtambuka, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika uratibu wa utekelezaji wa mikakati ya kuimarisha hali ya lishe nchini, kuboresha uratibu wa shughuli za utekelezaji wa usimamizi wa mazingira ikiwemo utekelezaji wa sera za mikakati ya Kitaifa na kuimarisha ushiriki katika mikutano ya kimataifa kuhusu mazingira, uchumi wa bluu, utawala bora, ikijumlisha uboreshaji wa mifumo ya uendeshaji wa taasisi za haki jinai nchini na vilevile, uratibu wa utekelezaji wa miradi na mikakati ya kuimarisha matumizi ya mifumo ya *TEHAMA*.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mikakati na mafanikio yaliyopatikana katika maeneo hayo, pamoja na maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji katika mwaka wa 2024/2025 yamebainishwa katika aya ya 193 hadi 207.

Mheshimiwa Spika, wakati tukielekea kuadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Serikali imeendelea kuchukua

hatua madhubuti za kuimarisha Muungano kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili ikiwa ni pamoja na kuratibu vikao vya Kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali zote zina nia ya dhati na thabiti ya kuhakikisha hoja zote za Muungano zilizobaki na zitakazojitokeza zinashughulikiwa kwa ushirikiano mkubwa kwa lengo la kuulinda na kuudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inaendelea na maandalizi ya sherehe za miaka 60 ya Muungano ambapo uzinduzi wa sherehe hizo utafanyika Zanzibar na kilele cha maadhimisho hayo kufanyika katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, napenda kutoa wito kwa taasisi zote za Serikali na sekta binafsi kuendelea kushiriki kikamilifu katika maandalizi na maadhimisho hayo ya miaka 60 ya Muungano wetu wa kipekee na adhimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itaendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo zinazotekelezwa pande zote mbili za Muungano kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na mahusiano ya kimataifa na kikanda. Katika kuimarisha mahusiano na ushirikiano na mataifa mengine duniani, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki katika shughuli mbalimbali za kikanda na kimataifa ili kuimarisha utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi kwa lengo la kuiwezesha nchi yetu kulinda na kutetea maslahi yake kisiasa, kijamii na kiuchumi ndani na nje ya mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali iliratibu ushiriki wa nchi katika majukwaa mbalimbali ya kikanda na kimataifa na ziara za kikazi za kimataifa za viongozi wakuu ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine walitembelea nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara hizo, nchi imenufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii kama vile masoko ya bidhaa za kilimo na mifugo zilizozalishwa hapa nchini, kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka nje, ongezeko la wafanyabiashara na wawekezaji kutoka nje na pia umevutia uwekezaji wa mitaji na teknolojia, tuna miradi mikubwa na ya kati, upatikanaji wa misaada na kuwezesha Watanzania kunufaika na ajira na ufadhili wa masomo ya ughaibuni.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki pia,Serikali iliratibu ziara za Viongozi Wakuu kutoka Mataifa mengine na wawakilishi wa mashirika ya kikanda na kimataifa kutembelea nchini. Ziara hizi zimesaidia kuimarisha uhusiano baina ya nchi yetu na mataifa mengine duniani. Orodha ya viongozi waliofanya ziara nchini, imebainishwa katika aya ya 213 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado ina nia ya dhati ya kutoa hadhi maalum kwa *Diaspora* ambao ni raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania kwa kuzingatia maombi waliyowasilisha Serikalini. Katika kutekeleza suala hili, mapitio ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje yamejumuisha masuala ya *Diaspora*. Aidha, ili kufanikisha utoaji wa huduma na hadhi maalum, Serikali pamoja na masuala mengine, imepanga kuweka mifumo ya utambuzi na vigezo vitakavyozingatiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza kwa vitendo zoezi la Serikali kuhamia Dodoma ili kuhakikisha huduma za Serikali zinatolewa kwa urahisi na ufanisi zaidi katika Makao Makuu ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza hilo, katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya ofisi za Wizara na taasisi pamoja na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya barabara za kisasa katika Mji wa Serikali pale Mtumba. Pia ujenzi wa majengo ya ofisi wa awamu ya pili katika mji huo huo umefikia wastani wa asilimia 75.5, ambapo tayari ofisi na Wizara tatu zimeshahamia katika majengo mapya na ni matarajio yetu kuwa ofisi za Wizara zilizobaki zitahamia katika majengo mapya ifikapo mwishoni mwa Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi katika Mji wa Serikali ikijumuisha ujenzi wa mfumo wa usambazaji umeme wa chini ya ardhi, huduma za TEHAMA na majitaka. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 27.59 zimelipwa kwa ajili ya malipo ya fidia ya wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya kuongeza eneo litakalotumika kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali itaendelea kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya ofisi za Wizara na taasisi pamoja na miundombinu wezeshi katika mji huo. Vilevile itaanza maandalizi ya ujenzi wa awamu ya tatu na mwisho ya ofisi za Wizara na taasisi, eneo lililotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Serikali pamoja na uendelezaji wa miradi ya kimkakati katika Makao Makuu ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Sanaa, Utamaduni na Michezo; Serikali kwa kutambua umuhimu wa kukuza utamaduni, sanaa na michezo imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha sekta hizo kwa kuzingatia kuwa sekta hizo ni chachu ya kuendeleza utamaduni wa Mtanzania, utambulisho wa Taifa, chanzo kikubwa cha ajira, kuimarisha afya pamoja na kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kukuza Lugha ya Kiswahili Kimataifa, Serikali imeanzisha vituo vipya viwili vya kufundisha Kiswahili kwa wageni katika Balozi zetu nchini Ufaransa na Uturuki na vituo tisa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Arusha. Jitihada hizo zimewezesha nchi yetu kuwa na jumla ya vituo 44 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni. Mkakati uliopo ni kuwa na vituo vya kufundisha Kiswahili katika Balozi zote za Tanzania kama njia ya kubidhaisha Kiswahili chetu Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, imeendelea kuimarisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili kuwawezesha wasanii kuendeleza kazi zao kwa kuwapa mikopo na elimu ya ujasiriamali. Hadi kufikia Februari, 2024, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.39 ilitolewa kwa Miradi 113 ya Utamaduni na Sanaa ambapo miradi hiyo imewanufaisha

wasanii 230,685, ambapo kati ya hao wanawake ni 131,492 sawa na asilimia 57 na wanaume ni 99,193 sawa na asilimia 43.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa na maono, kuboresha na kuhamasisha maendeleo ya michezo hapa nchini. Kufuatia juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika michezo sote tumeshuhudia Timu ya Taifa ya Wanaume ikifanikiwa kufuzu na kushiriki mashindano ya *AFCON* ya mwaka 2023 yaliyofanyika Januari na Februari, 2024 Nchini Ivory Coast pamoja na Timu ya Taifa ya Wanawake ya Mpira wa Miguu *Twiga Stars* kufuzu kucheza mashindano ya *WAFCON* yanayotarajiwa kufanyika Juni, 2024, Nchini Morocco. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutoa motisha kwa vilabu vya ndani vinavyoshiriki mashindano ya kimataifa kupitia Goli la Mama, ambapo amekuwa akitoa shilingi milioni Tano kwa kila goli linalofungwa katika hatua ya makundi na shilingi milioni Kumi kuanzia hatua ya robo fainali. Sote tumeshuhudia *Simba Sports Club* almaarufu *Wekundu wa Msimbazi* na *Young Africans Sports Club* almaarufu *Timu ya Wananchi* wakijitwalia shilingi milioni 45 kila mmoja katika hatua ya makundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Tanzania imepata mafanikio makubwa kwa kuwa nchi pekee iliyoingiza timu mbili kwenye hatua ya robo fainali ya Mashindano ya Klabu Bingwa Afrika, ikiwa ni kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania. Kufanya vizuri kwa timu zetu katika mashindano hayo kumesaidia kulitangaza soka letu kimataifa. Aidha, kufuatia matokeo yao ya michezo ya awali, ningependa kutumia fursa hii kuzitakia klabu hizo kila la heri katika michezo ya marudiano itakayochezwa tarehe 5 Aprili, 2024.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; nikihitimisha hotuba yangu, ningependa kutoa rai kwa Watanzania wote kuendelea kuliombea Taifa hususani tunapoanza Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu pamoja na kuunga mkono juhudi za Serikali za kuwaletea maendeleo katika sekta zote. Aidha, Ofisi ya Waziri

Mkuu itaendelea kuratibu na kufuatilia shughuli mbalimbali za Serikali kwa karibu ili kuhakikisha malengo tuliyojiwekea katika Dira ya Taifa ambayo utekelezaji wake unafikia ukomo mwaka 2025 yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa kipindi kilichopita na mwelekeo wa kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2024/2025, napenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Kuendelea na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa kuhakikisha wananchi na viongozi wanapata muda wa kutosha kujadili na kutoa maoni pamoja na kuzingatia maoni hayo katika rasimu ya Dira;

(ii) Kuendelea kuimarisha jitihada za upatikanaji wa umeme wa uhakika ikiwa ni pamoja na kuongeza uwekezaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati kwa wakati katika maeneo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya umeme ili kuhakikisha nchi inakuwa na huduma za uhakika na zitakazovutia uwekezaji;

(iii) Kuimarisha juhudi za kuongeza uzalishaji wa sukari nchini pamoja na kuvutia uwekezaji katika eneo hilo ili kuipatia ufumbuzi wa kudumu changamoto ya upatikanaji wa sukari nchini;

(iv) Viongozi wa Dini na wananchi kwa ujumla tuendelee kuliombea Taifa hili wakati linaingia kwenye kipindi cha maandalizi ya uchaguzi ili kuwa na amani, utulivu na mshikamano uweze kuimarika. Aidha, natoa rai kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika hatua za maandalizi na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024 ili kutumia haki yao ya kikatiba. Vilevile kuanza vyema maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025;

(v) Kuimarisha juhudi za ukusanyaji mapato ili kuongeza uwezo wa Taifa kujitegemea, pamoja na kubana matumizi katika maeneo yasiyokuwa na tija katika utoaji wa huduma kwa wananchi;

(vi) Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi za Utafiti, Taasisi za Elimu, Taasisi Binafsi na Wadau kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na

Makazi ya Mwaka 2022 wakati wa maandalizi ya miradi, programu na mipango mbalimbali na kuhakikisha taarifa ya anwani za makazi zinakuwa sehemu ya taarifa ya msingi katika kuandaa mpango kazi wa taasisi husika wakati wa kutoa na kupokea huduma.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025; kwa mwaka 2024/2025, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 350,988,412,000, kati ya fedha hizo, shilingi 146,393,990,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 204,594,422,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vilevile naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi181,805,233,000 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, shilingi172,124,423,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 9,680,810,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru kwa haya uliyotueleza yaliyofanyika na yanayotarajiwa kufanyika. Waheshimiwa Wabunge, nimeona baadhi yenu mmekaa wakati na ninyi bajeti yenu ameisema Waziri Mkuu, hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na utaratibu wetu, lakini ataingia Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea na Wenyeviti watakaokuwa wakiendelea kutoa Taarifa kutoka kwenye Kamati zetu kuhusiana na yale ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameyaleta

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Wako wageni wawili ambao wamefika pia na wako Jukwaa la Spika, walikuwa hawajatajwa kabla na hawa nao ni wageni wa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa na huyu ni Ndugu Ramadhani Kailima ambaye ni Mkurugenzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nafikiri nirudie cheo chake kwa sababu jina la Tume limebadilika, Mkurugenzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Yupo pia ndugu Abdul-Razaq Badru ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF)*. Karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimpishe Mheshimiwa Naibu Spika.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na Mawanda ya Uchambuzi; katika uchambuzi huo Kamati ilipitia jumla ya mafungu matano, nayo ni: -

(i) Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu;

(ii) Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu;

(iii) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa;

(iv) Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi; na

(v) Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na sehemu ya kwanza inayohusu uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli. Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 19,186,000,000; kati ya fedha hizo Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ililenga kukusanya shilingi 19,000,000,000; Fungu Na. 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi ililenga kukusanya shilingi 150,000,000; na Fungu Na. 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ililenga kukusanya shilingi 36,000,000.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha yafuatayo:-

(i) Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu imekusanya chini ya lengo, hadi kufika Februari, 2024 makusanyo ni shilingi 926,880,940.54 sawa na asilimia 4.87 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu hili lililenga kukusanya shilingi 19,000,000,000 kutoka kwenye Idara ya Mpiga Chapa wa Nyaraka za Serikali. Kamati ilielezwa kuwa kutokufikiwa kwa lengo ni kutokana na kuchelewa kuwasili kwa mashine nne kati ya saba zilizoagizwa nje ya nchi kwa ajili ya shughuli za uchapishaji. Aidha, mpango uliopo wa Serikali ni ukamilishaji wa ununuzi wa mashine mpya tatu, ambazo zitatumika kuchapisha nyaraka za uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa

mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, hivyo makusanyo yanakadiriwa kuongezeka kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo, jumla ya shilingi 1,054,142,370.54 sawa na asilimia 5.49 tu ya makusanyo yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu zilikusanywa na Ofisi hiyo. Uwiano huu haujafikia lengo la makusanyo ambalo ni asilimia 66.6 hadi kufika Februari, 2024.

(ii) Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi, hadi kufika mwezi Februari, 2024 imekusanya asilimia 84.17 ya lengo.

(iii) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa hawajafikia lengo la makusanyo kwa kuwa hadi kufika Februari, 2024 Ofisi hiyo imekusanya shilingi 1,000,000 tu sawa na asilimia 2.71 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Fungu hili unategemea vyanzo viwili ambavyo ni ada ya Usajili wa Vyama vya Siasa vya muda mrefu na muda mfupi na Ukodishaji wa Mgahawa na Kumbi za Mikutano katika Jengo jipya. Hadi kufikia Februari, 2024 Vyama vilivyoomba usajili havijatimiza masharti ya kupata usajili, pia kutokamilika kwa ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa linaloendelea kujengwa, hivyo ni chama kimoja tu ambacho kililipa ada ya usajili wa muda kwa kiasi cha shilingi 1,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kuwa, makusanyo hafifu ya baadhi ya taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, yanaweza kutafsiriwa kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi au vyanzo vya maduhuli vilivyoanishwa havikuwa vya uhakika na si endelevu. Kwa msingi huo, ni vyema Wizara na taasisi zake zote kuzingatia uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli.  Mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu unaoneshwa katika jedwali namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, inahusu uchambuzi wa matumizi ya Bajeti; Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; kwa

Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 29,940,040,000. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 25.8 zilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 4.07 zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari 2024, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 32.025 sawa na asilimia 106.96 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 22.247 sawa na asilimia 86 zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 5.009 sawa na asilimia 123 zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa sababu ya ongezeko ya fedha zilizopokelewa kwenye fungu hili ni kutokana na fungu hili kupokea shilingi 4,768,672,130.27 nje ya bajeti ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya maadhimisho na sherehe za kitaifa; mazishi ya viongozi wa kitaifa; madeni ya wazabuni; uandaaji wa mipango ya halmashauri ya kukabiliana na maafa; na urejeshaji hali kutokana na maafa yaliyotokea Wilaya ya Hanang, pamoja na kupokea shilingi 938,326,891 ya Miradi ya Maendeleo nje ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 25 Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 17,440,724,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo shilingi 1,706,724,000 ilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 15,734,000,000 ilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu ilipokea jumla ya shilingi 18,380,416,740.6 sawa na asilimia 105.38 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 17,461,760,740.61 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 110.9 na shilingi 918,656,000 sawa na asilima 53.8 zilipokelewa kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa sababu ya kupokea fedha nyingi kuliko bajeti ilioidhinishwa ni kutokana na gharama za uendeshaji wa Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu ambayo haikuwa imetengewa fedha wakati wa uidhinishwaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 24.661 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 23.721 ilitengwa kwa matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 1.136 ni mishahara na shilingi bilioni 5.021 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 17.56 ilitengwa kwa ajili ya ruzuku ya vyama vya siasa. Aidha, shilingi 940,000,000 ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2024, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilipokea jumla ya shilingi 15,727,984,210.47 sawa na asilimia 63.77. Kati ya fedha hizo. Shilingi15,721,984,210.47 sawa na asilimia 66.3 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 6,000,000 sawa na asilimia 0.63% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha vyama sita vya siasa vyenye sifa ya kupata ruzuku vilipatiwa ruzuku kama ifuatavyo: -

a) Chama Cha Mapinduzi (CCM);

b) *Alliance for Change and Transparency (ACT*-Wazalendo);

c) *National Convention for Construction and Reform* (NCCR – Mageuzi);

d) *The Civic United Front (CUF)* Chama cha Wananchi;

e) *Democratic Party (DP);* na

f) Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 91 - Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 24,406,490,000; kati ya fedha hizo shilingi 15,631,318,000 ilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 8,775,172,000 ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo shilingi 2,000,000,000 fedha za ndani zilitengwa kwa ajili ya

ujenzi wa awali wa Kituo cha Taifa cha Utengamao katika eneo la Itega, Dodoma na shilingi 6,775,172,000 fedha za nje kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya UKIMWI kwa wanaojidunga na wanaotumia dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2024, Ofisi hiyo ilipokea jumla ya shilingi 11,354,409,135.92 sawa na asilimia 46.52. Kati ya fedha hizo, shilingi 10,384,409,135.92 sawa na asilimia 66.43 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 970,000,000 sawa na asilimia 14.3 fedha za nje zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Fungu Na. 61 - Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi; kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 10,870,559,000. Kati ya fedha hizo shilingi 9,930,559,000 ilitengwa kwa matumizi ya kawaida, ambapo shilingi 4,212,026,000 ni mishahara na shilingi 5,718,533,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 940,000,000 ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2024, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea jumla ya shilingi 84,097,998,941 sawa na ongezeko la asilimia 773.59 ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 6.176 sawa na asilimia 62.22 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 77.915 sawa na asilimia 8,288.86 zilipokelewa nje ya ukomo wa bajeti. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 6.899 ni kwa ajili ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na.2 na Jedwali Na.3. Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ni wa kuridhisha, isipokuwa katika miradi ifuatayo:-

(a) Mradi wa Mfuko wa Dunia wa Kuzuia Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI *(Global Fund HIV/AIDS Prevention Project),* Wizara hadi kufikia Februari, 2024 imepokea kiasi cha shilingi 970,000,000 sawa na asilimia 14.31% ya fedha za nje zilizoidhinishwa,

mwendendo wa upatikanaji wa fedha kwenye mradi huu siyo wa kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa fedha za mradi huu zinatolewa na wafadhili. Aidha, Wizara inaendelea na jitihada za ufuatiliaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu linahusu Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya taarifa hii inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ninaanza na maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 12,054,000,000 ikilinganishwa na shilingi 19,186,000,000 katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ambavyo imeainishwa katika Jedwali Na.5. Hii ni sawa na upungufu wa asilimia 37.16 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inahusu matumizi ya kawaida; katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 111,766,168,000 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 18,603,908,000 ni mishahara na shilingi 17,563,000,000 ni ruzuku kwa vyama vya siasa na shilingi 75,579,260,000 ni matumizi mengineyo kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa asilimia 20.7 ukilinganisha na mwaka wa fedha unaoisha ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ndani ya ukomo wa bajeti ilikuwa shilingi

92,572,370,000. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya fedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma pamoja na kuanzishwa kwa Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri, ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya Kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu inahusu Miradi ya Maendeleo; katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 176,376,529,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 171,107,959,000 ni fedha za ndani na shilingi 5,268,570,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa shilingi 161,650,035,000 sawa na asilimia 1,097.7 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha, sababu ya ongezeko hilo imechangiwa na ongezeko la bajeti ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, Kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani. Kwa umahsusi, Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya usimamizi mahiri, hodari na shupavu wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mara ya kwanza kutenga fedha za maandalizi ya uchaguzi mkuu kwa kutumia fedha za ndani bila utegemezi wowote wa fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kwamba ipo haja ya Serikali kutenga fedha za ndani katika mradi wa programu ya kuendeleza kilimo na uvuvi kwani hadi kufikia Februari, 2024, mradi huu ulipokea asilimia 57.17 tu ya fedha za nje zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ya taarifa inahusu maoni na ushauri wa Kamati, maoni yetu ya jumla. Kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa Mafungu yote kuwa Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambao unaakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mahsusi fungu kwa fungu; kuhusu Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Serikali ihakikishe kwamba, fedha zinapatikana kikamilifu kwenye mradi namba 4,429 programu ya kuendeleza kilimo na uvuvi. Mbili Serikali ihakikishe kwamba ununuzi wa mashine za uchapaji pamoja na matengenezo ya mashine chakavu unakamilika kwa wakati kabla ya kuanza kwa maandalizi ya chaguzi za Serikali za Mitaa 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; Ofisi hii iweke mpango endelevu na mahsusi wa matumizi ya jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inayoendana na vipaumbele vya Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kukushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu kwa kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wa Shughuli za Serikali Bungeni na kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Waziri na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ambao wanamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake katika ofisi hiyo. Kwa umuhimu wao, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

(i) Mhe. Dkt. Doto Biteko Naibu Waziri Mkuu

(ii) Mhe. Jenista Joakim Mhagama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu

(iii) Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Dkt. Jim Yonazi; Mheshimiwa Jaji Francis S. Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa; Mheshimiwa Jaji Jacobs Mwambegele, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ndugu Kailima Ramadhan; na Ndugu Aretas James Lyimo, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1. Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

d) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya tano ni Hitimisho.

## 1.2. Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(c) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

## 1.3. Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu matano (5) ambayo ni: -

a) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu;

b) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu;

c) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa;

d) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi; na

e) **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu matano yaliyochambuliwa kama ifuatavyo; -

(a) Makusanyo ya maduhuli;

(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu;

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(e) Ulinganisho wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

### 2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 19,186,000,000**, kati ya fedha hizo **Fungu Na. 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ililenga kukusanya **Sh. 19,000,000,000**, **Fungu Na. 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi ililenga kukusanya **150,000,000** na **Fungu Na. 27** - Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa ililenga kukusanya **36,000,000**.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha yafuatayo:-

(a) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu imekusanya chini ya lengo, hadi kufika Februari, 2024 makusanyo ni **Sh. 926,880,940.54** sawa na asilimia **4.87** tu.

**Mheshimiwa Spika**, Fungu hili lililenga kukusanya **Sh. 19,000,000,000** kutoka kwenye Idara ya Mpiga chapa wa Nyaraka za Serikali. Kamati ilielezwa kuwa kutokufikiwa kwa lengo ni kutokana na kuchelewa kuwasili kwa mashine nne (4) kati ya saba (7) zilizoagizwa nje ya nchi kwa ajili ya shughuli za uchapishaji. Aidha, Mpango uliopo wa Serikali ni ukamilishaji wa ununuzi wa mashine mpya tatu, ambazo zitatumika kuchapisha nyaraka za uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, hivyo makusanyo yanakadiriwa kuongezeka kwa wakati huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa uchambuzi huo, Jumla ya **Sh. 1,054,142,370.54** sawa na **asilimia 5.49 tu** ya makusanyo yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu zilikusanywa na Ofisi hiyo. Uwiano huu haujafikia lengo la makusanyo ambalo ni **asilimia 66.6** hadi kufika Februari, 2024.

(b) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi hadi kufika Mwezi Februari, 2024 imekusanya kiasi cha Sh. **126,261,430** sawa na **asilimia 84.17** ya lengo la Makusanyo.

(c) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa hawajafikia lengo la makusanyo kwa kuwa hadi kufika Februari 2024 Ofisi hiyo imekusanya **Sh. 1,000,000** sawa na **asilimia 2.71** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Fungu hili unategemea vyanzo viwili ambavyo ni **ada ya usajili** wa Vyama vya Siasa vya muda mrefu na muda mfupi na **ukodishaji wa mgahawa, na kumbi za mikutano** katika jengo jipya. Hadi kufikia Februari, 2024 Vyama vilivyoomba usajili havijatimiza masharti ya kupata usajili, pia kutokamilika kwa ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya

Msajili wa Vyama vya Siasa linaloendelea kujengwa, hivyo ni chama kimoja tu ambacho kililipa ada ya usajili wa muda kwa kiasi cha **Sh. 1,000,000**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, makusanyo hafifu ya baadhi ya taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu -Sera, Bunge na Uratibu, yanaweza kutafsiriwa kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi, au vyanzo vya maduhuli vilivyoanishwa havikuwa vya uhakika na si endelevu. Kwa msingi huo, ni vyema Wizara na taasisi zake zote kuzingatia uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli.

Aidha, mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

**JEDWALI NA. 1: MAKUSANYO YA MADUHULI 2023/2024**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MAKUSANYO YA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu | 19,000,000,000 | 926,880,940.54 | 4.87 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 150,000,000 | 126,261,430 | 84.17 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 36,000,000 | 1,000,000 | 2.71 |
| **JUMLA KUU** | **19,186,000,000** | **1,054,142,370.54** | **5.49** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

## 2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti

### 2.3.1 Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, fungu hili iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 29,940,040,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 25,868,718,000** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 5,393,717,000** ni Mishahara na **Sh. 20,475,001,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Aidha, **Sh. 4,071,322,000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo **Sh. 1,880,000,000** ni fedha za ndani kwa ajili ya Ujenzi wa Kiwanda cha Kupiga Chapa cha Serikali Dodoma na **Sh. 2,191,322,000** ni fedha za nje kwa ajili ya uratibu wa Programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 32,025,534,969.68** sawa na asilimia **106.96** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Sh. 22,247,213,948.41** sawa na asilimia **86.0** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 5,009,648,891** sawa na **asilimia 123** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa sababu ya ongezeko ya fedha zilizopookelewa kwenye fungu hili ni kutokana na Fungu hili kupokea sh **4,768,672,130.27** nje ya bajeti ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya maadhimisho na sherehe za kitaifa; mazishi ya viongozi wa kitaifa; madeni ya wazabuni; uandaaji wa Mipango ya Halmashauri ya kukabiliana na maafa; na urejeshaji hali kutokana na maafa yaliyotokea Wilaya ya Hanang, pamoja na kupokea Sh. **938,326,891** ya miradi ya maendeleo nje ya Bajeti

### 2.3.2 Fungu Na. 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 17,440,724,000** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 1,706,724,000** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 15,734,000,000** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi Binafsi ya Waziri

Mkuu ilipokea jumla ya **Sh. 18,380,416,740.61** sawa na **asilimia 105.38** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Kati ya fedha hizo, **Sh. 17,461,760,740.61** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi mengineyo sawa na asilimia **110.9** na **Sh. 918,656,000.00** sawa na asilima **53.8** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa sababu ya kupokea fedha nyingi kuliko bajeti ilioidhinishwa ni kutokana na gharama za uendeshaji wa Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu ambayo haikuwa imetengewa fedha wakati wa uidhinishwaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**2.3.3 Fungu Na. 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 24,661,051,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 23,721,051,000** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 1,136,662,000** ni Mishahara na **Sh. 5,021,389,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Sh. 17,563,000,000** ilitengwa kwa ajili ya Ruzuku ya Vyama vya Siasa. Aidha, **Sh. 940,000,000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilipokea jumla ya **Sh. 15,727,984,210.47** sawa na asilima **63.77** kati ya fedha hizo, **Sh. 15,721,984,210.47** sawa na **asilimia 66.3** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 6,000,000** sawa na **asilimia 0.63** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.
Aidha, Vyama sita vya Siasa vyenye sifa ya kupata ruzuku vilipatiwa ruzuku, vyama hivyo ni: -

a) Chama cha Mapinduzi (CCM);

b) Alliance for Change and Transperancy (ACT – Wazalendo);

c) National Convention for Construction and Reform (NCCR – Mageuzi);

d) The Civic United Front (CUF – Chama cha Wananchi);

e) Democratic Party (DP); na

f) Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

**2.3.4 Fungu Na. 91 - Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 24,406,490,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 15,631,318,000** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 8,775,172,000** ilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Sh. 2,000,000,000** fedha za ndani zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa awali wa Kituo cha Taifa cha Utengamao katika eneo la Itega, Dodoma na **Sh. 6,775,172,000** fedha za nje kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya UKIMWI kwa wajidunga na wanaotumia dawa za kulevya. Hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi hiyo ilipokea jumla ya **Sh. 11,354,409,135.92** sawa na **asilimia 46.52**, Kati ya fedha hizo, **Sh. 10,384,409,135.92** sawa na asilimia **66.43** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 970,000,000** sawa na asilimia **14.31** fedha za nje zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**2.3.5 Fungu Na. 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 10,870,559,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 9,930,559,000** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 4,212,026,000** ni Mishahara na **Sh. 5,718,533,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Aidha, **Sh. 940,000,000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea jumla ya **Sh. 84,093,898,981.28** sawa na ongezeko la **asilimia 773.59** ya fedha iliyoidhinishwa, Kati ya fedha hizo, **Sh. 6,178,553,497.28** sawa na **asilimia 62.22** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, **Sh. 77,915,345,484.00** sawa na **asilimia 8288.86** zilipokelewa nje ya ukomo wa bajeti. Kati ya fedha hizo **Sh. 66,899,421,145.00** ni kwa ajili ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la

Wapiga Kura na **Sh. 11,015,924,339.00** ni kwa ajili ya uendeshaji wa Uchaguzi mdogo wa Ubunge katika jimbo la Mbarali na uchaguzi wa Madiwani katika kata 29 za Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2 na Jedwali Na. 3.

**JEDWALI NA. 2: MCHANGANUO WA MATUMIZI YA KAWAIDA 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 25,868,718,000 | 22,247,213,948.41 | 86 |
| **Fungu 25** – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 17,440,724,000 | 18,380,416,740.61 | 110.9 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 23,721,051,000 | 15,721,984,210.47 | 66.3 |
| **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | 15,631,318,000 | 10,384,409,135.92 | 66.43 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 9,930,559,000 | 6,178,553,497.28 | 62.22 |
| **JUMLA KUU** | **92,592,370,000** | **52,143,759,260.85** | **56.31** |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**JEDWALI NA. 3: MCHANGANUO WA BAJETI YA MAENDELEO 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 4,071,322,000 | 5,009,648,891 | 123 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 940,000,000 | 6,000,000 | 0.63 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 940,000,000 | 77,915,345,484 | 8288.86 |
| **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | 8,775,172,000 | 970,000,000 | 11 |
| **JUMLA KUU** | **14,726,322,000** | **83,900,994,375** | **569.73** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ni wa kuridhisha, isipokuwa katika miradi ifuatayo: -

a) **Mradi Na. 6389: Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Dodoma** Wizara hadi kufikia Februari, 2024 imepokea kiasi cha **Sh. 6,000,000** sawa na **asilimia 0.63** mwendendo wa upatikanaji wa fedha kwenye mradi huu sio wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa kiasi cha fedha kilichotumika ni kwa ajili ya malipo ya Karani wa mradi, fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu zimelipwa kupitia mfuko wa hazina Fungu 21.

Aidha, ujenzi wa jengo umefikia asilimia 84 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Aprili, 2024.

b) **Mradi wa Mfuko wa Dunia wa Kuzuia Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (Global Fund HIV/AIDS Prevention Project)** Wizara hadi kufikia Februari, 2024 imepokea kiasi cha **Sh. 970,000,000** sawa na **asilimia 14.31** ya fedha za nje zilizoidhinishwa, mwendendo wa upatikanaji wa fedha kwenye mradi huu sio wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa fedha za mradi huu zinatolewa na wafadhili, aidha Wizara inaendelea na jitihada za ufuatiliaji wa fedha hizo.

## 2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, wakati Waziri Mkuu alipowasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 aliidhinishiwa jumla ya **Sh 57,537,376,680** kwa Miradi ya Maendeleo. Katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika Jedwali Na. 4

**JEDWALI NA. 4: MITADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2023/2024**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 |
|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4429** Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi | 2,191,322,000 |
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4937** Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali | 1,880,000,000 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | **NA. 6389** Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Dodoma | 940,000,000 |
| **Fungu 61** – Tume ya | Uboreshaji wa Daftari la | 940,000,000 |

| | | |
|---|---|---|
| Taifa ya Uchaguzi | Kudumu la Wapiga Kura | |
| **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Utengamao (National Rehabilitation Center), Itega – Dodoma | 2,000,000,000 |
| **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | Mradi wa Mfuko wa Dunia wa Kuzuia Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (Global Fund HIV/AIDS Prevention Project) | 6,775,172,000 |
| **JUMLA KUU** | | **14,726,494,000** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea mradi mmoja kati ya minne inayosimamiwa na Wizara na kuchambua utekelezaji wa mradi huo kama ifuatavyo:

**2.4.1 Mradi Na. 4429: Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea kituo cha Ukuzaji viumbe maji kingolwira kilichopo katika Manispaa ya Morogoro, mradi huu una kitotoleshi cha samaki kimoja, mabwawa sita yanayofanya kazi katika ufugaji wa samaki (yenye mita za mraba 1,200), mabwawa kumi na sita ya kufugia samaki (yenye mita za mraba 13,050) ambayo yanahitaji ukarabati na kisima kimoja cha maji.

**Mheshimiwa Spika**, Kituo hicho kinauwezo wa kuzalisha vifaranga vya samaki **100,000** kwa mwezi, Kamati ilielezwa kuwa endapo matengenezo yatafanyika kwenye mabwawa 16 yaliopo basi uzalishaji utaongezeka hadi kufikia vifaranga vya samaki **1,000,000**. Aidha, kituo kimekuwa kikitoa huduma za ugani na mafunzo kwa vitendo kwa wananchi, wanavyuo na watafiti kutoka vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi.

## 2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

## 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 12,056,000,000** ikilinganishwa na **Sh. 19,186,000,000** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ambavyo imeainishwa katika Jedwali Na. 5. Hii ni na sawa na upungufu wa **asilimia 37.16** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.

**JEDWALI NA. 5: MADUHULI KWA MWAKA 2024/2025**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 |
|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 19,000,000,000 | 12,000,000,000 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 36,000,000 | 36,000,000 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 150,000,000 | 20,000,000 |
| **JUMLA KUU** | **19,186,000,000** | **12,056,000,000** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kwamba, upungufu wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa fungu 37 ni uzingatiaji wa maoni ya Kamati kuwa Wizara iweke malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

Aidha, Kamati ilielezwa upungufu wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Fungu 61 ni kutokana na kusitishwa kwa ukodishaji wa kumbi za mikutano kwenye majengo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuwa kumbi hizo zitakuwa zinatumiwa na Tume kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uboreshaji wa Daftari la mpiga kura, uchaguzi mkuu na kuimarisha usalama katika kipindi hicho.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 111,766,168,00** Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 18,603,908,000** ni mishahara, **Sh. 17,563,000,000** ni ruzuku kwa vyama vya Siasa na **Sh. 75,599,260,000** ni matumizi mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na. 5

**JEDWALI NA. 6: MCHANGANUO WA MATUMIZI YA KAWAIDA 2024/2025**

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 6,932,937,000 | 26,921,042,000 | 0 | 33,853,979,000 |
| **Fungu 25** – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 1,687,420,000 | 24,504,128,000 | 0 | 26,191,548,000 |
| **Fungu 27** – | 1,181,418,000 | 6,295,400,000 | 17,563,000,000 | 25,039,818,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | | | | |
| **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | 4,657,413,000 | 12,302,509,000 | 0 | 16,959,922,000 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 4,144,720,000 | 5,576,181,000 | 0 | 9,720,901,000 |
| **JUMLA KUU** | **18,603,908,000** | **75,599,260,000** | **17,563,000,000** | **111,766,168,000** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **asilimia 20.7** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa **Sh. 92,592,370,000**. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma pamoja na kuanzishwa kwa Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria.

### 3.3 Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 176,376,529,000/=** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 171,107,959,000** ni fedha za ndani, na **Sh. 5,268,570,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **Sh. 161,650,035,000** sawa na **asilimia 1,097.7** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha, sababu ya ongezeko hilo imechangiwa na ongezeko la bajeti ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 6.**

**JEDWALI NA. 7:MCHANGANUO WA BAJETI YA MAENDELEO 2023/2024**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | |
|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4937** Ujenzi wa Kiwanda cha uchapaji nyaraka za Serikali Dodoma | 1,235,635,000 | 0 |
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4429** Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi | 0 | 5,268,570,000 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | **NA. 6389** Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa Zanzibar | 940,000,000 | 0 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 | 167,617,818,000 | 0 |
| **Jumla Ndogo** | | **171,107,959,000** | **5,268,570,000** |
| **JUMLA KUU** | | **176,376,529,000** | |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani. Kwa umahususi, Kamati inaipongeza Serikali ya awamu ya sita chini ya usimamizi mahiri, hodari na shupavu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa mara ya kwanza kutenga fedha za maandalizi ya uchaguzi Mkuu kwa kutumia fedha za ndani bila utegemezi wowote wa fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kwamba, ipo haja ya Serikali kutenga fedha za ndani katika mradi wa Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi kwani hadi kufikia Februari 2024 mradi huo ulipokea asilimia **57.17** tu ya fedha za nje zilizoidhinishwa.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kuwa Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambao yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

### 4.2 Ushauri Mahususi Fungu kwa Fungu

#### 4.2.1 Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

i) Serikali ihakikishe kwamba, fedha zinapatikana kikamilifu kwenye Mradi Na. 4429 Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi.

ii) Serikali ihakikishe kwamba Ununuzi wa mashine za uchapaji pamoja na matengenezo ya mashine chakavu unakamilika kwa wakati kabla ya kuanza kwa maandalizi ya chaguzi za Serikali za Mitaa 2024.

### 4.3 Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa

Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa iweke mpango endelevu na mahsusi wa matumizi ya jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inayoendana na vipaumbele vya Ofisi hiyo.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.

16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.
21. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wa Shughuli za Serikali Bungeni na kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi Mkubwa. Aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Waziri na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ambao wanamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majumu yake katika ofisi hiyo. Kwa umuhimu wao, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Jenista Joakim Mhagama, Mb. – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

2. Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga, Mb. – Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Jim Yonazi, Mhe. Jaji Francis S. Mutungi - Msajili wa vyama vya Siasa, Mhe. Jaji Jacobs Mwambegele – Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Ndg. Kailima Ramadhan na Ndg. Aretas James Lyimo – Kamishina Jenerali wa Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, ndc kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
03 Aprili, 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kusoma vizuri. Waheshimiwa sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Mwenyekiti una dakika 10, *summarize* umalizie kwenye kuidhinisha pesa, dakika 10 tu taarifa yako tayari ipo kwenye *Hansard*.

**MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa naomba taarifa yangu yote iingie kwenye kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa mujibu wa Kanuni 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kudumu ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Mfuko wa Bajeti wa Bunge Fungu 42 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaundwa kwa mujibu wa Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, Ofisi ya Bunge ina jukumu la kutoa huduma kwa Wabunge ili kuwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 63 ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Bunge Mwaka wa Fedha 2023/2024; Mfuko wa Bunge ulianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge, Sura ya 115. Kifungu hicho kilianzisha Mfuko wa Bunge na kutoa maelekezo ya namna Mfuko utakavyosimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja kama ulivyosema kwamba niende kwenye maoni na kuomba bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi Fungu 42 - Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha 2025 yamezingatia dira na malengo ya taasisi, majukumu ya idara na vitengo na maelekezo yaliyotolewa katika mwongozo wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2024/2025 ni sehemu ya rasilimali ya kutekeleza Mpango na Mkakati wa Ofisi wa mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 unaotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo mahususi ya mpango huu ni kuwezesha Waheshimiwa Wabunge kutekeleza majukumu yao ya kikatiba kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamezingatia mahitaji ya msingi yakiwemo mahitaji na shughuli za Bunge, mikutano ya Bunge, Kamati za Bunge na uendeshaji wa Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mfuko wa Bunge umepewa ukomo wa bilioni 181.8 sawa na ongezeko la asilimia 7.58 ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2023 ya shilingi bilioni 168.994. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 23.87 ni mshahara, shilingi bilioni 148.254 ni fedha za matumizi mengineyo. Aidha fedha za matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 9.68, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 8.97 ni

fedha za ndani na shilingi milioni 704.34 ni fedha za nje. Mchanganuo wa ongezeko la bajeti umeainishwa katika jedwali namba mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maduhuli, ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi milioni 147.967 itakayotokana na ukodishaji wa ukumbi wa mikutano pamoja na kodi ya pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vya bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2024 vimeoneshwa vingi sana, viko takribani 18 ambapo nisingeweza kuvisoma, kwa hiyo vyote viingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati; utwaaji wa maeneo yanayozunguka Bunge. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia katika kulipa fidia kwa wamiliki binafsi wa maeneo yanayozunguka Bunge. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba taasisi zote za umma zinahamishwa kwa wakati ili kupisha uendelezaji wa maeneo hayo kwa Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; naomba nihitimishe kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vyema mashauriano ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Zainab Katimba aliyekuwa Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kamati inawatakia kila la kheri katika majukumu yao mapya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge, naomba majina yao yote yaingia katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc,* Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam uliowezesha kufanikisha kazi za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge, Fungu 42 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye jumla ya shilingi 181,805,233,000 ambapo kiasi cha shilingi 23,870,772,000 ni kwa ajili ya mshahara, shilingi 148,253,651,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 9,680,810,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ahsante. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/25.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, Ofisi ya Bunge ina jukumu la kutoa huduma kwa Wabunge ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 63 (2) na (3) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) kipengele cha (c), Kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha pamoja na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* ili kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/25.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inatoa mrejesho wa kikao cha mashauriano kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge fungu 42 hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2024, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti wa Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa fedha 2024/25.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**Mheshimiwa Spika,** mfuko wa Bunge ulianzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge Sura ya 115. Kifungu hicho kilianzisha mfuko wa Bunge na kutoa maelekezo ya namna mfuko huo utakavyosimamiwa na kuendeshwa.

**Mheshimiwa Spika,** mfuko wa Bunge hutengewa fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji mbalimbali, ambapo **asilimia 88** ya mahitaji hayo ya fedha hutumika kugharamia Mikutano ya Bunge, Kamati za Bunge, Posho ya Jimbo, Usafiri kwa Wabunge, Matibabu kwa Wabunge, Shughuli za Vyama vya hiyari vya Kibunge, Michezo ya Mabunge ya

Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na sehemu iliyobaki ya **asilimia 12** hutumika kutekeleza shughuli za kiutawala na Uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura ya 348, Sheria ya Manunuzi ya Umma Sura ya 410, Mpango Mkakati wa mwaka 2021/22-2025/26 pamoja na Mpango wa Muda wa Kati wa mwaka 2022/23 – 2024/25. Utekelezaji wa Bajeti umezingatia malengo yaliyotarajiwa kufikiwa katika vipindi husika ili kuboresha huduma mbalimbali kulingana na mahitaji halisi kwa lengo la kuliwezesha Bunge na Wabunge kutimiza wajibu wao kikatiba.

**2.1 Bajeti ya Mfuko wa Bunge ya mwaka 2023/24.**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 168.994.** Kati ya Fedha hizo **shilingi bilioni 23.605** ni fedha za Mishahara, **shilingi bilioni 140.22** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, (OC) na **shilingi bilioni 5.169** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 4.7** ni fedha za Ndani na **shilingi milioni 469.02** ni fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2024 Mfuko wa Bunge ulipokea jumla ya **Shilingi bilioni 119.229** sawa na **asilimia 70.55** ya bajeti nzima. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **shilingi bilioni 15.779** sawa na **asilimia 66.84** ya bajeti, matumizi mengineyo ni **shilingi bilioni 101.896** sawa na **asilimia 72.67** ya bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za maendeleo fedha zilizopokelewa ni **shilingi bilioni 1.554** sawa na **asilimia 33.07** ya bajeti. Fedha hizo zilitumika kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa nyumba mbili (2) za Viongozi pamoja na ukarabati wa majengo ya Bunge. Aidha, taratibu za kununua na kusimika Mitambo ya Ulinzi na Usalama zinaendelea. Jedwali Na. 1 linaonyesha mchanganuo wa fedha zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 29 Februari 2024.

**Jedwali Na. 1: Fedha zilizopokelewa hadi 29 Februari, 2024**

| AINA YA MATUMIZI | FEDHA ZILIZOIDHINISHWA (A) | FEDHA ZILIZOPOKELEWA (B) | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI (B/A) |
|---|---|---|---|
| **Mishahara** | 23,605,226,000 | 15,778,568,628 | 66.84 |
| **Matumizi Mengineyo** | 140,219,683,075 | 101,895,522,545 | 72.67 |
| **Maendeleo** | 5,169,020,000 | 1,554,339,105.47 | 33.03 |
| | **168,993,929,075** | **119,228,430,278.47** | **70.55** |

**Chanzo:** *Mfuko wa Bunge*

### 2.2 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya kiasi cha **shilingi milioni 131.766** fedha za maduhuli. Hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2024 kiasi cha **shilingi milioni 76.678** kimekusanywa sawa na **asilimia 58.19**. Fedha hizi zimetokana na kodi ya pango katika Jengo la Utawala Annex pamoja na kukodisha Kumbi za Mikutano katika Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam na Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wakati na kulingana na mahitaji ya mfuko wa Bunge ili kuwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

### 2.3 Utwaaji wa Maeneo Yanayozunguka Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Bunge katika mwaka wa fedha 2023/24 ulipokea kiasi cha **shilingi bilioni 12.215** kwa ajili ya kulipa fidia kwa wamiliki wote wa maeneo binafsi yanayolizunguka Bunge. Ulipaji huo ulifanyika baada ya Serikali kutangaza katika Gazeti la Serikali Toleo la 51 la tarehe 22 Desemba, 2023. Utolewaji wa fedha hizo ni utekelezaji wa pendekezo la Tume ya Utumishi wa Bunge pamoja na Kamati ya Bunge ya Bajeti ili kuongeza eneo la Bunge kutokana na mahitaji na sababu za kiusalama.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza pendekezo la Tume na Kamati. Hatua hii inaenda kuongeza ukubwa wa eneo la Bunge kutoka mita za mraba **42,312** hadi **165,236.** Taratibu kuhusu utwaaji wa maeneo ya Umma yaliyo chini ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Wakala wa Ununuzi wa Serikali (GPSA), Machinjio ya Mifugo na Wakala wa Uhifadhi wa Chakula Taifa (NFRA) bado zinaendelea.

### 2.4 Shughuli Zilizotekelezwa Katika Bajeti ya Mwaka 2023/24

**Mheshimiwa Spika,** mfuko wa Bunge umefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Uratibu wa shughuli za Bunge kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Ofisi wa mwaka 2021/22-2025/26;

ii. Kuratibu Mikutano ya Bunge Mitatu (3) pamoja na Kamati zake;

iii. Kulipa stahili za Wabunge na Watumishi kwa wakati;

iv. Kushiriki katika Mikutano mbalimbali ndani ya nchi kwa wabunge na watumishi;

v. Kushiriki katika Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge ni mwanachama;

vi. Kushiriki katika michezo ya Wabunge - Kigali nchini Rwanda na Watumishi mkoani Iringa; vii. Kugharamia shughuli za uendeshaji wa Ofisi; viii. Kuajiri Watumishi wapya (44) ambao wameongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Bunge.

### 2.6 Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Bunge, Ofisi ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Mabadiliko ya mara kwa mara ya viwango vya kubadilisha fedha za kigeni yamesababisha kupanda kwa gharama za uendeshaji wa shughuli za Ofisi; na

ii. Kutokupokea fedha za nje za Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) kumeathiri shughuli zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa na mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, kwa sasa Ofisi ya Bunge inaendelea kushirikiana na kuwasiliana na Wadau wa Maendeleo ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinapatikana kabla ya mwaka wa fedha kumalizika.

## 3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU 42 - MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 yamezingatia Dira na Malengo ya Taasisi, Majukumu ya Idara na Vitengo na maelekezo yaliyotolewa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25. Aidha, Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2024/25 ni sehemu ya rasilimali ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Ofisi wa Mwaka 2021/22 -2025/26 unaotekelezwa kwa kipindi cha Mwaka mmoja mmoja. Malengo mahususi ya Mpango huo ni kuwezesha Waheshimiwa Wabunge kutekeleza majukumu yao ya kikatiba kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Maandalizi ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25 yamezingatia mahitaji ya msingi yakiwemo mahitaji ya shughuli za Bunge (Mikutano ya Bunge na Kamati za Bunge) na uendeshaji wa Ofisi.

### 3.1 Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Mfuko wa Bunge umepewa ukomo wa **shilingi bilioni 181.805** sawa na ongezeko la **asilimia 7.58** ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2023/24 ya **shilingi bilioni 168.994**. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 23.871** ni mishahara, **shilingi bilioni 148.254** ni fedha za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za matumizi ya maendeleo ni **shilingi bilioni 9.681,** kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 8.976** ni fedha za ndani na **shilingi milioni 704.34** ni fedha za nje. Mchanganuo wa ongezeko la Bajeti umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Ulinganisho wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 na 2024/25**

| AINA YA MATUMIZI | 2023/2024 | MAPENDEKEZO YA BAJETI 2024/2025 | ONGEZEKO/ PUNGUZO |
|---|---|---|---|
| **Mishahara** | 23,605,226,000 | 23,870,772,000 | 265,546,000 |
| **Matumizi Mengineyo** | 140,219,683,075 | 148,253,651,000 | 8,033,967,925 |
| **Maendeleo** | **5,169,020,000** | **9,680,810,000** | **4,511,790,000** |
| Fedha za ndani | 4,700,000,000 | 8,976,470,000 | 4,346,070,000 |
| Fedha za nje | 469,020,000 | 704,340,000 | 165,720,000 |
| **JUMLA** | **168,993,929,075** | **181,805,233,000** | **12,811,303,925** |

**Chanzo:** *Mfuko wa Bunge*

### 3.2 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa maduhuli, Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya **shilingi milioni 147.967** yatakayotokana na ukodishaji wa Kumbi za Mikutano pamoja na kodi ya pango.

## 4.0 VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/25 Mfuko wa Bunge unatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kugharamia Mikutano minne (4) ya Bunge na Kamati;

ii. Kugharamia Posho ya Jimbo na Usafiri wa Wabunge na stahiki nyingine kwa Wabunge na Watumishi;

iii. Kugharamia matibabu ya Wabunge na familia zao ndani na nje ya nchi pamoja na Watumishi kwa utaratibu wa Bima ya Afya;

iv. Kusimamia uendeshaji wa Ukumbi wa Bunge, Mitambo na Mashine;

v. Kununua vishikwambi, bendera pamoja na katiba kwa ajili ya Wabunge wa Bunge la 13;

vi. Kugharamia ushiriki wa Wabunge katika vyama vya Kikanda na Kimataifa vya SADC-PF, SADCOPAC, PAP, EAC, CPA Africa Region, CPA International, FP- ICGLR, IPU, OACPS-EU;

vii. Kugharamia ushiriki wa Wabunge katika Michezo ya Afrika Mashariki (EAC) na Watumishi katika mashindano ya SHIMIWI;

viii. Kuwajengea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kikatiba;

ix. Kugharamia ununuzi na usimikaji wa mitambo ya ulinzi na usalama;

x. Ununuzi wa Vitendea Kazi kwa Watumishi hususan Watumishi wapya;

xi. Ununuzi wa Kompyuta za Maktaba kwa ajili ya matumizi ya Wabunge na Watumishi;

xii. Ununuzi wa magari mawili, moja ni la Kiongozi na gari la pili kwa ajili ya Wagonjwa;

xiii. Kuwezesha Watumishi kushiriki mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi;

xiv. Kuratibu kazi ya kukarabati Jengo la Ukumbi wa Bunge na majengo ya Ofisi ya Bunge;

xv. Kugharamia urushaji wa vipindi vya televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;

xvi. Kufanya maandalizi ya kuboresha Mfumo wa Sauti katika Ukumbi wa Bunge;

xvii. Kugharamia uandaaji wa Mpango wa Matumizi ya ardhi (Master Plan) wa maeneo mapya ya Bunge;

xviii. Kuratibu utoaji wa Habari kwa umma na elimu kwa wananchi kuhusu Bunge likiwemo Jarida linalohusu shughuli za Kibunge zilizofanyika; na

xix. Kugharamia masuala mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa Ofisi kwa ujumla.

## 5.0 MAONI YA KAMATI

### 5.1 Utwaaji wa Maeneo yanayozunguka Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia katika kulipa fidia kwa wamiliki binafsi wa maeneo yanayozunguka Bunge. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba taasisi zote za umma zinahamishwa kwa wakati ili kupisha uendelezaji wa maeneo hayo kwa ofisi ya Bunge.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, na Uratibu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawapongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, (Mb) aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Zainabu Katimba, (Mb) aliyekuwa mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI. Kamati inawatakia kila la kheri katika majukumu yao mapya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb – M/Mwenyekiti
2. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
3. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb
4. Mhe. Dkt. Charles Kimei, Mb
5. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
6. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb
7. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
8. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb
9. Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb
10. Mhe. Stella Ikupa, Mb
11. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb
12. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
13. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb
14. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb
15. Mhe. Rashid Abdalla Rashid, Mb
16. Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb
17. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb
18. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
19. Mhe. Omar Ali Omar, Mb
20. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo

na kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye jumla ya **shilingi 181,805,233,000** ambapo kiasi cha **shilingi 23,870,772,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **shilingi 148,253,651,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi 9,680,810,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Omari Mohamed Kigua, (Mb)
**M/MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
03 Aprili, 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kulinda muda na unaweza ukampitia Mheshimiwa Shekilindi pale akusaidiesaidie mambo mengine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Mwenyekiti dakika kumi, taarifa yako tayari iko kwenye *Hansard*.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE K.n.y. MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, awali ya yote naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa

Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa taarifa ya utekelezaji na makadirio ya (Fungu 92), naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua mambo makuu matatu yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Makadirio ya matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(iii) Maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Fungu 92.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, yanatokana na Kamati kufanya mapitio ya mambo makubwa matatu:-

(i) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 92;

(ii) Hali ya upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2024.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi ulilenga Bunge kujiridhisha na utoshelevu wa utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha Bajeti husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi; kuhusu uzingatiaji na utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati; Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa jumla ya maeneo kumi na mbili (12) yalitolewa maoni na ushauri ili kuboresha utendaji wa Serikali. Maeneo mawili yametekelezwa kikamilifu na maeneo 10 bado yapo katika hatua ya utekelezaji. Kamati inasisitiza nguvu zaidi iongezwe kwenye maeneo ambayo utekelezaji unaendelea ili yakamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa yaliyobainika wakati wa ziara ya Kamati; Kamati ilitembelea magereza yaliyopo katika Mkoa wa Singida na Geita ili kupata taarifa kuhusu hali ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika magereza hayo. Pia ilitembelea na kukagua Konga za WAVIU katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini, Mradi wa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana – Timiza Malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-

(i) Upatikanaji wa uhakika wa huduma za upimaji wa Virusi vya UKIMWI na utoaji wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI *(ARVs)* kwa WAVIU hasa katika magereza na mahabusu;

(ii) Upatikanaji wa huduma jumuishi ya kinga dhidi ya maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI katika Mradi wa Timiza Malengo;

(iii) Uhamasisha katika jamii kuhusu upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari na kujua hali zao za kiafya na kuhakikisha watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanadumu katika huduma za tiba na matunzo na kutoa elimu ya ufuasi mzuri wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI na kupinga unyanyapaa na ubaguzi kwa WAVIU kupitia Konga za WAVIU zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini;

(iv) Kuimarika kwa shughuli za uchumi kwa wanawake vijana na wasichana balehe kupitia miradi mbalimbali ya ujasiriamali inayoratibiwa na *Global Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto tulizozibaini ni:-

(i) Kutokutekelezwa kwa Mwongozo wa Utoaji Huduma kwa Wafungwa na Mahabusu wa Wizara ya Afya ambao unaelekeza kwamba jukumu la kuwatibu wafungwa na mahabusu ni la Mganga Mkuu wa Hospitali katika eneo gereza lilipo;

(ii) Uhaba wa dawa za kutibu wafungwa na mahabusu hususani wakati wa dharura;

(iii) Uhaba wa rasilimali fedha katika Konga za WAVIU katika kutekeleza afua za UKIMWI kwa uendelevu; na

(iv) Baadhi ya vikundi vya wanawake na vijana kushindwa kuanzisha miradi ya ujasiriamali kwa wakati kutokana na kukosa namba za *NIDA* kwa ajili ya kupata huduma za Kibenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusiana na upatikanaji wa fedha; upatikanaji wa fedha za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya shilingi 25,862,966,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo unapatikana katika ukurasa wa nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufika mwezi Februari, 2024, Tume ilipokea kiasi cha shilingi 4,292,797,045.93, sawa na asilimia 16.5 ya Bajeti yote. Katika upande wa fedha za maendeleo, ilibainika hadi mwezi Februari, 2024, kati ya shilingi 22,192,149,000.00 zilizoidhinishwa *TACAIDS* ilipata asilimia 10.7 tu ya fedha. Aidha, katika Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(AIDS Trust Fund – ATF)* katika Mwaka wa Fedha zilitengwa shilingi 1,880,000,000 na hadi kufikia mwezi Februari ilikuwa imeshapokea shilingi milioni 940 sawa na asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla hali ya upatikanaji wa fedha si ya kuridhisha. Aidha, Kamati inasisitiza fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya masuala ya UKIMWI zitolewe kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa za kipindi hiki kilichobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, unaonesha kuwa maeneo ya vipaumbele yamezingatia miongozo iliyotolewa japo bado kumekuwa na changamoto ya Serikali kutenga fedha za ndani kidogo kwa ajili ya uratibu wa masuala ya UKIMWI, jambo linaloashiria kuwa na utegemezi mkubwa wa fedha za nje kutokana na wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mapitio ya Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2024/2025; katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Fungu 92 limeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 4,543,483,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Tume imeomba kuidhinishiwa shilingi 13,266,498,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI inaonesha kuwa bajeti imeshuka kwa asilimia 30.1, ambapo fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo hazijaongezeka ilikinganishwa na mwaka 2023/2024 na fedha za nje za maendeleo zimepungua kwa wastani wa asilimia 43.9. Mchanganuo unapatikana katika kielelezo namba tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kupungua kwa fedha za bajeti ya maendeleo kutoka nje, bado bajeti ya maendeleo kwa kiasi kikubwa inategemea fedha kutoka nje. Hali hii ni dhahiri kuwa bado tuna changamoto ya kutegemea fedha za wafadhili kwa kiwango kikubwa katika kuratibu masuala ya UKIMWI jambo ambalo linatishia usalama wa WAVIU pale ambapo wafadhili watasitisha kutoa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushauri wa Kamati; baada ya kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2023/2024 na makadirio ya fedha kwa mwaka 2024/2025 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Fungu 92, tunaomba kutoa maoni yafuatayo:-

(i) Katika suala la upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI, Serikali itoe fedha zote za Tume ya Kudhibiti UKIMWI kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kuwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa muda uliopangwa;

(ii) Serikali iimarishe Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI na kuweka mpango madhubuti wa kupata fedha, kupata vyanzo mahususi vya mapato ya ndani vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya miradi inayolenga kudhibiti VVU na UKIMWI;

(iii) Kuongeza kiwango cha fedha za ndani zinazotengwa kupitia Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI *(AIDS Trust Fund)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza afua za UKIMWI, Serikali imejiwekea malengo ya kufikia asilimia 95-95-95. Katika 95 ya kwanza tumefikia asilimia 82, 95 ya pili 97 na 95 ya tatu asilimia 94. Bado kuna changamoto ya malengo ya asilimia 95 ya kwanza ambayo inahusu kupima na kujitambua. Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo: -

(i) Serikali iongeze nguvu na jitihada katika kufikia shabaha ya kwanza inayohusu watu wale wanaoishi na maambukizi ya UKIMWI kupima na kujua hali zao za afya;

(ii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii kuhusu virusi vya UKIMWI ili kupunguza unyanyapaa pamoja na maambukizi mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana:-

(i) Serikali inashauriwa ianzishe mradi maalum wa ujasiriamali kwa jinsi zote ambao utajumuisha ushiriki wa wavulana balehe na wanaume vijana;

(ii) Serikali ibuni miradi mikubwa yenye tija zaidi itakayosaidia kuinua uchumi kwa WAVIU walio katika vikundi mbalimbali; na

(iii) Iongeze wigo wa mradi huu katika halmashauri na mikoa mbalimbali nchini ili kufikia na kunufaisha walengwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa afua za UKIMWI gerezani; Kamati inashauri itekeleze Mwongozo wa Utoaji Huduma katika Magereza ambapo inamtaka Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali kutoa huduma hizo na kuhakikisha kwamba kunapatikana na dawa kwa matibabu ya dharura ya wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; tunatoa pongezi kwa uongozi wako kwa jinsi unavyoongoza Bunge, uongozi wa Wizara kwa

ushirikiano mkubwa wanaotupatia. Pia tunawashukuru *TACAIDS* kwa ushirikiano mkubwa, lakini mwisho tunawashukuru Sekretarieti ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuchambua bajeti hii na kusimamia Fungu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Udhibiti UKIMWI - Fungu 92 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU (TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA –*TACAIDS*) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na majukumu mengine, kinaainisha moja ya jukumu la Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI ni kushughulikia Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Katika kutekeleza jukumu

hilo, mnamo tarehe 21 Machi, 2024, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya **Fungu 92** – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya **(Fungu 92),** naomba kutoa Taarifa ya Kamati inayofafanua mambo makuu matatu (3) yafuatayo: -

(a) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(b) Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(c) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu **Fungu 92** -Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)*.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 2.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kushauri ipasavyo kuhusu makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilifanya uchambuzi wa wasilisho la Serikali kuhusu mambo makuu matatu (3) ambayo ni: -

(a) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

(c) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 yanatokana na Kamati kufanya mapitio ya mambo makuu yafuatayo: -

(a) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu; **Fungu 92** - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(b) Hali ya upatikanaji wa Fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2024; na

(c) Utekelezaji wa malengo yaliyokuwa yamewekwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi huo ulilenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha na utoshelevu wa utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi, ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha Bajeti husika.

### 2.2 Uchambuzi kuhusu Uzingatiaji na Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Ili kujiridhisha na namna Serikali inavyozingatia na kutekeleza ushauri wa Kamati unaotolewa katika Bunge lako Tukufu, Kamati ilichambua Taarifa iliyowasilishwa kuhusu uzingatiaji na utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa jumla ya maeneo kumi na mbili (12) yalitolewa maoni na ushauri ili kuboresha utendaji wa Serikali. Kati ya maeneo hayo yaliyotolewa ushauri, maeneo mawili (2) yametekelezwa kikamilifu na maeneo kumi

(10) yapo katika hatua ya utekelezaji. Kwa msingi huo bado inahitajika kutoa msisitizo na kuweka nguvu zaidi katika maeneo ambayo utekelezaji wake unaendelea ili yakamilishwe.

## 2.3 Uchambuzi wa yaliyobainika wakati wa Ziara ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyopo katika mkoa wa Singida na Geita. Miradi hiyo inaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kupitia Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania.

Vile vile, Kamati ilitembelea magereza yaliyopo katika Mkoa wa Singida na Geita ili kupata Taarifa kuhusu hali ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika magereza hayo. Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 12 hadi 17 Machi, 2024 ambapo Konga za WAVIU katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini, Mradi wa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana – Timiza Malengo, Gereza la Wilaya ya Chato na Gereza la Wilaya ya Manyoni zilitembelewa na kukaguliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini uwepo wa mafanikio na changamoto mbalimbali na hivyo kutoa ushauri wa namna ya kukabiliana na changamoto zilizobainika. Mafanikio yaliyobainika ni kama ifuatavyo; -

i) Upatikanaji wa uhakika wa huduma za upimaji wa Virusi vya UKIMWI na utoaji wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI (ARVs) kwa WAVIU hasa katika magereza na mahabusu. Kwa mfano, katika Gereza la Wilaya ya Chato kuna WAVIU 24 na Gereza la Wilaya ya Manyoni kuna WAVIU 5 wanaotumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI;

ii) Kuwafikia Wasichana balehe na Wanawake vijana kwa kiwango kikubwa kwa kutoa huduma jumuishi ya kinga dhidi ya maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI kupitia Mradi wa Timiza Malengo unaolenga kuwasaidia Wasichana balehe na Wanawake vijana;

iii) Kuhamasisha jamii kuhusu upimaji wa Virusi vya UKIMWI kwa hiari na kujua hali zao za kiafya, kuhakikisha watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wanadumu katika huduma za tiba na matunzo kwa kutoa elimu ya ufuasi mzuri wa dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI na kupinga unyanyapaa na ubaguzi kwa WAVIU kupitia Konga za WAVIU zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini;

iv) Kuimarisha na kukuza uchumi wa Wanawake vijana na Wasichana balehe kupitia miradi mbalimbali ya ujasiriamali inayoratibiwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia (Global Fund) wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kupitia Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania, imebainika kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazoathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

i) Kutokutekelezwa kwa Mwongozo wa Utoaji huduma kwa Wafungwa na Mahabusu uliotolewa terehe 25 Mei, 1998 na Wizara ya Afya ambao ulielekeza kuwa jukumu la kuwatibu Wafungwa na Mahabusu ni la Mganga wa Hospitali ya Serikali katika eneo gereza lilipo;

ii) Uhaba wa dawa za kutibu Wafungwa na Mahabusu hususani wakati wa dharura;

iii) Uhaba wa rasilimali fedha kwa Konga za WAVIU katika kutekeleza afua za UKIMWI kwa uendelevu; na

iv) Baadhi ya vikundi vya Wanawake Vijana na Wasichana Balehe kushindwa kuanzisha miradi ya ujasiriamali kwa wakati kutokana na kukosa namba za NIDA kwa ajili ya kupata huduma za Kibenki.

## 2.4 Uchambuzi kuhusu Upatikanaji wa Fedha

### 2.4.1 Upatikanaji wa Fedha za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS)* - Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Taarifa ya hali ya upatikanaji wa fedha kwa lengo la kujiridhisha na kiwango cha fedha zilizotolewa ili kuwezesha utekelezaji wa malengo na vipaumbele vya Tume kama ilivyokuwa imeidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/24 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 25,862,966,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Fedha za Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,670,817,000.00** ni Matumizi ya Kawaida yenye kujumuisha Mishahara **1,897,434,000.00** na **Shilingi 1,773,383,000.00** za Matumizi Mengineyo**.** Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo ni **22,192,149,000.00** ambapo kati yake fedha za ndani ni **Shilingi 1,880,000,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 20,312,149,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, hadi kufika mwezi Februari, 2024, Tume ilipokea kiasi cha **Shilingi 4,292,797,045.93** sawa na asilimia **16.59** ya Bajeti yake yote. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa fedha za Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 1,915,108,181.93** sawa na **asilimia 52.17** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida fedha zilizotolewa kwa ajili ya Mishahara ni **Shilingi 1,104,716,488.00** sawa na **asilimia 58.22** ya fedha zote za Mishahara zilizoidhinishwa. Fedha za Matumizi Mengineyo zimetolewa **Shilingi 810,391,693.93** sawa na **asilimia 45.7** ya fedha zote za Matumizi Mengineyo zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Fedha za Maendeleo, imebainika kuwa hadi mwezi Februari 2024, kati ya **Shilingi 22,192,149,000.00** zilizoidhinishwa, kiasi cha **Shilingi 2,377,688,864.00** zimepokelewa sawa na **asilimia 10.71** ya fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu wakati wa kuidhinisha bajeti ya mwaka 2023/2024. Fedha hizi za Maendeleo zilizotolewa zinajumuisha Fedha za Ndani **Shilingi 940,000,000.00** sawa na **asilimia 50** ya Fedha za Ndani zilizoidhinishwa pamoja na Fedha za Nje **Shilingi 1,437,688,864.00** sawa

na **asilimia 7.08** ya Fedha zote za Nje za Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

### 2.4.2 Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (*Aids Trust Fund - ATF*)

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi mwezi Februari, 2024 fedha za ndani za maendeleo zilizotolewa ni **Shilingi 940,000,000.00** sawa na **asilimia 50**. Fedha hizo zilizotolewa zimetumika katika kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo kutoa elimu ya kuzuia maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na unyanyapaa kwa wafanyakazi na wanafunzi wa vyuo 16 vya elimu ya juu na kati vya mikoa ya Kilimanjaro na Arusha; Kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za ununuzi na usambazaji wa dawa za septrin kwenye mikoa ya Tabora, Shinyanga, Mwanza, Geita, Kagera, Kigoma, Katavi, Mbeya, Njombe, Ruvuma, Mtwara, Lindi na Dar es Salaam. Vile vile, kugharamia kikao cha wataalamu wa kisekta na kikao cha Makatibu Wakuu wa baadhi ya wizara za kisekta ili kufanya mapitio ya andiko la mapendekezo ya vyanzo endelevu vya fedha za Mfuko, Kuhuisha na kuunganisha Mifumo ya kielektroniki ya uchangiaji fedha kwenye Akaunti ya makusanyo ya NMB, lipa namba ya tigo, Airtel Money, namba ya malipo ya Serikali (Control Number) kwenye Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) ili kumrahisishia mchangiaji kupitia "*AIDS TRUST FUND App*" na Uendeshaji wa vikao vya robo mwaka vya bodi ya Mfuko kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Kielelezo NA. 1: MCHANGANUO WA FEDHA ZILIZOIDHINISHWA NA FEDHA ZILIZOPOKELEWA KUANZIA JULAI, 2023 HADI FEBRUARI, 2024**

| MAELEZO | KILICHOIDHINISHWA | KILICHOTOLEWA | ASILIMIA |
|---|---:|---:|---:|
| Mishahara | 1,897,434,000.00 | 1,104,716,488.00 | **58.22** |
| Matumizi Mengineyo | 1,773,383,000.00 | 810,391,693.93 | **45.7** |
| **Jumla (Fedha za Matumizi ya Kawaida)** | **3,670,817,000.00** | **1,915,108,181.93** | **52.1** |
| Maendeleo Ndani | 1,880,000,000.00 | 940,000,000.00 | **50** |
| Maendeleo Nje | 20,312,149,000.00 | 1,437,688,864.00 | **7.08** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jumla (Fedha za Maendeleo)** | **22,192,149,000.00** | **2,377,688,864.00** | **10.71** |
| **Jumla Kuu** | **25,862,966,000.00** | **4,292,797,045,93** | **16.59** |

***Chanzo: Taarifa ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, hali ya upatikanaji wa fedha ambayo ni wastani wa **asilimia 16.59** si ya kuridhisha ukizingatia ni muda mchache uliobaki kumaliza Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kamati inasisitiza fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Masuala ya UKIMWI zitolewe kwa wakati ili kutokwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa kipindi husika.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu 92 (Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Uchambuzi ulizingatia uhusiano wa makadirio hayo na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025, Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano 2021/22 – 2025/26 na Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaonesha kuwa maeneo ya vipaumbele katika makadirio hayo yamezingatia miongozo iliyopo japokuwa bado kumekuwa na changamoto ya Serikali kutenga fedha za ndani kidogo kwa ajili ya uratibu wa Masuala ya UKIMWI jambo linaloashiria kuwa na utegemezi mkubwa wa fedha za nje kutoka kwa wafadhili.


## 3.1 Mapitio ya Makadirio ya Fedha kwa Mwaka 2024/2025

### 3.1.1 Fedha zinazoombwa kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI – Fungu 92

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha wa 2024/25, Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania – Fungu 92 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,542,483,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,817,358,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 2,725,125,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Aidha, Kwa upande wa fedha za Maendeleo, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 13,266,498,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 1,880,000,000.00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 11,386,498,000.00** ni Fedha za nje.

**Kielelezo NA. 2: FEDHA ZINAZOOMBWA KUIDHINISHWA KWA MWAKA 2024/2025**




***Chanzo; Randama ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2024/2025***

**Mheshimiwa Spika**, Mwelekeo wa bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI unaonesha kuwa bajeti imeshuka kwa **asilimia 31.1** ambapo fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo hazijaongezeka ikilinganishwa

na mwaka 2023/2024 na fedha za nje za maendeleo zimepungua kwa **asilimia 43.9.** Vilevile, fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zimeongezeka kwa **asilimia 23.7** ambapo fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo zimeongezeka kwa **asilimia 53.6** na fedha kwa ajili ya Mishahara zimepungua kwa **asilimia 4.2.** Lifuatalo ni jedwali linaloonesha ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 na fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa kipindi cha mwaka 2024/2025.

### 3.1.2 Ulinganisho wa Fedha zilizoidhinishwa Mwaka 2023/2024 na Fedha zinazoombwa Kuidhinishwa Mwaka 2024/2025

**Kielelezo NA. 3: ULINGANISHO WA BAJETI YA MWAKA 2023/2024 NA 2024/2025**

| MAELEZO | 2023/2024 | 2024/2025 | ONGEZEKO/PUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI MENGINEYO (OC)** | 1,773,383,000.00 | 2,725,125,000.00 | +951,742,000.00 | **53.6** |
| **MISHAHARA** | 1,897,434,000.00 | 1,817,358,000.00 | -80,076,000.00 | **-4.2** |
| **JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA** | **3,670,817,000.00** | **4,542,483,000.00** | +871,666,000.00 | **23.7** |
| **MAENDELEO NDANI** | 1,880,000,000.00 | 1,880,000,000.00 | - | **00** |
| **MAENDELEO NJE** | 20,312,149,000.00 | 11,386,498,000.00 | -8,925,651,000.00 | **-43.9** |
| **JUMLA YA FEDHA ZA MAENDELEO** | **22,192,149,000.00** | **13,266,498,000.00** | -8,925,651,000.00 | **-40.2** |
| **JUMLA** | **25,862,966,000.00** | **17,808,981,000.00** | **-8,053,985,000.00** | **-31.1** |

***Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania 2023/2024 na 2024/2025***

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi umefanyika wa kulinganisha Bajeti ya Tume kwa Mwaka 2023/2024 na 2024/2025 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 3 na kubaini kuna ongezeko kwenye fedha za

matumizi ya kawaida kwa **asilimia 23.7.** Baadhi ya vifungu na kasma zilizoongezewa fedha ni pamoja na Kifungu 1001, Kasma 22010 inayohusu Usafiri wa ndani ya nchi ambapo fedha zimeongezeka kutoka **Shilingi 211,600,000.00** mwaka 2023/2024 hadi **Shilingi 350,640,000.00** mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la **asilimia 65.7,** ongezeko lingine ni katika Kasma 22014 ya Huduma na Ukarimu ambapo fedha zimeongezeka kutoka **Shilingi 13,000,000.00** mwaka 2023/2024 hadi **Shilingi 32,020,000.00** mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la **asilimia 146.** Ongezeko katika Kifungu hicho linatokana na Shughuli ya mikutano ya Wadau kwa ajili ya mapitio ya Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla katika bajeti ya Matumizi ya Kawaida hususan katika Matumizi Mengineyo (OC), uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa fedha zimeongezeka kwa **asilimia 53.6.**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Fedha za Maendeleo za Ndani zimetengwa fedha kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) **Shilingi 1,880,000,000.00** zitakazotumika katika maeneo makuu matatu ambapo **asilimia 60** ni kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa huduma za kuzuia VVU na utoaji elimu ya VVU na UKIMWI; **asilimia 30** zimeelekezwa kuwezesha uendeshaji wa mfuko ikiwemo kugharamia vikao vya kisheria vya kila robo mwaka vya bodi ya mfuko na utafutaji wa rasilimali za kutunisha mfuko; na **asilimia 10** ni kwa ajili ya kukabiliana na madhara ya UKIMWI *(Impact mitigation)* ikihusisha kuwawezesha WAVIU kiuchumi *(Economic Empowerment)*.

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya kupungua kwa fedha za bajeti ya ya Maendeleo kutoka nje, bado bajeti ya Maendeleo kwa kiasi kikubwa inategemea fedha kutoka nje. Kwa hali hii ni dhahiri kwamba bado kuna changamoto ya kutegemea fedha za wafadhili kwa kiwango kikubwa katika kuratibu Masuala ya UKIMWI jambo ambalo linatishia usalama wa WAVIU pale ambapo wafadhili watasitisha kutoa fedha hizo.

## SEHEMU YA TATU

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania – **Fungu 92**, sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

### 4.1 Upatikanaji wa Fedha za Ndani kwa Ajili ya Afua za UKIMWI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza Serikali ifanye yafuatayo:-

i) Itoe fedha zote za Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa muda uliopangwa;

ii) Iimarishe Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI na kuweka mipango madhubuti ya kupata vyanzo mahsusi vya mapato ya ndani vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya miradi inayolenga kudhibiti VVU na UKIMWI; na

iii) Iongeze kiwango cha fedha za ndani inazotenga kupitia Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI (*Aids Trust Fund - ATF)* kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa afua mbalimbali za kudhibiti UKIMWI bila kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi.

### 4.2 Utekelezaji wa Afua za UKIMWI

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza afua za UKIMWI, Serikali imejiwekea malengo ya kufikia asilimia 95-95-95 ifikapo 2030. Hadi sasa, Serikali imefanikiwa katika 95 ya kwanza kufikia asilimia 82, 95 ya pili kufikia asilimia 97 na 95 ya tatu kufikia asilimia 94. Kamati imebaini kuwa kuna changamoto katika kufikia malengo ya asilimia 95 ya kwanza ambayo inahusu kupima na kujitambua. Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo: -

i) Iongeze nguvu na jitihada zaidi katika kufikia shabaha ya kwanza inayohusu watu wote wanaoishi na maambukizi ya VVU kupima na kujua hali zao za maambukizi hususani wanaume; na

ii) Iendelee kutoa elimu kwa jamii kuhusu virusi vya UKIMWI ili kupunguza unyanyapaa pamoja na maambukizi mapya.

### 4.3 Utekelezaji wa Mradi wa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu wa ujasiriamali umelenga kuwafikia Wasichana balehe na Wanawake vijana kwa kiwango kikubwa kwa kutoa huduma jumuishi ya kinga dhidi ya maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI. Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

i) Ianzishe mradi maalum wa ujasiriamali kwa jinsi zote ambao utajumuisha ushiriki wa Wavulana Balehe na Wanaume Vijana;

ii) Ibuni miradi mikubwa yenye tija zaidi itakayosaidia kuinua uchumi kwa WAVIU walio katika vikundi mbalimbali; na

iii) Iongeze wigo wa mradi huu katika Halmashauri na Mikoa mbalimbali nchini ili kufikia na kunufaisha walengwa wengi zaidi.

### 4.4 Utekelezaji wa Afua za UKIMWI Gerezani

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekua ikitekeleza afua mbalimbali za UKIMWI gerezani ili kudhibiti maambukizi ya UKIMWI katika magereza yote nchini. Katika kuboresha na kuimarisha mapambano dhidi ya UKIMWI gerezani, Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

i) Isimamie utekelezaji wa Mwongozo wa Utoaji huduma kwa Wafungwa na Mahabusu uliotolewa terehe 25 Mei, 1998 na Wizara ya Afya ambao ulielekeza kuwa jukumu la kuwatibu Wafungwa na Mahabusu ni la Mganga wa Hospitali ya Serikali katika eneo gereza lilipo; na

ii) Ihakikishe kuna upatikanaji wa uhakika wa dawa magerezani kwa ajili ya kutibu Wafungwa na Mahabusu hususani wakati wa dharura.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Vilevile, nawashukuru na kuwapongeza Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika**, Namshukuru pia Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama (Mb) na Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa walioipatia Kamati wakati wote walipohitajika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Napenda pia kumshukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Dkt. Jim James Yonazi pamoja na Maafisa wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kumshukuru Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Dkt. Jerome Philip Kamwela na Watendaji wote wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kipekee naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Faustin Engelbert Ndugulile, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Bernadeta Kasabango Mushashu, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb - "
6. Mhe. Christopher Olonyokie Ole Sendeka, Mb - "
7. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb - "
8. Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla, Mb - "
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb - "
10. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb - "
11. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - "
12. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb - "
13. Mhe. Josephine Genzabuke, Mb - "
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - "
15. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - "
16. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb - "
17. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb - "
18. Mhe. Seif Salum Seif, Mb - "
19. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb - "
20. Mhe. Zubeida Khamis Shaib, Mb - "
21. Mhe. Jacquiline Andrew Kainja, Mb - "
22. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb - "

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake wakati wote. Kipekee, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John Mvunta na Ndugu Jairo Joseph Odero kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Fungu 92 kiasi cha Shilingi 17,808,981,000.00 ambapo Shilingi 4,542,483,000.00 ni Matumizi ya Kawaida na Shilingi 13,266,498,000.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2024/2025.**

**Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.**

Mhe. Stanslaus Haroon. Nyongo, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA**
**NA MASUALA YA UKIMWI**

3 Aprili, 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kusoma vizuri sana Mwenyekiti. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika kumi.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI WA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Naomba taarifa hii ya Kamati yote iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi na uchambuzi wa Kamati imebainishwa kama ilivyo katika taarifa, lakini sambamba na hilo naomba nizungumzie matokeo ya uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu

Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika mambo makuu manne ambayo yamebainishwa katika ukurasa wa pili hadi wa tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli, kwamba katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 46.5. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2024, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 30.7, sawa na asilimia 66 ya malengo yaliyokusudiwa. Jedwali namba moja katika ukurasa wa tatu hadi ukurasa wa nne wa taarifa hii linaonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 19.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 9.13 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 7.18 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 3.6 ni kwa ajili ya ruzuku na mishahara kwa Wakala wa Usalama Mahali pa kazi *(OSHA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Januari, 2024 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu ilipokea jumla ya bilioni 10.7, sawa na asilimia 54 ya fedha iliyoidhinishwa kama inavyooneshwa katika jedwali Na.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, ilitengewa jumla ya bilioni 14.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 13 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1.33 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2024, ofisi imepokea kiasi cha shilingi bilioni 10.3 sawa na asilimia 69.9 ya fedha zote. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 310.42 ni fedha za nje. Aidha, ofisi ilipokea shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye miradi ambayo ilitengewa fedha, kulikuwa na Mradi wa Programu 6205 ya Kukuza Stadi Za Staha *(decent work country program)* iko pale inajieleza katika ukurasa wa tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Mradi wa 6568 Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini iko pale katika ukurasa wa 10. Marekebisho ya Vyuo na Ujenzi wa Vyuo vya Watu Wenye Ulemavu iko ukurasa wa 11. Vilevile Mradi wa 5441 Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa wa Mapambano dhidi ya UVIKO 19 iko ukurasa wa 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna Mradi 4952 wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Februari, 2024, hakuna fedha ya maendeleo iliyotolewa katika mradi huu. Uchambuzi wa Kamati umebainisha kuwa, katika kipindi cha miaka mitano Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 1.0 tu kati ya shilingi bilioni 5.0 zilizotengwa kwa miaka yote mitano. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha ili kuwawezesha vijana waweze kujishughulisha na shughuli za uzalishaji ili kusaidia kupunguza ombwe la vijana wasio na ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie kuhusiana na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ambayo yako kuanzia ukurasa wa 13 mpaka ukurasa wa 14. Sambamba na hilo uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 umezungumzia kuhusu maduhuli ambayo yanaoneshwa katika ukurasa wa 15. Pia ukurasa wa 16 umezungumzia uchambuzi wa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa fedha za matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, unaonekana katika jedwali Na.7. Sambamba na hilo, uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo umebainishwa kwenye ukurasa wa 18 ambao umezungumzia kwamba katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya

Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu - Fungu 65 limetengewa jumla ya bilioni 14.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 12.6 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1.8 ni fedha za nje. Aidha, Tume ya Usuluhishi - Fungu 15 imetengewa jumla ya milioni 460 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inakwenda mpaka ukurasa wa 18, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kuwa inatoa fedha za maendeleo kwa wakati ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi katika kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati; kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla katika Mafungu yote ambayo yamebainishwa kuanzia ukurasa wa 20 mpaka ukurasa wa 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani nizungumzie mradi mmoja katika yote ambao una mambo ya kusisitiza, nao ni ule Mradi Na. 4952 - Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Utolewaji wa fedha kwa ajili ya Mfuko huu siyo wa kuridhisha. Hivyo, tunaishauri Serikali iweze kutoa hizi fedha ili kusudi vijana waweze kupata mikopo sambamba na hilo kurudisha mikopo. Vilevile zile programu nyingine ziko ukurasa wa 22 na zinaendelea mpaka ukurasa wa 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Serikali ihakikishe kwamba inaongeza bajeti ya kutosha kwa Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi *(OSHA)* ili waweze kuajiri watumishi, kuongeza vitendea kazi vya kuwawezesha kufanya kazi na kuisaidia nchi katika eneo la usalama wa wafanyakazi na pia kuwawezesha wakala kuongeza kasi ya kukagua maeneo mengi zaidi nchini. Taarifa nyingine inaendelea ukurasa wa 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye hitimisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii.

Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za Kudumu za Bunge kama zilivyowasilishwa na taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Paschal Katambi kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi katika ofisi yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bi. Mary Ngelela Maganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi *ndc*, kwa kuratibu shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kwa Mheshimiwa Naibu Spika, 2024/2025 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**3 APRILI, 2024**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi; Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha2023/2024;

b) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

c) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na

d) Sehemu ya Tano ni hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kanuni ya 6 (5)(a)

ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, zinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya ofisi hii.

Aidha, Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa na kwamba naliomba Bunge lako Tukufu liijadili hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu pamoja na Taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inagusa mafungu mawili. **Fungu 65** ambalo ni Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na **Fungu 15** ambalo ni Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA). Naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mafungu yote mawili tarehe 21 na 25 Machi 2024.

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu Hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika mambo makuu manne yafuatayo:-

(a) Makusanyo ya maduhuli;

(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya kawaida;

(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na

(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni.

### 2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 46,500,000,000**. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilikuwa imekusanya **Shilingi 30,702,341,017.80** sawa na **Asilimia 66** ya malengo yaliyokusudiwa. Vyanzo vya makusanyo hayo ni Ada za Vibali vya Ajira za Wageni **Shilingi 30,323,141,017.80,** Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira **Shilingi 61,500,000,** Ada za Maombi ya kufanya kazi nje ya Nchi **Shilingi 312,450,000** na Mapato mengineyo **Shilingi 250,000**. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekena katika Jedwali Na. 1.

**JEDWALI NA. 1: FUNGU 65 - MAKADIRIO NA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

| **MAKADIRIO NA MAKUSANYO 2023/2024** | | | |
|---|---|---|---|
| **Chanzo** | **Makadirio (tsh.)** | **Makusanyo (tsh.)** | **Asilimia** |
| Ada za Vibali vya ajira za Wageni | 43,975,630,595.00 | 30,323,141,017.80 | 69 |
| Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira | 175,000,000 | 61,500,000 | 35 |
| Uuzaji wa Nyaraka za Zabuni | 4,625,000 | 0 | 0 |
| Pango la Mnara wa Simu | 12,000,000 | 0 | 0 |
| **MAKADIRIO NA MAKUSANYO 2023/2024** | | | |
| **Chanzo** | **Makadirio (tsh.)** | **Makusanyo (tsh.)** | **Asilimia** |
| Ada za Pango | 8,492,400 | 0 | 0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi | 2,330,000,000 | 312,450,000 | 13 |
| **Jumla** | **46,500,000,000.** | **30,702,341,017.80** | **66** |

***Chanzo: Randama ya Bajeti ya 2023/2024 Fungu 65***

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

(a) Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa jumla ya **Shilingi 30,702,341,017.80** sawa na **asilimia 66** ya makusanyo yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu yalikusanywa katika kipindi hicho.

(b) Baadhi ya vyanzo vya mapato havijakusanya kabisa na vingine vimekusanya chini ya aslimia 50.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati imebaini kuwa mwenendo wa makusanyo kwa mwaka huu kwenye baadhi ya vyanzo vya makusanyo si wa kuridhisha. Mathalani, Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira imekusanya kwa asilimia 35 na Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi ni asilimia 13 tu. Kamati imeona kuwa sababu za makusanyo kuwa madogo kwenye baadhi ya vyanzo hivi ni kutokana na kasi ndogo ya kuwaunganisha Watanzania na fursa za ajira za nje ya nchi na kuchelewa kusaini makubaliano ya ushirikiaono wa uratibu wa ajira za Watanzania na nchi za kimkakati ambazo zina fursa nyingi za ajira. Aidha sababu nyingine ni uhaba wa Watumishi katika Idara ya Kazi nchini jambo linalopelekea kushingwa kufanya kaguzi za mara kwa mara kwenye maeneo yenye Waajiri wa Kigeni na kukosekana kwa mfumo wa kukusanya mapato yanayotokana na ujira kutoka kwa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi.

## 2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 19,920,510,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 9,138,868,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 7,180,664,682.06** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 3,600,977,317.94** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahala pa kazi (OSHA).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilipokea jumla **Shilingi 10,785,839,998.98** sawa na **asilimia 54.1** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 4,002,681,588.85** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 4,845,598,246.20** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 2,791,283,552.00** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahala pa kazi (OSHA). Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

**JEDWALI NA. 2: MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2023/2024**

| **MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2023/2024** | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2023/2024** | **Fedha zilizopokelewa** | **Asilimia ya mapokezi** |
| Mishahara | **7,180,664,682.06** | 4,845,598,246.20 | 67 |
| Oc | **9,138,868,000.00** | **4,002,681,588.85** | 44 |
| Ruzuku ya mshahara (OSHA) | **3,600,977,317.94** | 2,791,283,552 | 78 |
| **Jumla** | **19,920,510,000** | **10,785,839,998.98** | **54.1** |

***Chanzo:*** *Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 65*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba kwa ujumla, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (**Fungu 65)** imepokea jumla ya **Shilingi**

**10,785,839,998.98** sawa na **asilimia 54.1** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kwaida.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) **Fungu 15** iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 5,181,056,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo kiasi cha **Shilingi 2,664,898,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 2,516,158,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2023, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 2,906,739,847** sawa na **asilimia 56** Mchanganuo wa Fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2023 ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na.3

**JEDWALI NA. 3: MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2023/2024**

| **MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2023/2024** | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2023/2024** | **Fedha zilizopokelewa** | **Asilimia ya mapokezi** |
| Mishahara | **2,664,898,000.00** | 1,364,302,000.00 | 51.2 |
| Oc | **2,516,158,000.00** | 1,542,437,847 | 61.3 |
| Jumla | **5,181,056,000** | **2,906,739,847** | 56 |

***Chanzo:*** *Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 15.*

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi kuhusu mwenendo wa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Fungu 65 na 15 Kamati imebaini masuala yafuatayo;

(a) Mapokezi ya fedha za Matumizi ya kawaida kwa **Fungu 65** ni **Shilingi 10,785,839,998.98** sawa na **asilimia 54.1** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

(b) **Fungu 15** limepokea fedha ya matumizi ya kawaida kiasi cha **Shilingi 2,906,739,847** sawa na **asilimia 56** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida si wa

kuridhisha. Hivyo ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe kiasi cha fedha kilichosalia kwa mafungu yote mawili kabla ya tarehe 30 Juni ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## 2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi wa Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilitengewa jumla ya **Shilingi 14,749,713,680** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 13,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,334,936,275** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2024 Ofisi imepokea kiasi cha **Shilingi 10,310,422,480.00**, sawa na **asilimia 69.9** ya fedha zote. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 10,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 310,422,480.00** ni fedha za Nje. Aidha Ofisi ilipokea **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya Mfuko wa Watu wenye Ulemavu ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati wa kuhitimisha bajeti ya Serikali ya Mwaka 2023/202**.** Mgawanyo wa fedha hizo umeainishwa katika Jedwali Na. 4.

**JEDWALI NA. 4: FUNGU 65 - MITADI YA MAENDELEO ILIOTENGEWA FEDHA 2023/2024**

| MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2023/2024 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Namba na jina la mradi** | **Bajeti iliyotengwa 2023/2024** | | **Mapokezi ya fedha hadi kufikia marchi 2024** | | **Asilimia ya mapokezi** |
| | **Fedha za ndani** | **Fedha za nje** | **fedha za ndani** | **fedha za nje** | |
| Na. 6205: Programu ya Kukuza Kazi za Staha Nchini | 0.00 | 1,334,936,275 | | 310,422,480.00 | 23 |
| Na. 6581: Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini | 9,000,000,000 | 0 | 9,000,000,000 | 0 | 100 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Na.4954 ujenzi wa vituo vya Ufundi na Ukarabati wa vyuo vya watu wenye ulemavu | 3,000,000,000 | 0 | 0 | | 0 |
| Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu | 1,000,0000,000 | | 1,000,000,000 | 0 | 100 |
| Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana | 1,000,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla Kuu** | **13,000,0000,000** | | **10,000,000,000** | **310,422,480** | **69.9** |

***Chanzo.*** *Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 65.*

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **Fungu 15,** Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) inatekeleza mradi mmoja wa mfumo wa Usimamizi wa Uendeshaji Mashauri (ECMS). Mradi huu uliidhinishiwa **Shilingi 700,000,000.** Hadi kufikia Februari 2024, Tume ilikuwa imepokea **Shilingi 396,265,000.00** sawa na **asilimia 57** ya fedha zilizoidhinishwa**.**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Maendeleo kama ifuatavyo:-

(a) Kwa ujumla mapokezi ya fedha za maendeleo kwa Fungu 65 ni **asilimia 69.9** ambapo mapokezi ya fedha za nje yapo chini ya kiwango kilichotarajiwa ambapo ilipokea **asilimia 23.2** ya makadirio. Hali hii ya mapokezi ya fedha za nje yameathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopangwa;
Aidha Fungu 15 limepokea **asilimia 57** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo.

(b) Kamati pia imebaini kwamba, **Fungu 65** ilitengewa **Shilingi 3,000,000,000** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya ufundi

vya watu wenye ulemavu na **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Hata hivyo hadi kufikia Februari 2024 hakuna fedha yoyote iliyopokelewa na Ofisi hiyo kutekeleza miradi husika. Ni maoni ya Kamati kuwa mwenendo huu wa mapokezi ya fedha hauleti tija na unaweza kuathiri utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kujua sababu za kutolewa kidogo kwa fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo ambapo ilibainika kwamba ni kutokana na ucheleweshaji kutoka kwa wadau wanaohusika. Kamati inashauri mawasiliano yaendelee kufanyika ili fedha hizo zitolewe kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha hapo Juni, 2024 ili Miradi iliyopangwa kutekelezwa itekelezwe na kuwapatia wananchi huduma zilizokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya miradi mitano ilitekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Kamati ilifuatilia na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

### 2.4.1 Mradi Na. 6205 Programu ya Kukuza Kazi za Staha (Decent Work Country Program)

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unahusu kukuza na kujenga stadi za Maisha kwa vijana kupitia programu ya kazi za staha. Taarifa zinaonyesha kuwa, fedha zinazotumika kutekeleza mradi huu ni fedha za nje kwa asilimia mia moja. Jumla ya **Shilingi 1,334,936,275** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia Februari, mradi ulipokea **Shilingi 310,422,480.**

Aidha, Kamati ilibaini kuwa miongoni mwa kazi zilizofanyika ni kufanya tathmini na mapitio ya sera ya vijana ya 2007 na Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii. Mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa watu wenye ulemavu ya Mwaka 2004, kuratibu ushiriki wa vijana kumi kwenye mkutano wa sita wa jukwaa la Vijana Afrika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa tija ya mradi huu bado haijaonekana kwa kuwa bado upo katika hatua za awali na haujafikia idadi kubwa ya walengwa. Kamati ina maoni kuwa Ofisi ya

Waziri Mkuu ilijielekeze zaidi kwenye programu za kujenga staha za Maisha kwa vijana ili kuleta tija ya mradi huu.

### 2.4.2 Mradi Na. 6581 Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 9,000,000,000**. Hadi kufikia Februari, 2024 programu hii ilikuwa imepokea **Shilingi 9,000,000,000.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu katika chuo cha St. Antoni Vocational Training CentreMusoma na Chuo cha RVPSC- Mwanza ambapo jumla ya vijana 272 wanapata mafunzo ya uanagenzi katika vyuo hivyo. Lengo la ziara ilikuwa ni kuona utekelezaji wa mradi huu na kubainisha mafanikio na changamoto za utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Programu ya Uanangezi imetoa mafunzo kwa vijana 9,593 na vijana 6,000 wameanza mafunzo mwezi Januari 2024. Hata hivyo Kamati ilibaini kuwa upatikanaji wa vijana katika mradi huu bado haujulikani miongoni mwa Watanzania. Serikali ihakikishe inamrahisishia mwananchi kupata taarifa kuhusu programu hii ili kuwezesha vijana wengi kunufaika na fursa hii. Vilevile udadisi wa Kamati ulidhihirisha kuwa vijana wanaonufaika na mafunzo haya hupata ujuzi wenye manufaa, lakini inakuwa vigumu kwa ujuzi huo kuwasaidia katika Maisha halisi. Sababu ya ugumu huo ni ukosefu wa mitaji ya kupata vifaa na vitendea kazi vya kuweza kujiajiri na kuajiri wengine. Hali hiyo isipofanyiwa kazi, programu ya kukuza ujuzi nchinihaitakuwa na tija.

### 2.4.3 Marekebisho na Ujenzi wa Vyuo vya Watu Wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutimiza takwa la kikanuni la kukagua Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Marekebisho kwa vijana wenye Ulemavu Bujora- Mwanza. Kamati ilijulishwa kuwa thamani ya mradi ni **Shilingi 504,596,806.67** ambazo ni fedha kutoka Shirika la GIZ. Ujenzi huo unahusisha Madarasa 10, Vyoo 20, Ofisi za

Walimu 8 na unatarajia kukamilika mwezi Aprili, 2024. Kamati ilibaini kuwa, kasi ya utekelezaji wa mradi huu si ya kuridhisha licha ya fedha zote kutolewa kwa wakati.

### 2.4.4 Mradi Na.5441 Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu umewezesha kufanya ukarabati wa vyuo vinne vya Ufundi Stadi na Marekebisho ambavyo ni Luanzari-Tabora, Sabasaba- Singida, Mtapika Masasi Mtwara na Yombo- Dar Es Salaam na umegharimu kiasi cha **Shilingi 3,468,608,626** Ukarabati huu umewezesha vyuo vilivyokuwa vimefungwa kufunguliwa na kuanza kutoa mafunzo.

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 12 Machi 2024 Kamati ilipata fursa ya kutembelea Chuo cha Ufundi Stadi cha Watu wenye Ulemavu na Marekebisho Luanzari- Tabora. Kamati ilielezwa kuwa thamani ya mradi wa ukarabati katika chuo hiki ni **Shilingi 689,004,953.17** ambapo gharama za vifaa ni Shilingi 484,744,670, ufundi ni Shilingi 146,936,429.50 na gharama za vifaa vya kufundishia ni Shilingi 57,323,850. Ukarabati huo ulihusisha ukarabati wa jengo la Karakana, Jengo la Utawala, Bweni la Wavulana, bwalo la chakula, Bweni la Wasichana, Jiko, Vyoo, na nyumba 3 za watumishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi huu ambao umegharimu kiasi cha **Shilingi 689,004,953.17** ambapo kwa uhalisia kiasi hicho cha fedha hakiendani na hali ya utekelezaji wa mradi. Aidha, utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu licha ya kupatiwa fedha zote kwa wakati. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ihakikishe fedha inayopelekwa kutekeleza miradi inatumika kama ilivyokusudiwa na ujenzi uendane na thamani ya fedha inayotumika katika kutekeleza miradi hiyo.

### 2.4.5 Mradi Na. 4952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Februari 2024, hakuna fedha ya maendeleo iliyopokelewa katika mradi huu. Uchambuzi wa kamati unaonesha kuwa katika kipindi cha miaka mitano Serikali imetoa kiasi cha Shilingi 1,000,000,000 tu kati ya Shilingi 5,000,000,000 zilizokuwa zimetengwa kwa miaka yote mitano hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya mkopo kwa vijana na kusababaisha kushindwa kutekeleza malengo yaliyokusudiwa. Mathalani katika mwaka wa fedha 2022/2023 mahitaji ya mkopo yaliyowasilshwa Ofisi ya Waziri Mkuu yalikuwa na thamani ya shilingi 6,700,000,000 ikilinganishwa na fedha iliyokuwepo ambayo ni Shilingi 3,600,000,000(Revolving Fund).

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha katika mradi huu ili kuwawezesha vijana wengi kufanya shughuli za uzalishaji na hivyo kusaidia kupunguza ombwe la vijana wasio na ajira nchini.

**2.4.6 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa utekelezaji unaridhisha na kwa baadhi ya maeneo Ofisi inaendelea na utekelezaji wa ushauri huo wa Kamati kwa kuwa utekelezaji wake ni endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** ushauri ambao haujazingatiwa ni pamoja na Serikali kuongeza Bajeti ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ili mfuko uweze kuwafikia vijana wengi. Bajeti hii haikuongezwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 na badala yake imeshuka hadi kufikia Shilingi 657,252,862. Kamati haioni nia thabiti ya Serikali ya kuwawezesha vijana kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu ili kuanzisha na kuendeleza miradi yao ya uzalishaji mali.

**Mheshimiwa Spika,** Programu ya Ukuzaji Ujuzi Nchini pia haijaongezewa bajeti kwa kuzingatia makubaliano baina ya Sekta Binafsi na Serikali ambapo moja ya tatu ya tozo ya SDL inatakiwa

itumike kugharamia programu hii. Kamati inaendelea kushauri kuwa Serikali itenge moja ya tatu kama ilivyo kwenye makubaliano ili zielekezwe katika kuwaongezea ujuzi na kufikia lengo la kuongeza ujuzi kwa vijana 681,000 wanaotakiwa kupata mafunzo haya katika kipindi cha miaka mitano.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya Shilingi **40,500,000,000** ikilinganishwa na **Shilingi. 46,505,749,995** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Makadirio yamepungua kwa **Shilingi 6,005,749,995** sawa na **asilimia 13** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha. Fedha hizi zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika ada za maombi ya Vibali vya Kazi kwa Wageni, Malipo ya Usajili wa Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira nchini, Ada za maombi ya kufanya Kazi nje ya Nchi na kodi ya mnara wa mawasiliano. Mchanganuo wa lengo la kukusanya kwa Fungu 65unaonekana katika Jedwali Na.5 hapa chini.

**JEDWALI NA. 5: FUNGU 65 - ULINGANISHO WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025**

| MAKADIRIO NA MAKUSANYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025 | | | |
|---|---|---|---|
| **Maelezo** | **2023/2024 (Tsh.)** | **2024/2025 (Tsh.)** | **Asilimia/Pungufu au ongezeko** |
| Ada za Vibali vya ajira za Wageni | 43,975,630,595 | 38,154,505,600 | -13.2 |
| Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira | 175,000,000 | 174,000,000 | -0.57 |
| Uuzaji wa Nyaraka za Zabuni | 4,625,000 | 8,492,400 | 84 |
| Pango la Mnara wa Simu | 12,000,000 | 12,000,000 | o |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi. | 2,330,000,000 | 2,325,000,000 | -0.21 |
| **Jumla** | **46,505,749,995** | **40,500,000,000** | **-13** |

***Chanzo***: *Randama ya Bajeti ya 2023/2024 fungu 65.*

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

(a) Makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamepungua kwa **Shilingi 6,005,749,995** sawa na punguzo la **asilimia 13**

(b) Makusanyo ya maduhuli kutoka kwenye chanzo cha ada za Vibali vya Ajira kwa Wageni kimepungua kwa asilimia 13.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji ili kutaka kujua sababu ya kupungua kwa makisio ya maduhuli ambapo ilibainika kuwa ni kutokana na baadhi ya miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inaajiri wageni wengi kukamilika. Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuweka mikakati thabiti ya kuwaunganisha Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi na kuweka mfumo madhubuti wa kukusanya mapato kwa yatokanayo na ujira kwa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi ili kuongeza mapato.

**3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu **Fungu 65** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 23,776,408,000** ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 7,798,238,676** ni mishahara, **Shilingi 5,339,301,324** ruzuku ya mishahara OSHA na **Shilingi 10,638,868,000** ni matumizi mengineyo (OC). Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 19** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo iliidhinishiwa **Shilingi 19,920,510,000** kati ya Fedha hizo **Shilingi 9,138,868,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 7,180,664,682.06** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 3,600,977,317.94** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahali pa kazi (OSHA) kama ilivyochanganuliwa katika Jedwali Na. 6

**JEDWALI NA. 6: FUNGU 65 - ULINGANISHO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025**

| **ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 65 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **2023/2024 (Tsh.)** | **2024/2025 (Tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** |
| Mishahara | 7,180,664,682 | **7,798,238,676** | 617573994 | 9 |
| OC | 9,138,868,000 | **9,138,868,000** | 0 | 0 |
| Ruzuku | 3,600,977,317 | **5,339,301,324** | 1,738,324,010 | 48.2 |
| **Jumla** | **19,920,510,000** | **23,776,408,000** | **3,855,898,000** | **19** |

***Chanzo:*** *Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 65*

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **Fungu 15** imekadiriwa kutumia kiasi cha **Shilingi 6,308,976,000** sawa na ongezeko la **asilimia 7.2** Ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2023/2024. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 2,861,776,000** ni kwa ajili ya Mishahara sawa na ongezeko la **asilimia 7.3** na **Shilingi 2,861,776,000** kwa matumizi mengineyo sawa na ongezeko la **asilimia 14.** Mgawanyo wa fedha za matumizi kwa Mwaka 2024/2025 ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 7.

**JEDWALI NA. 7: FUNGU 15 - ULINGANISHO WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA**

| **ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 15 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **2023/2024 (Tsh.)** | **2024/2025 (Tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** | **Ongezek/ pungufu (%)** |
| Mishahara | 2,664,898,000 | 2,861,776,000 | 196,878,000 | 7.3 |
| OC | 2,516,158,000 | 2,861,776,000 | 345,618,000 | 14 |
| **Jumla** | **5,881,056,000** | **6,308,976,000** | **427,920,000** | 7.2 |

***Chanzo.*** *Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 15*

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala yafuatayo:-

(a) **Fungu 65** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **asilimia 19** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha.

(b) **Fungu 15** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **asilimia 7.2** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili la asilimia 12 katika Fungu 65 ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ni matumaini ya Kamati kuwa fedha hizo zitatolewa kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, (Fungu 65) imetengewa jumla ya **Shilingi 14,491,388,000** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 12,629,011,000** ni fedha za ndani, na **Shilingi 1,862,377,000** ni fedha za nje. Aidha katika Tume ya Usuluhishi (CMA) Fungu 15 imetengwa jumla ya **Shilingi 460,077,000** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 8.

**JEDWALI NA. 8: FUNGU 65 ULINGANISHO WA BAJETI YA FEDHA ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHADHA 2023/2024 NA 2024/2025**

| ULINGANISHO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2023/2024 na 2024/2025 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NAMBA NA JINA LA MRADI** | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024** | | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025** | |
| | **Fedha za ndani** | **Fedha za nje** | **Fedha za ndani** | **Fedha za nje** |
| Na. 6205: Programu ya Kukuza Kazi za Staha Nchini | 0 | 1,334,936,275 | 0 | 1,402,474,504 |
| Na. 6581: Programu | 9,000,000,000 | 0 | 10,807,383,821 | 0 |
| ya Kukuza Ujuzi Nchini | | | | |
| Na.4954 Mfuko wa Watu wenye Ulemavu (GIZ) | 0 | 0 | 0 | 459,905,245 |
| Mfuko wa Watu wenye Ulemavu | 1,000,000,000 | 0 | 1,619,286,666 | 0 |
| Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana | 1,000,000,000 | 0 | 657,252,868 | 0 |
| **Jumla Kuu** | **11,000,000,000** | **1,334,936,275** | **12,629,011,000** | **1,862,377,000** |

***Chanzo.*** *Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 65.*

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo Kamati ilibaini kuwa Bajeti ya fedha za Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 zimeongezeka kwa **Shilingi 1,629,011,000** sawa na **asilimia 15** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha. Kamati imebaini kuwa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana zimepungua kwa **Shilingi 342,747,132** sawa na **asilimia 34.** Aidha Fedha za Programu ya Kukuza Ujuzi zimeongeka kwa **Shilingi 1,807,383,821** sawa na **asilimia 20** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati kwa kuongeza bajeti ya Proramu hii, hata Kamati bado inaona ongezeko hilo haliendani na makubaliano ya matumizi ya Tozo ya Maendeleo ya Ujuzi (SDL) baina ya Serikali na Sekta Binafsi kuwa moja ya tatu ya

mapato yatumike katika programu hii. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kuongeza bajeti katika miradi hii ili kupunguza wimbi la vijana wasiokuwa na ajira.

Aidha, Bajeti ya fedha za maendeleo za nje zimeongezeka kwa **Shilingi 527,440,728** sawa na asilimia 40 ilkilinganishwa na mwaka unaoisha. Kwa Upande Mwingine fedha za miradi ya Maendeleo kwa Fungu 15 zimepungua kwa **Shilingi 239,993,000** sawa na **asilimia 34** Jambo litaloathiri ukamilishaji wa usimikaji wa mfumo wa kieletroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha za maendeleo ili Ofisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

i) Kamati imebaini kuwa mwenendo wa makusanyo ya Mapato kwa **Fungu 65** kwenye baadhi ya vyanzo vya makusanyo si wa kuridhisha.Mathalani, Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira wamekusanya kwa **asilimia 35** na Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi ni **asilimia 13 tu**. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kusaini Makubaliano ya ushirikiano wa ajira na nchi za kimkakati ambazo zina fursa nyingi za ajira kwa Watanzania ili kuweza kupata ajira nyingi na kuongeza mapato ya nchi. Aidha Serikali iharakishe uboreshaji wa mfumo wa kukusanya mapato yanayotokana na ujira kutoka kwa

Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi ili kuongeza mapato ya nchi.

ii) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuna sababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua. Hivyo, serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio. Aidha Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa upatikanaji wa fedha za nje ni wa kusuasua;

iii) Katika **Mradi Na. 4952, Mfuko wa Maendeleo wa Vijana** utolewaji wa fedha kwa ajili ya mfuko huu si wa kuridhisha, kwani katika kipindi cha miaka mitano Serikali imetoa kiasi cha Shilingi 1,000,000,000 tu kati ya Shilingi 5,000,000,000 zilizokuwa zimetengwa kwa miaka yote mitano hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya mkopo kwa vijana na kusababisha kushindwa kutekeleza malengo yaliyokusudiwa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa fedha hizi kila mwaka na kwa wakati na kuongeza kiasi cha mtaji wa mfuko huu ili kuongeza idadi ya vijana wanaopata mkopo kupitia mfuko huu ili waweze kupata mtaji wa kuanzisha shughuli za uchumi. Aidha Kamati inaishauri Serikali kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza mtaji wa mfuko huu kuliko kutegemea ruzuku kutoka Serikalini kama ilivyo sasa.

iv) Kutorejeshwa kwa mikopo inayotolewa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kunapelekea kutofikiwa lengo la kuendelea kukopesha vijana wengine. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa fedha zinazokopeshwa zinarejeshwa kwa wakati ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika na mradi huu.

v) **Mradi Na. 6581 Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini**. Kamati ilibaini kuwa mwenendo wa mgao wa fedha kwaajili ya utekelezaji wa programu hii umekuwa ukishuka kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano kinyume na makubaliano ya matumizi ya michango wanayotozwa waajiri ya kukuza ujuzi (Skills and

Development Levy-SDL) jambo lililosababisha kushuka kwa idadi ya vijana wanufaika kutoka wastani wa vijana 42,000 hadi 12,000. Kamati inashauri kuwa Serikali itenge na kutoa fedha za programu hii kwa kufuata makubaliano ya kutoa 1/3 ya michango wanayotozwa waajiri ya kukuza ujuzi(SDL) ili kuweza kuongeza idadi ya vijana na kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa jumla ya vijana 681,000 wanaotakiwa kupata mafunzo ya ujuzi katika kipindi cha miaka mitano. vi) Serikali ihakikishe kuwa ujuzi unaopatikana katika programu ya uanagenzi haupotei. Serikali ione namna ya kutoa vifaa/ vitendea kazi kwa vijana wanaonufaika na programu hii ili waweze kujiajiri na kuajiri wengine. Aidha, Serikali ione namna ambayo mikopo itokanayo na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana inawanufaisha vijana ambao tayari wana mafunzo mbalimbali yanayotolewa na programu hii.

vii) Fedha za Maendeleo kwaajili ya kusimika mfumo wa kieletroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu katika **Fungu 15** zimeshuka kutoka **Shilingi 700,000,000** katika mwaka wa fedha 2023/2024 hadi **Shilingi 460,007,000,000** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 jambo linaloathiri ukamilishaji wa usimikaji wa mfumo huu. Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya Tume, sambamba na kutoa fedha kwa wakati ili waweze kusimika mifumo katika mikoa yote 32 nchini ili kuongeza ufanisi wa utatuzi wa migogoro na kuendana na mfumo wa kielektroniki unaotumiwa na Mahakama.

viii) Ukarabati na Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi naMarekebisho kwa Watu wenye Ulemavu umechukua muda mrefu licha ya fedha zote kutolewa kwa wakati. Serikali ihakikishe kuwa Ujenzi na Ukarabati wa vyuo hivyo unakamilika kwa wakati na ujenzi huo uendane na thamani ya fedha inayotumika katika kutekeleza miradi hiyo.

ix) Serikali ihakikishe kwamba inaongeza Bajeti ya kutosha ya Wakala wa Usalama na afya mahala pa kazi (OSHA) ili waweze kuajiri watumishi na kuongeza vitendea kazi vya kuwawezesha kufanya kazi ya kuisaidia nchi katika eneo la usalama wa

wafanyakazi na pia itawezesha Wakala kuongeza kasi ya kukagua maeneo mengi ya kazi Nchini.

x) Kukosekana kwa Mfumo wa kukusanya mapato kwa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi kunapelekea nchi kukosa mapato. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha kwa haraka Mfumo utakaowezesha kupata mapato yatakayotumwa nchini kama sehemu ya ujira kwa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi.

xi) Serikali iweke mikakati na kuongeza kasi ya kuwaunganisha Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi kwa kusaini makubaliano ya kuratibu ajira za Watanzania na nchi nyingi zaidi za kimkakati ambazo zina fursa nyingi za ajira ili kuongeza ajira, kipato kwa Watanzania na nchi kwa ujumla.

xii) Watu wenye ulemavu wamekuwa hawajumuishwi vya kutosha kwenye programu mbalimbali nchini. Kamati inashauri kuwa Serikali iweke mkakati maalumu wa kuwajumuisha watu wenye ulemavu kwenye Programu ya Taifa ya kukuza ujuzi nchini na programu zingine ili kuhakikisha kuwa fursa kwa watu wenye ulemavu zinaimarishwa.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb. – Mwenyekiti
2. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb. – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe.Tamima Haji Abass, Mb.
4. Mhe.Neema Gerald Mwandabila, Mb.

5. Mhe.Tecla Mohamedi Ungele, Mb.
6. Mhe.Kabula Enock Shitobela, Mb.
7. Mhe.Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb.
8. Mhe. Katani Ahmadi Katani, Mb.
9. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
10. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb.
11. Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb.
12. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
13. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb.
14. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb.
15. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
16. Mhe. Sanya Juma Jafar, Mb.
17. Mhe. Shanif Mansoor Jamal, Mb.
18. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb.
19. Mhe. Neema Kachiki Lugangira, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe.Deogratius John Ndejembi, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Naibu Waziri Mhe. Paschal Patrobass Katambi, Mb kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Bi. Mary Ngelela Maganga.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. hoja.

Fatma Hassan Toufiq, Mb
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii**
03 Aprili, 2024

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kusoma vizuri. Waheshimiwa Wabunge sasa tunaanza mjadala, Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika hotuba ya bajeti iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitangulie kutoa taarifa za masikitiko makubwa. Katika Jimbo letu la Kilwa Kaskazini, siku nne zilizopita tulipatwa na maafa makubwa ya mafuriko kutokana na mvua kubwa za *El-Nino* zinazoendelea kunyesha katika Milima ya Matumbi zilizosababisha kupoteza maisha ya watoto wetu wawili waliokuwa wakisoma darasa la sita katika Kijiji cha Chumo. Tulimpoteza kijana wetu mdogo anaitwa Hawa Haji Kekarange, lakini pia tulimpoteza Abdul Aziz Kapanda. Mwenyezi Mungu aziweke roho zao marehemu hawa mahali pema peponi. Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kuchangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu moja kwa moja leo nitajikita katika upande wa sekta ya barabara ambayo imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mvua za *El-Nino* hapa nchini. Changamoto ni kubwa na tusipozifanyia kazi katika kipindi hiki, basi hata ile asilimia 5.4 ya ukuaji wa uchumi inaweza isifikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa barabara hii ya Tingi **-** Kipatimu. barabara ile ambayo ipo katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini imeathirika sana. Barabara ile tangu tarehe 9 Desemba,

2023 ilipata changamoto kubwa za kutopitika. Vilevile, sababu siyo tu mvua za *El-Nino* bali pia kumekuwepo na malori yenye uzito mkubwa usiolingana na uwezo wa barabara, madaraja na makalavati yaliyopo kule ambao umesababisha madaraja yabomoke kabla hata ya mvua na mafuriko ya juzi na matokeo yake upitikaji wa barabara umekuwa mgumu. Tuzingatie kwamba yale malori yamekuwa yakifanya kazi kubwa ya kupeleka malighafi za ujenzi wa bandari ya uvuvi kule Kilwa Masoko (Mradi mkubwa wa kimkakati ambao Serikali yetu imewekeza kwa kiasi kikubwa). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuzorota kwa barabara ile kumesababisha hata ule Mradi wa Kilwa Masoko wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi nao umezorota kwa sababu hayapeleki ile malighafi ya mawe ya ujenzi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutokana na *El-Nino* mambo ndiyo yamekuwa magumu zaidi, juzi tu yalipotokea yale mafuriko maeneo manne ya tuta la barabara yaliyo jirani kabisa na madaraja pamoja na makalavati yamekatika na sasa barabara ile haipitiki kabisa kwa asilimia mia moja pamoja na umuhimu wake huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba barabara ile inakwenda kwenye kumbukumbu za Maji Maji ambazo zitatuongezea ufanisi katika utalii ambazo umepata *GN* hivi majuzi. Kwa hiyo, naiomba Serikali iiangalie ile barabara kwa jicho la pekee na kwa kuwa barabara ile ina milima mirefu ambayo inatiririsha maji kila siku. Kwanza Serikali ichukue hatua ya kurekebisha miundombinu ya barabara ile ili sehemu kubwa ya barabara ipite juu ya milima badala ya kupita bondeni. Kwa mfano, mafuriko yaliyotokea juzi yametokea katika Bonde la Chumo ambalo lina urefu wa zaidi ya kilometa tano na barabara imepita humo humo kwenye bonde. Kwa hiyo, nafikiri kwamba sasa wataalam wetu wabuni utaratibu ambao barabara hii isipite sehemu ya mabonde pale ambapo hakuna ulazima wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo napenda kuishauri Serikali ni kwamba, barabara ile katika maeneo yenye miinuko mikali, tutengeneze barabara za zege ili ziwe na uhakika wa

kupitika muda wote wa mwaka. Pia wawepo wenzetu wa *TARURA* na *TANROADS* waweze kuhudumia ipasavyo kupitia bajeti ambayo tutaipitisha hapa keshokutwa na pia hata zile fedha za dharura zinazopelekwa kwa ajili ya barabara zetu za *TANROADS* na *TARURA*, nyingi zimekwenda katika maeneo ambayo siyo ya kipaumbele. Kwa mfano, kuna barabara ya kijijini kutoka Kipatimu kwenda Kibata makalavati na madaraja yalivunjika tangu tarehe 9 Desemba, mvua kubwa za *El-Nino* zilipokuwa zimepamba moto, mpaka wakati huu ile barabara ambayo ilipewa *first priority* na wenzetu wa *TARURA* haijashughulikiwa. Badala yake milioni 200 zilizoletwa kwa ajili ya dharura zimepelekwa kwenye barabara ambayo ni *priority* namba sita kwa mujibu wa ushauri wa wataalam wetu. Naomba *priorities* za wataalam zizingatiwe ili kule ambako kuna changamoto kubwa, basi *solution* iweze kupatikana mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nina ushauri wa kitaifa, janga la *El-Nino* limetokea nchi nzima na maafa yamekuwa makubwa. Kwa hiyo, tunahitaji uwekezaji mkubwa kwenye barabara zetu zote hapa nchini, kwamba bajeti ya Wizara yetu ya Ujenzi iweze kuongezwa hadi kufikia asilimia 30 ya bajeti nzima ya Serikali Kuu ili asilimia 60 za zabuni ziweze kutangazwa mapema mara tunapokuwa tumepitisha bajeti zinazohusika na barabara. Keshokutwa tukipitisha kuanzia *TARURA* basi wapewe ruhusa ya kuweza kutangaza zabuni. Pia *TANROADS* wapewe ruhusa angalau asilimia 60 itangazwe mara moja tutakapopitisha bajeti ili mwaka wa fedha unapoanza na kazi ya marekebisho makubwa ya barabara ambazo zimeathirika kwa kiasi kikubwa na mvua za *El-Nino* ianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne ambalo ningependa kushauri ni kwamba, fedha za dharura pia zitengwe, tusisubiri mpaka dharura itokee. Hata kama zitakaa Makao Makuu ya *TANROADS* au Wizarani siyo mbaya ili dharura itakapotokea mara moja kazi ya kurekebisha miundombinu iliyoathirika iweze kwenda kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitengo vinavyohusika na *technical audit* kule *TANROADS* na kule *TARURA* pia viimarishwe kwa kupewa fedha za kutosha kwa ajili ya kumudu kufanya kazi zao. Kuongezewa vile vile watumishi au wataalam wa kutosha ili waweze kushughulika

na changamoto zote zinazoendelea na waweze kupewa vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika changamoto ambayo ilionekana Mkoani Lindi na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ya kukuta mtaalam wa falsafa anasimamia barabara na maeneo mengine inasemekana wapo wataalam wa minyororo baridi na wataalam wa saikolojia ambao wanasimamia barabara. Hili tatizo lingeweza kuonwa na *technical auditors* kama kitengo hiki kingefanya kazi zake sawasawa na marekebisho yangefanyika mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitengo hiki pia kipewe jukumu la kufanya utafiti wa barabara zetu zote, madaraja yetu yote, makalavati yetu yote ili kuhakikisha kwamba kabla athari kubwa hazijajitokeza, ziweze kushughulikiwa mapema. Kwa sababu miundombinu mingi ya barabara imeanza kujengwa tangu mwanzoni mwa mwaka 2000, kwa hiyo, *lifespan* ya hizi barabara, madaraja na makalavati sehemu kubwa zimekwishapitwa na wakati. Hata hivyo, kwa kuwatumia wataalam wetu hawa wa *technical audit* wanaweza wakatuwekea mambo sawasawa na tukaweza kufanya *preventive maintenance* na hatimaye hizi barabara zikapitika kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa licha ya Waziri na Naibu Waziri kuwa wanatutembelea katika maeneo mengi hata kama Barabara yangu ya Tingi – Kipatimu Mheshimiwa Waziri hajaweza kufika, basi ajitahidi afike kila maeneo. kwa sababu Mawaziri hawana uwezo wa kufika kila eneo wawatume Maafisa Waandamizi waje wakague hizo barabara ili waone uhalisia. Unaweza ukakuta unapokea taarifa mezani, mwisho wa siku hali sivyo ilivyo huko ambako barabara zinajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja namba saba ambayo ningependa kuishauri Serikali ni ujenzi wa mifereji pembezoni mwa barabara. Barabara zetu nyingi hasa zile za vumbi na hata zile za lami baadhi hazina mifereji. Unakuta barabara imejengwa tu mifereji ya kupitisha maji hakuna, mvua zikinyesha zinapita katikati ya barabara na kuharibu barabara vibaya sana. Kama mvua za *El-Nino* zilivyo

mwaka huu, barabara zimegeuka kuwa mito na hatimaye zimekuwa na madhara kama haya ambayo nimeyasema. Kwa hiyo, naomba tuone namna ya kufanya ili ujenzi uweze kuimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia utafiti wa barabara zetu na namna ya ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane, muda wako umekwisha.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jioni tutakuwa na Mheshimiwa Tecla Ungele, tutaanza naye, watafuata Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Joseph Kamonga na Mheshimiwa King.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 10.00 Jioni.

*(Saa 6.58 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano yanaendela)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele ulishatajwa, jiandae Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia…

**NAIBU SPIKA:** Unaweza ukasogea mbele ukitaka kuchangia *comfortably.*

*(Hapa Mhe. Tecla M. Ungele alisogea kwenye kipaza sauti kilichokuwepo mbele yake)*

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili nami nichangie hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipatia zawadi hii ya uzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuleta ustawi na maendeleo ya jamii ya Watanzania.  Nampongeza pia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kazi kubwa ya kusimamia kazi za Serikali na pia kwa wasilisho zuri la bajeti na hotuba ya bajeti ya Wizara yake. Hotuba hiyo imesheheni mambo mengi ya sekta mbalimbali nchini zikiendelea kuleta maendeleo na kuchochea maendeleo. Pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zote zilizoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, wanafanya kazi nzuri kwa maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nauelekeza kwenye maeneo kadhaa. Hotuba ya Waziri Mkuu ina mambo mengi, lakini kutokana na muda, nitachangia maeneo machache tu. Kwanza, ni usafiri na usafirishaji. Tumeshuhudia miundombinu ikiboreshwa; barabara za mijini na vijijini na Watanzania wote ni mashahidi, lakini

miundombinu hiyo imeharibiwa na mvua kubwa ya *El-Nino*. Tumeshuhudia maeneo mengine mawasiliano yalikatika. Kwa mfano kule Liwale, Barabara ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale na Barabara ya Masasi - Nachingwea kwenda Liwale, Barabara ya kutoka Nanganga kwenda Ruangwa, zote zilikatika na maeneo hayo yalikuwa hayana mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ni muhimu sana katika ustawi wa jamii, kusafirisha mazao, kusafirisha watu na kadhalika na maendeleo yote tu yanategemea usafiri. Ombi langu, barabara hizi zijengwe kwa umakini mkubwa kweli na kwa kiwango cha lami; vile vile Masasi – Nachingwea – Liwale, Nangurukuru kwenda Liwale na Daraja lile la Nanganga ambayo inaunganisha Wilaya ya Masasi na kule Ruangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia madaraja yajengwe kwa uimara mkubwa. Maeneo tuliyokuwa tumetegemea yawekwe makalvati, ndiyo hayo mvua hizi kubwa zimefika zikayavunja yale makalvati na kuyazoa kabisa, sasa hivi kumebaki wazi kabisa. Kwa hiyo, yatengenezwe madaraja makubwa na imara ya kupitisha maji katika maeneo mapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nachangia liko Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Kuna *program* hii ya kukuza ujuzi kwa vijana, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, vijana wamepata nafasi kwenda kusoma vyuo hivyo, tumeenda kule Rwazari kule Tabora Manispaa na kule *St. Antony* Manispaa ya Musoma na kwingineko, wanapata ujuzi wa ushonaji, useremala na mambo ya umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, kwanza idadi ya vijana iongezeke na ichukue maeneo mengi ya Tanzania, kwa sababu maeneo mengi yana vijana ambao hawana ujuzi, lakini pia kuna vijana ambao wako kwenye makundi maalum, nao wanahitaji ujuzi, kwani nao wana umuhimu na wana vipaji vikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu lingine, vijana hawa wapatiwe vifaa vya kufanyia kazi wakishamaliza masomo.

Tunawafundisha ujuzi pale, wanapata ujuzi vizuri sana na wenyewe wanafurahi sana, tumewaona tulipokuwa tumeenda wakati wa ziara za Kamati. Wanafurahi sana kupata ile nafasi na wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iweke bajeti maalum ya kununua vifaa ili vijana wale wakishatoka kwenye mafunzo, wakisharudi majumbani kwao, basi kuwepo na mwendelezo wa kazi zile, wakajiajiri wenyewe na wakaendelee kufanya kazi ya kujipatia riziki, badala ya kutoka pale na ujuzi wao ambao hautakuwa na maana, kwa sababu wengine hawana uwezo wa kumudu kununua vifaa vya kufanyia shughuli zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ishengoma, wajiandae Mheshimiwa Kamonga na Mheshimiwa King.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipatia nafasi ya kuchangia jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Reli ya Kati kujengwa kwa viwango vya kimataifa. Nachukua nafasi hii kumpongeza Rais kwa jinsi alivyoendeleza ujenzi huu mpaka sasa hivi umefikia hatua ambayo tayari imeshaanzishwa ambapo wananchi wa Morogoro waliona jaribio la mwendokasi lilifanyika na wananchi wa Pwani. Kwa sasa hivi kwa upande wa Morogoro mpaka Dar es Salaam ni kilomita 300, ni asilimia 98.84 na Morogoro - Makutopora ni asilimia 96. Kwa hiyo, ni jambo zuri ambalo wananchi tunajivunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu na ushauri ni kuwa, tuendelee kuhimiza wananchi, reli hii ikikamilika waweze kuitumia vyema, kwa sababu reli hii ni utalii, ni uchukuzi na inaongeza uchumi wa wananchi. Kwa mfano, kwenye vituo vyetu vya treni hii ya mwendokasi kwa mfano Morogoro tukiwa na Ngerengere, Morogoro Mjini na Kilosa, wananchi wote na vituo vingine vya Dodoma na

kuendelea mpaka Mwanza na Kigoma waweze kuhamasika kujitayarisha kuwa na biashara kusudi wananchi waweze kukuza uchumi wao pamoja na ajira, hasa upande wa wanawake pamoja na watoto wakiwemo wanawake wa Mkoa wa Morogoro waweze kujitahidi kuona ni jambo muhimu sana la kujivunia reli hii ya mwendokasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere, ambalo tunajivunia sana Tanzania kuwa nalo, litafua umeme ambao unatosheleza kutumika katika Nchi yetu ya Tanzania pamoja na kuwauzia nchi jirani. Ombi langu, umeme huu ambao tayari tumeshaushuhudia na wananchi wa Morogoro na Pwani Rufiji wameshuhudia kuwa mtambo Na.1 tayari umewashwa, pamoja na vyanzo vingine vya umeme, kwa hiyo, wakati utakapozalishwa kwa wingi, kaya zote waweze kupata umeme wa kutosha kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Kiwanda cha Sukari Mkulazi. Kiwanda hiki tumekitembelea, kinaendelea vizuri katika hatua zake za ujenzi kwa asilimia 96 kama ilivyosema hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Vile vile kimetoa ajira kwa wananchi na sana sana ni vijana. Kuna vijana wengi, lakini tulipoongea nao, naona Serikali ifuatilie kuangalia maslahi yao yanakuwaje nak ama yanaendana na kazi wanayoifanya kusudi waweze kuendelea na uzalishaji wa sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo naunganisha na shamba la Mkulazi Na.2 ambalo lipo Dakawa hapo hapo karibu na kiwanda cha sukari ambacho kinazalisha hiyo miwa inayochakatwa kwenye kiwanda hicho cha sukari. Ni kweli tulikuwa na tatizo la sukari kwa sababu ya mvua ya *El-Nino,* maji yalijaa kwenye miwa kiasi watu walishindwa kuvuna miwa, lakini sasa hivi tunategemea kuwa hicho kiwanda kitaweza kuzalisha tani 50,000 kwa mwaka ambayo itaweza kupunguza tatizo la sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kuwa, mashamba ya uzalishaji sukari miwa yaweze kuendelea kuangaliwa ikiwepo Kagera, Kilombero *I* na Kilombero *II,* kikiwepo Kiwanda cha Kilimanjaro na viwanda vingine mashamba yaweze kuanzishwa kusudi sukari iweze kuzalishwa kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine ni kwenye upande wa mahindi. Huwa tunaanzisha maghala ya Serikali ambayo huhifadhi mahindi ili wakati wa njaa tuyatumie. Kwa hiyo, huu mpango unaweza ukatumika kwa upande wa sukari, tukaweza kuwa na maghala ya sukari ambayo yanaweza kutumika wakati tuna uhaba wa sukari. Hilo ni jambo muhimu ambalo naomba liangaliwe pamoja na ajira kwa watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba kuongelea ni nishati. Nashukuru umeme umeenea kwa wastani wa vijiji vyote, umeme wa *REA* unaendelea, lakini nahimiza na naishauri Serikali kuwa wananchi wanaomba vitongoji vyote viweze kupata umeme. Umeme ni viwanda, umeme ukimulika na wewe mwenyewe unafurahi. Vile vile umeme ni elimu, kwa sababu wanafunzi watatumia umeme kujisomea na kujifunza. Kwa hiyo, naomba sana jambo hilo la umeme liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa kutoa nishati safi ya kupikia ambapo kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati wameweza kutoa kongamano la wanawake na kuwapatia vitendea kazi wanawake wajasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, wadau wote wenye uwezo, wamuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa kusambaza mitungi kusudi tuweze kutokana na matumizi ya kuni ambazo zina madhara ya kiafya, zinaharibu mazingira na kuongeza athari za tabia nchi. Kwa hiyo, nawaomba sana wadau wote waweze kuliangalia hilo jambo la nishati safi. Pamoja na hayo, nishati mbadala ikiwepo *biogas,* upepo viweze kutumika kwa sababu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni elimu. Elimu ni jambo muhimu sana. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita amefanya kazi nzuri sana kwa upande wa elimu, ila ushauri wangu, bado kuna wanafunzi wengi ambao wamemaliza shule, wana sifa za kwenda vyuo vikuu, lakini hawana mikopo licha ya mikopo kupandishwa juu. Kwa hiyo, naomba bajeti iweze kuongezwa zaidi ili kuwasaidia

wanafunzi wanaostahili kwenda vyuo vikuu ili kila mmoja aweze kutimiza ndoto zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa madarasa makongwe ya sekondari pamoja na msingi ikiwepo shule zetu za huko mikoani kwenye halmashauri, naomba sana uangaliwe. Nimetembelea, kweli nimeona madarasa mengine ukiacha hii ya UVIKO ambayo tumeweza kukarabati na ambayo tumeweza kujenga ya sekondari pamoja na *primary,* lakini mengine pembeni unakuta bado ni machakavu. Kwa hiyo, naomba yaangaliwe kusudi yaweze kukarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, amefanya jambo kubwa sana, lakini bado kuna matatizo ya nyumba nyingine kama nilivyosema juzi, nyumba ya akina mama na watoto bado hazijamalizika, ziweze kumalizika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Dkt. Ishengoma nafikiri…

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga, Mheshimiwa King jiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambazo zinaendelea na kule Jimboni kwangu Ludewa wananchi wanazishuhudia zinaonekana kwa macho. Ila leo naomba nijikite zaidi kwenye maeneo ya miundombinu ya barabara Jimboni kwangu Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, nianze kwa kutoa pole nyingi sana kwa wananchi wa Kijiji cha Liugayi kilichopo Kata ya Luilo, Kijiji cha Lifuma na Kitongoji cha Liumba kwa mafuriko makubwa ambayo wazee wenye umri mkubwa wanasema mara ya mwisho yalionekana mwaka 1963/1964. Mto Ketewaka kutokana na mvua nyingi ambazo zilinyesha upande wa Ruvuma kwa maana ya Mbinga na upande wa Ludewa na Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Ketewaka ambao unaenda kuungana na Mto Ruhuhu ulifurika sana na kuweza kuathiri wananchi wa Kijiji cha Liugayi kama nilivyoeleza ambapo nyumba zao zimebomoka, mazao yao yamesombwa na maji, kwa hiyo, hawana chakula, hali kadhalika, mifugo yao imesombwa na maji. Kwa hiyo, kuna wananchi kama wa kaya 20 wanaishi kwenye Kanisa hivi sasa. Hali kadhalika, Kijiji cha Kiyogo, Kijiji cha Kipingu, Ngerenge na baadhi ya mashamba ya wananchi wa kandokando ya Mto Mchuchuma, Kijiji cha Igalu na Kijiji cha Mbongo. Kwa hiyo, nitoe pole nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa huko, nilikwenda kuwafariji wananchi, kimsingi naomba Serikali iweze kutoa msaada wa haraka. Hatuwezi kumkufuru Mwenyezi Mungu kwa kuleta mvua nyingi kwa sababu mvua tunaihitaji, tunaiombea wakati wote tuweze kuipata na kule Ludewa imetusaidia, mwaka huu tuna mahindi mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Kilimo aanze kututafutia masoko, ni mvua hiyo hiyo ndio imewezesha kutokana na Mheshimiwa Rais kuleta ruzuku ya mbolea, wananchi wamelima zaidi na mazao wamepata zaidi, lakini mvua kutokana na kuzidi imesababisha maafa kama ambavyo nimesema. Kwa hiyo nitoe pole nyingi kwa wananchi na niwasihi waendelee kuwa na subira kwa sababu Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na wasaidizi wake wanaendelea kuliratibu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu ya barabara, natambua kwamba Wizara hii inashughulika na mambo mengi ya wananchi na jana nimetoka Ludewa, wananchi wanatarajia kusikia nikisemea changamoto mbalimbali ambazo zinazikabili barabara mbalimbali za Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na barabara ambazo ziko chini ya *TANROADS*, niishukuru Serikali awamu ya kwanza ilitoa shilingi bilioni 179 kwa ajili ya kutujengea barabara kwa kiwango cha zege, kilometa 50 kutoka Lusitu hadi Mawengi. Barabara imekamilika na inatumika vizuri na ni barabara bora sana kutokana na kiwango kile cha zege. Changamoto ni kuwa, jiografia yetu ina milima mikali sana kwa hiyo kifusi kimekuwa kikiporomoka, milima inaporomoka inafunga barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi mimi mwenyewe nimepata vikwazo sehemu mbili, kwenye hii Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda, pale Mlima Kimelembe kuna kazi inaendelea ya kukata mlima mita 20 ambao ulikuwa unagharimu maisha ya watu na mali zao, Serikali ilitoa fedha bilioni tano kwa ajili ya kuukata mlima. Sasa bahati mbaya mvua ziliwahi kufika kabla mkandarasi hajafika mwisho wa kazi, lakini nadhani hata ule upana wa barabara nao ulikuwa mdogo, kwa sababu ule udongo ni udongo ambao uko kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo mvua inaponyesha unayeyuka kama biskuti unaporomoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Manda kuwafariji wale wananchi wa Bonde la Ruhuhu nilikuwa siwezi kupita Ruvuma kwa sababu Mto Ruhuhu ulifurika. Kuna Mto Kipingu nao ulijaa maji, gari haiwezi kupita na kwa upande wa Nyasa maji yalikuwa yamejaa, hakuna gari linapita, lakini Mlima Kimelembe ulikuwa umeporomoka umefunga barabara. Kwa hiyo ningeugua kule, nisingeweza kufikishwa hata hospitali ya wilaya labda ningepewa milungulungu na wale wananchi ambazo ni tiba mbadala ambazo wao wamekuwa wakitumia muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba tukio hili lilinikuta mimi, sasa wananchi wanakuwa katika hali gani pale ambao barabara zinafunga, wanakuwa hawawezi kupelekwa sehemu yoyote. Kwa hiyo naomba juhudi za haraka sana na za makusudi ziweze kufanywa na Serikali kuongeza wataalam ili kwenda kutathmini na kuweza kuona ni namna gani tunaweza tukapata suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mlima Kimelembe kwa bahati mbaya sana uligharimu maisha ya kijana mmoja wa bodaboda ambaye hata miaka 30 hajafikisha. Kifusi kilishuka na kwa bahati mbaya alikuwa pale, akafunikwa akafariki. Tunaiombea roho yake ipumzike kwa amani huko aliko. Kwa hiyo naomba sasa Serikali iweze kutuma wataalam waungane na wale wa *TANROADS* waliopo Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Meneja wa *TANROADS* pale Njombe, ni msikivu na mwepesi sana, ukimpigia simu yuko tayari kuacha shughuli zake kwenda kusaidia. Siku ile nimefungiwa nilimpigia simu, alitoka mwenyewe na wataalam wakaenda kufungua barabara. Sasa kwa bahati mbaya sana ilifunga maeneo mawili na huku kwenye hii ya Lusitu - Mawengi na yenyewe ilikuwa imefunga hata kupeleka mitambo ilikuwa haiwezekani. Kwa hiyo zinahitajika juhudi za makusudi na za haraka sana ziweze kuchukuliwa ili kuondoa vikwazo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kuna barabara nyingine ambayo ni ya *TANROADS* ambayo inaitwa Mkiu - Liganga kwenda Madaba, barabara hii ndio inayoenda kwenye Mgodi wa Liganga, ambako kuna utajiri mkubwa, tani milioni 126 za chuma ambazo ndani yake ina *titanium* na *vanadium*. Madini ambayo yana thamani zaidi ya mara 20 ya chuma chenyewe. Kwa hiyo ni barabara muhimu na ni barabara ya kiuchumi na inaunganisha na Mkoa wa Ruvuma kwa jirani yangu Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama. Sasa pale kuna lile eneo la Ndolela na kwenyewe kuna daraja pale limeondolewa na maji. Kwa hiyo, naomba sana, tunashirikiana vizuri na Mheshimiwa Mhagama kufuatilia kwa sababu wananchi wangu nayo ni *alternative route* na hilo eneo la Ndolela lina mashamba makubwa ya kiuchumi ambayo nayo ni barabara ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ule mpango wa kuijenga Barabara hii ya Mkiu – Liganga - Madaba ungeanza haraka, kwa sababu Mheshimiwa Rais anavyozungumzia uwekezaji wa Mchuchuma na Liganga amechoka kusikia ngonjera hizi za muda mrefu. Hii inatakiwa iwe *reflected* kwenye barabara. Namwona

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi anaandika, namshukuru sana Mheshimiwa kwa usikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Rais anavyozungumzia barabara ya kiuchumi, ya kimkakati, ya uwekezaji, haya yawe *reflected* kule kwenye barabara hata wananchi wakiona ujenzi umeanza kwa kiwango cha lami watajua ni yale ambayo Mheshimiwa Rais anayazungumza. Kwa hiyo niombe sana Serikali iweze kuchukua hatua za haraka kwa sababu hata kutoka Mkiu kwenda Lugarao mwaka huu wananchi wamehangaika sana. Kuna daraja pale, unapotoka Lugarao kwenda Shaurimoyo kwenye Chuo cha *VETA* napo pana hali ngumu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya yote hayo, nimpongeze sana yule Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Njombe yule mama, kwa kweli anafanya kazi nzuri, anajituma sana. Namwomba Waziri wa Ujenzi wasituhamishie labda kama watampandisha cheo, hilo sitakuwa na uwezo wa kuzuia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara vilevile inaanzia Mlangali – Lupanga kwenda Ikonda, Ikonda ni hospitali kubwa sana ambapo wananchi wengi wanategemea kwa ajili ya matibabu. Namshukuru Mheshimiwa Bashungwa, mwezi uliopita alikuja Ludewa, alifanya mkutano mkubwa pale Mlangali na alitoa ahadi nzuri sana kuhusu hii barabara. Kwa hiyo naomba nisiizungumzie sana ila tu ule mpango wa kuendeleza *lot three* kutoka pale Mawengi mpaka Nkomang'ombe. Naomba sana Serikali iendelee na iweze kujengwa kwa kiwango cha zege kwa sababu sasa hivi malori ya makaa ya mawe zaidi ya 40 yanakwama mle barabarani. Ukiwauliza kwa nini msisubiri mvua ziishe ndio mje? Wanasema haiwezekani Wakurugenzi wa Makampuni wamekuja wana *order* kubwa nzuri zenye faida, kwa hiyo malori lazima yaendelee kwenda. Kwa hiyo ni ishara kwamba tusipojenga kipande hiki kilometa 68 kutoka Mawengi mpaka Nkomang'ombe, tunafunga uchumi wa nchi na tunazuia pato la Taifa kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Ruvuma walipoanza kuchimba makaa ya mawe waka-*shoot* kwenye makusanyo ya *TRA* kutoka kusikojulikana mpaka kuwa namba tatu, kwa hiyo kuna uchumi, kuna kodi nyingi pale. Barabara kama hizi ambazo zinakuza pato la Taifa, zinaleta uchumi, zingepewa kipaumbele kwa sababu zinaweza kuongeza fedha ambazo zitakwenda kujenga barabara maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ambazo ziko chini za *TARURA*, Kata ya Ibumi nayo iko kisiwani, mwananchi akiugua pale hawezi kupelekwa hospitali ya wilaya, hawezi kupelekwa popote kwa sababu vifusi vimedondoka na vimefunga barabara. Daraja la Mto Ketewaka na lenyewe limekuwa changamoto. Halikadhalika kuna barabara hii inayoanzia Kigasi inakwenda Milo - Ludende mpaka Amani inaunganisha kata nne na barabara nyingine inayokwenda Madilu eneo la…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga pole na msiba, muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa King, wajiandae Mheshimiwa Chaurembo na Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu na nikushukuru kwa kupata hii nafasi ili niweze kuongea mambo ya kitaifa ambayo yanahusiana na asilimia 38 ya Watanzania ambao ni milioni 23 ya *population* yetu ya milioni 61 ambao ni *labor force* ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka niongelee kitu kimoja, kuna msemo wa Kiswahili unasema kwamba; chanda chema huvishwa pete, kabla sijaenda huko. Nazipongeza taasisi za *NSSF,*

*PSSSF, WCF, OSHA, CMA* na taasisi zote ambazo ziko chini ya Wizara hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme na msemo mwingine; ada ya mja hunena, muungwana ni vitendo. Muungwana ukinena unatakiwa utende. Katika Mpango wetu wa Taifa umezungumzia kwamba utazidi kuhamasisha kukuza ajira na ujuzi, hii iko katika *paragraph* ya mwanzo katika mpango mpya. Pia kuna makubaliano ya *Association of Tanzania Employers (ATE),* waajiri wa Tanzania walikubaliana na Serikali kwamba zikusanywe *skills development levy* na *one third* ipelekwe kama ni *investment* katika kukuza ujuzi kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *agenda* yangu ni moja tu, ni Mradi Na. 6581 ambayo ni Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi. Hii programu walikubaliana, Serikali na Waajiri kwamba, itatoka *one third* ya *skills development levy* ili kutazama *gap of skills* ambayo inakosekana katika viwanda vyetu, katika maeneo yetu ya kazi na ndio maana hawa wamechangia, badala yake sasa muungwana amenena lakini hajatenda kwa sababu mpaka sasa hivi hiki kitu bado hakijafanyika na tumezoea kupeleka shilingi bilioni tisa katika bilioni 300 zinazokusanywa za *skill development levy.* Tunapata *gap of skills* kwa sababu hatufuati haya makubaliano yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nazungumzia *investment* katika ujuzi, *investment* katika ujuzi kwa Tanzania, mwaka jana kwa Watanzania milioni 61 tuliwekeza bilioni tisa. Mwaka huu tumeshuka tumewekeza bilioni 7.8 katika nchi ambayo sasa tunakwenda katika kipato cha kati, nchi ambayo ukiitazama tuko nyuma kiujuzi, halafu katika mipango yetu tunasema kwamba hiki ni kipaumbele. Naomba tutende yale tunayoyasema. Kipaumbele hiki kweli katika hawa vijana milioni 23 tunaweza tukakuza ujuzi kwa bilioni saba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mpango Mkuu wa Miaka Mitano umezungumzia kwamba tutakuza ujuzi kwa vijana 681,000. Hapa ina maana kwamba kila mwaka tungekuza ujuzi kwa vijana 136,200, lakini kwa bahati mbaya msimu uliopita tulikwenda na vijana 10,000 tu ambao ni sawasawa na asilimia saba ya hii 136,000 ya

mwaka. Mwaka huu *plan* yetu kukuza ujuzi kwa ajili ya kupata ajira kwa vijana 12,280, ni sawasawa na asilimia tisa ya mwaka. Kwa maana hiyo hii asilimia tisa ndio itakayokwenda kukuza ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye *paragraph* ya 163 na 164 ya hotuba yake ukurasa wa 81 na 82 alielezea kwamba tutatengeneza fursa za ajira 470,257, lakini Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi imetaka tutengeneze fursa za ajira 8,000,000 na hii itakuwa ni sawasawa na asilimia 29 kwa mwaka. Milioni nane kwa mwaka maana yake ni sawasawa na kupata fursa za ajira 1,600,000, badala yake tunapata 470,000, ina maana hapo bado tunaenda kuanguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe uwekezaji katika *program* hii ni mdogo tena ni mdogo mno, ni sawasawa na kusema kwamba hakuna kitu. Waarabu wana kitu wanasema kwamba kuna kitu kinaitwa *Mudahala*, *Mudahala* ni kumpaka mtu mafuta kwa mgongo wa chupa. Maana yake anaona anapakwa mafuta, lakini kumbe mafuta yako ndani ya chupa, kwa maana hiyo tunakuwa tunamdanganya na kwa kuwa tunajidanganya wenyewe ni sawasawa na kujitekenya halafu tunacheka. Sasa hapa hatufikii malengo ambayo tumeyaweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo *statistics* hapa, nchi yetu ina watu milioni 61, *labor force* yetu ni milioni 23, lakini pia *skilled labor* ni asilimia 3.6 peke yake, lakini inatakiwa tufikie asilimia 12. Ni sawasawa tunafikia *labor force* ya watu 828,000 ambao ndio waliosoma katika milioni 61, ndio *skilled labor*, hapa tuko chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija ukatazama katika hotuba ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu amesisitiza kwamba itolewe *one third* kama tulivyokubaliana na tusipofanya hivyo ina maana kwamba hii *program* inaweza ikafanyika lakini isilete tija. Tumebaini katika ziara yetu ya Kamati watu wanasomeshwa lakini inakuwa kama anakwenda na kurudi shule, hana kifaa chochote, anarudi mtaani anasahau kila kitu. Ina maana bado elimu hiyo ya ufundi huo tunayowapa inakuwa haileti tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati pia umesema kwamba, ni lazima ipelekwe hii, lakini kuna Sheria ya Mafunzo Mheshimiwa Mwigulu alikuja nayo hapa kwenye *Finance Act* katika *Finance Bill,* alikubali kuweka *one third* kama iwe *ring fenced,* lakini tunashangaa mwisho Serikali haikupitisha. Hapa ninayo *Hansard* ya tarehe 26 Juni, Mheshimiwa Mwigulu alisema hili jambo litaletwa mwaka huu kwa sababu mwaka jana halikuweza kufanikishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuzungumza hivi hivi isipokuwa bora labda tujilinganishe na wenzetu ambao na wao wako katika hizi nchi za Afrika, wao wanawekeza vipi na wamefanikiwa vipi? Tutazame Botswana, Botswana imewekeza dola milioni 11.35 ambayo inakuwa ni sawasawa inakaribia kwenye shilingi kama bilioni 25 za Tanzania, lakini Mauritius imewekeza karibu ya bilioni 70. Sisi Tanzania tunawekeza shilingi bilioni 9.0, Mauritius *population* yao ni 1,301,636, lakini vijana ambao ni *labor force,* ni sawasawa na watu 532,000, sisi ukitutazama tuko wengi milioni 23 tunawekeza fedha kidogo kuliko ya wao. Botswana *labor force* yao ni 1,145,000 lakini fedha walizowekeza ni nyingi kuliko sisi na ukitazama *population* yao ni ndogo kuliko sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda tutazame katika *skilled labor* au *labor force* ambao ipo. Wenzetu, watu ambao wamekuwa *employed* ni 400,000 katika *labor force* ya 500,000, vijana 400,000 wamekuwa *employed*, vijana 100,000 ndio wako nje ya ajira, lakini bado wamewekeza vizuri. Hiyo ni *Mauritius*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija Botswana katika 970,000 waliokuwa wamekuwa *employed* ni 732,000 na 232,000 pekee ndio ambao wamekuwa *unskilled*. Hii inatokana na maamuzi ya makusudi na utashi wa kisiasa. Sisi tuna vijana wengi lakini hatutaki kuheshimu makubaliano. Sasa tatizo linakuja wapi? Tatizo linakuja kwamba bado hatujakubali kubadilika na kama hatutakubali kubadilika ina maana kwamba hatutoweza kufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huu ni wakati wa kufanya mageuzi katika kutazama ufundi unaohitajika katika soko. Hawa

*employers* wanatoa hizi fedha ili tuangalie *required force* inayotakiwa pale. Kwa hiyo zile *skills* zinazotakiwa na hawa waajiri ni lazima sisi tuweze kuzi-*produce* lakini hatuwezi kutoa zile *skills* kwa sababu tunaangalia vitu vingine. Hizi fedha zimekosa *clarity,* hazina uwazi na uwazi wenyewe kwamba hatujui kiasi gani kimekadiriwa kwenda kule, sisi tunasema iende *one third* kwa makubaliano, lakini inakwenda bilioni tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwigulu alituahidi kwamba atafanya liwezekanalo ili aweze kukidhi haja ya kupeleka hizi fedha kule ili ziwe nyingi, lakini mpaka leo hatujaona *mid-year review*. Kwenye hii *mid-year review* ingeonesha kwamba kuna fedha zimekwenda kwa ajili ya ku-*train* watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanachangiwa kutokana na…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa King, ahsante.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** …msimamo katika kutazama vijana. Naweza nikasema neno moja ambalo niliwahi kulisema…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa King muda wako umekwisha.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** …Mungu anasema; *famaa amalali Mussa ila dhuriya,* waliomuamini Musa ndio maana akashinda walikuwa ni vijana, lakini sisi vijana tunawatelekeza, hatutaki kufanya kama Musa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba na jiandae Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja kwa sababu hotuba hii ya bajeti imekidhi mambo mengi ambayo tumekuwa tukiyatarajia Wabunge katika majimbo yetu, lakini imeonesha namna gani ya mambo yaliyotekelezwa katika sekta ya afya, elimu, barabara, maji na umeme, kwa hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa kuweza kuyafanya yote haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo yapo mambo machache ambayo yanahitaji marekebisho ya haraka ili tuweze kusonga mbele. Mara kadhaa toka tuanze Bunge hili nimekuwa nikipigia kelele suala la wananchi wa Rangitatu mpaka Kongowe kulipwa fidia zao, ni mwaka wa saba sasa wananchi wale wametathminiwa. Kama unavyojua sisi wananchi wa Dar es Salaam nyumba zetu ndiyo biashara zetu, ndiyo sehemu zinazotupatia riziki. Kwa hiyo nyumba sasa zimekuwa hazipangishiki na haziuziki, tumeendelea kupata ugumu wa maisha kutokana na kutokulipwa fidia zaidi ya miaka saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile sehemu inayotaka kulipwa fidia ni kwa ajili ya kujengwa barabara ile ambayo inatoka Rangitatu kwenda Kongowe. Wote mtakuwa mashahidi bahati nzuri Waziri Mkuu naye ndiyo njia yake ya kuingilia Dar es Salaam, barabara ile imekuwa na msongamano mkubwa kila mwaka tunaizungumzia. Nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri leo amenijibu kwamba barabara imepata kibali cha kutangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hoja yangu ya msingi tunatangaza barabara kujengwa, je, hawa watu ambao tumewaweka muda mrefu bila ya kulipwa fidia tunawafanyaje. Naomba sana Serikali itupe majibu lini watu hawa watalipwa fidia na lini barabara hii itaanza kujengwa ili tuondoe sintofahamu ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara katika barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nataka kuliongelea ni suala zima la alama za X nyekundu zinazowekwa katika maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Dar es Salaam. Katika Jimbo

langu Barabara yote inayotoka Rangitatu - Charambe kwenda mpaka Maji Matitu – Chamanzi mpaka Msongola kupitia Mbande pande zote mbili imewekewa X, sasa tunajiuliza hawa wenzetu wa *TANROADS* wanaweka X kwa sababu gani. Bahati nzuri sisi wengine tumezaliwa Dar es Salaam, maeneo tunayokaa ndiyo tuliyozaliwa. Tunafahamu historia ya maeneo yale, maeneo yale yalikuwa ni Vijiji vya Ujamaa ambapo wazawa wa pale walitoa ardhi zile kwa ajili ya kuwapa makazi ndugu zao waliokuja katika maeneo yale lakini kwa masharti watakapokata mti basi mti ule ulipwe fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kijiji kile kukua Serikali tunaishukuru iliamua kututengenezea barabara na mwaka 1994 Serikali kupitia Kampuni ya *ADUCO* iliamua kuboresha barabara ile, barabara ile ilijengwa kwa upana wa mita saba na nusu kwa pande zote mbili kwa maana ya mita 15. Wakati inajengwa miti ya wazee wetu ililipwa fidia na ikapisha ujenzi wa barabara ile mpaka sasa tunapita kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007 Sheria ya Barabara Namba 13 ilitungwa. Katika sheria ile inaelezea barabara itakuwa na mita 27.5 pande zote za barabara kutoka katikati ya barabara, hoja yetu tunayojiuliza, unatuwekea X je, barabara ile ilipandishwa hadhi mwaka gani na ilipandishwa hadhi kwa *GN* namba ngapi? Ili tuone kama kweli X zile zinazowekwa zinaendana na ile sheria ya mwaka 2007 iliyotungwa Sheria Namba 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sheria ile wakati inatungwa hakuna aliyelipwa fidia na kama wapo waliolipwa fidia basi tuwaombe wenzetu wa *TANROADS* watuletee orodha ya watu waliolipwa fidia ili tupishe eneo lile kwa amani. Tumekuwa tukiwaomba mara kwa mara, lakini wameshindwa kufanya hivyo hatimaye Serikali kupitia Mkuu wa Mkoa imesitisha zoezi lile la kubomoa, zoezi lile tunasema limesitishwa kwa mdomo, tunaomba tupewe maandishi kwamba zoezi hili limesitishwa kwa sababu moja, mbili na tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi tunayo maswali ya kujiuliza, moja, tunataka tujue *GN* namba ngapi na ya mwaka gani iliipandisha

hadhi barabara ile ili tuweze kujua sasa kama sisi tuliokuwepo tulikuwepo kimakosa au tuko sawasawa. Jambo la pili ni wananchi wangapi walilipwa fidia baada ya *GN* ile kutoka, lakini jambo la tatu kwa nini Wizara ya Ardhi imetoa hati miliki katika maeneo yale pande zote mbili za barabara? Wananchi siyo tu wanamiliki leseni za makazi wanamiliki kwa hati miliki, tunaomba tupewe majibu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunataka tujue ni vigezo gani ambavyo *TANROADS* walitumia kulipa fidia watu waliokuwa barabarani wakati wanajenga stendi ya mwendokasi na hawa waliopo sasa hivi watakiwe kubomolewa bila kulipwa fidia. Mambo haya yameleta taharuki kubwa sana kwa wananchi kwa sababu ni zaidi ya kaya 100,000 zinaenda kuathirika katika barabara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua Jimbo la Mbagala na Jimbo la ndugu yangu Jerry ndiyo yanaongoza kwa *population* kubwa hapa nchini, kwa hiyo mjue kitendo kilichofanywa na *TANROADS* kimeenda ku-*disturb* siasa za Dar es Salaam. Naomba sasa Serikali ije na kauli ambayo itawatoa hofu wananchi wa Mbagala Rangitatu, Charambe, Chamazi na Msongola.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nizungumzie suala la miundombinu ya barabara. Tunafahamu mvua zimenyesha na barabara zimeharibika kwa kweli katika Jimbo zima la Mbagala kama siyo Mkoa wote wa Dar es Salaam barabara zimeharibika sana, tunawaomba sana *TANROADS* na *TARURA* waje warekebishe barabara zile ili ziweze kupitika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho tunazo mamlaka au taasisi mbili zinazojenga barabara hapa nchini. Tunao *TANROADS* na *TARURA,* ushirikiano wao hauko sawasawa kwa sababu wakati fulani *TANROADS* wanajenga barabara na wanaweka mifereji lakini maji wanaelekeza katika makazi ya watu na wanasema wananchi suala la maji yale kuyapeleka mtoni ni suala la *TARURA,* je wali-*check* bajeti za *TARURA* wakalinganisha na bajeti zao ili kuona barabara ile itajengwa na *TARURA* watapokea yale maji kuyapeleka mtoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba sana watendaji wetu wa Serikali pale wanapotaka kufanya maamuzi ambayo yatawagusa wananchi moja kwa moja hasa suala la bomoa bomoa waangalie historia ya maeneo yale, sisi tunawafahamu, ukiangalia *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam wote wanaofanya kazi sasa hivi ni watu ambao wamekuja miaka ya 2000, wangeuliza historia kwa wenzao waliokuwepo nyuma wangepata hadhi ya barabara ile ilikuwaje ili sasa wakurupuke na mipango yao ya kuweka X.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo, naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Benki ya *NMB* imeandaa iftar maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge. Iftar hii itafanyika katika viwanja vya Bunge kesho siku ya Alhamisi tarehe 4 kuanzia saa 12.30. Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote mnaalikwa katika iftar hiyo.

Mheshimiwa Ndaisaba, jiandae Mheshimiwa Salome.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni Rais ambaye amejipambanua vizuri kwa Watanzania na ameonesha kiu ya kutibu matatizo ya Watanzania, mahali popote unapokwenda unapotaja mama kabla hujaendelea Watanzania wanamalizia vichwani Samia, ni kwa namna ambavyo Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonesha nia, uthubutu na ari kubwa ya kutatua matatizo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Watanzania wanampenda Mama Samia na Watanzania wa Ngara wanampenda sana Mama Samia kwa sababu Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha mapenzi makubwa kwa Watanzania hasa kupitia miradi

mikubwa ya maendeleo anayoisukuma kwenye Jimbo la Ngara na maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda kwenye mchango wangu halisi, nisiruke bila kumpongeza sana Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa pamoja na Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wengine wote na Naibu Mawaziri waliopo kwenye hii ofisi ya Waziri Mkuu. Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na hao wengine sijawataja Jenista Mhagama naye yuko mle mle na wengine hakika ni miongoni mwa viongozi ambao nchi hii wametafsiri vizuri matakwa na maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Watanzania, sasa viongozi hawa wakiongozwa na Mheshimiwa Majaliwa wanatekeleza vizuri Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na wanasimamia vizuri shughuli za Serikali. Hakika tunawapongeza sana, chukueni maua yenu *live* hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nielekeze mchango wangu kwanza kabisa kwenye eneo la kuwezesha wanafunzi wa elimu ya juu hapa nchini. Dhamira ya *HESLB* ilikuwa ni kuhakikisha Watanzania wengi wanaweza kusoma elimu ya vyuo vikuu na elimu ya vyuo vya kati, tunaipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeifanya ya kuhakikisha inatoa mikopo pamoja na kuongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu, lakini kuna kundi la Watanzania kama ambavyo ipo kwenye *school dropout* kwa maana ya ngazi za chini hivyo hivyo na vyuo vikuu sasa hivi kuna *university dropout*. Nataka nikwambie Mheshimiwa Naibu Spika na Bunge lako hivi tunavyozungumza Wabunge wengi wanafuatwa na wazazi pamoja na wanafunzi waliotoka vyuo vikuu wakienda kuombwa wasaidie kusomesha watu walioko vyuo vikuu, ukiuliza unaambiwa mtoto alikosa mkopo. Baada ya kukosa mkopo kuna wazazi wanaouza mifugo, mwenye ng'ombe anauza, mwenye kuezua nyumba anaezua na wenye kuuza viwanja wanauza. Kwa bahati mbaya wazazi wengi hawatoboi miaka mitatu au miaka minne, wengi wanaishia katikati. Matokeo yake unakuta mwananchi wa kijijini ameuza mali yake lakini watoto hawajamaliza vyuo vikuu, wanarudi nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba kwa dhati ya moyo wangu kabisa, Serikali wafanye uchunguzi wa haraka wawabaini wanafunzi ambao wame-*drop* vyuo vikuu, waende *HESLB* wawape mikopo hao watu ili warudi vyuo vikuu wamalizie. Lipo kundi kubwa mpaka jana mimi nyumbani kwangu wamekuja wazazi zaidi ya sita, wote watoto wameshindwa kumalizia vyuo vikuu kwa sababu wamekosa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kero kubwa kwa Wabunge wengi kwa sababu wazazi wale wanahisi sisi Wabunge tuna mifuko tunaweza tukachukua fedha za kuweza kuwasaidia watoto wakamaliza vyuo vikuu. Sasa kundi hili naomba litafutwe, lihudumiwe kwa kuwa linajulikana. Mtu anaandika barua kwamba naacha kuendelea na chuo kwa sababu amekosa ada, anarudi nyumbani anakaa mwaka mzima, vyuo vikuu wanazo taarifa, Serikali ifanye mawasiliano, wachukue takwimu za hawa Watanzania, wasaidieni wapate mikopo waende wakamalizie vyuo vikuu. Naomba hili jambo mlipe kipaumbele kwa sababu watu wanalalamika na kuna kundi huko limeachwa. Naomba Watanzania hawa waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili kwa sababu hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu inakuwa na mawanda mapana, naomba niongelee eneo la miundombinu hasa upande wa miundombinu ya barabara. Sisi ni miongoni mwa Watanzania ambao wamewahi kupewa ahadi sugu ya muda mrefu ya kujengwa kwa barabara kwa kiwango cha lami. Naibu Waziri hapa anaifahamu, ameshakwenda mpaka akawaahidi wananchi wa Rulenge. Hii ni Barabara ya kutoka Mrugarama kwenda mpaka Rulenge, kutoka Rulenge mpaka Tembo *Nickel*, kutoka Rulenge mpaka Kumbuga, Murusagamba na Nyakahura, barabara ina urefu wa kilometa 114.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya barabara hii kama haijengwi hata ule Mgodi wa Tembo *Nickel* hauwezi kufanya kazi. Watanzania wote wanafahamu ni kwa kiasi gani tunatarajia mgodi wa Tembo *Nickel* ulete fedha nyingi kwenye nchi lakini kwa bahati mbaya kama hakuna barabara ya lami ile *nickel* haiwezi kuchimbwa. Hivi tunavyozungumza kuna mitambo imeshindwa kupita kuelekea Tembo *Nickel* ili wawekezaji waendelee kuwekeza na kujenga ule

mgodi kwa sababu hakuna barabara ya lami. Natambua juhudi nyingi ambazo tumeshazifanya, nakumbuka *engagement* ambazo nimeshazifanya na Wizara mbalimbali zinazohusika, nawaomba kwa unyenyekevu mkubwa kuhakikisha fedha yote imeingia kwenye bajeti hii. Sijawahi kukamata shilingi lakini kwa hili kwa sababu wananchi wangu wameahidiwa mwaka 1995, 2000, 2005, 2010, 2020 mpaka mimi naingia tumeahidi na Mawaziri wote wameahidi.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa unyenyekevu mkubwa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ninayotaka nimpe msemaji ni kwamba ile barabara ikijengwa kwenda kwenye machimbo hayo ya *nickel* itajenga barabara nyingi kutokana na faida ambayo itapatikana kwenye ile biashara ya *nickel*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa hiyo.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, yaani ndugu yangu natamani wangekuwa wanaruhusu kuja Bungeni na soda ningekupatia *pepsi*, nimeipokea hiyo taarifa. Naomba barabara hii itendewe haki na bajeti iingie ili barabara hii isaidie barabara nyingine za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine kwa upande wa miundombinu inasikitisha sana ni eneo la miundombinu ya umwagiliaji. Serikali ilifika Ngara Rulenge eneo la Vigombo na kuanza kujenga Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Vigombo zaidi ya miaka tisa iliyopita. Kwa bahati mbaya wale watu sijui hela waliitafunia barabarani wakati wanakuja kumalizia ujenzi, ile skimu ilitelekezwa mpaka leo, kwa miaka tisa iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya *engagement* na Serikali nimewaomba, sasa naomba niwakumbushe sasa hivi haiwezekani mimi nikapiga kura ya ndiyo kama ile skimu ya Vigombo fedha yake haijaingizwa kwenye bajeti kwa sababu tumewadanganya na tumewaahidi wananchi vya kutosha, muda umefika wa kwenda kukamilisha skimu ya umwagiliaji ya Vigombo, naomba wahusika watenge fedha twende tuwapatie haki wananchi. Kwa bahati mbaya Wabunge wengi wanajua ile miradi haikuwa Ngara tu ilikuwa maeneo mengi, sijui nini kilitokea ilitelekezwa na wakati muafaka wa kwenda kukamilisha miradi hiyo umefika, naomba bajeti iingizwe ili twende tukakamilishe ujenzi wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni eneo la kilimo. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu wananchi wa Jimbo la Ngara wamelima mazao mengi ikiwemo mazao ya mahindi. Hivi karibuni tumevuna zaidi ya *metric ton* laki moja na kwa bahati bei ya mahindi imeshuka kilo moja ya mahindi ni shilingi mia mbili. Nashukuru baada ya kupaza sauti Serikali imewatuma *NFRA* kwenda kufanya tathmini ili waanze kununua yale mahindi kwa bei elekezi ya Serikali, lakini tathmini ya nini wakati unakwenda sokoni unakuta mzigo wa mahindi umejaa, si uje na pesa anza kununua, pakiza kwenye fuso, lete Dodoma, tunza kwenye maghala ya Serikali? Siwaelewi kwa sababu mahindi yapo ya kutosha zaidi ya *metric ton* laki moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwa unyenyekevu mkubwa ianze kununua. Utafiti wakati mahindi unayaona unatafiti nini, unataka ugundue kitu gani zaidi ya mahindi yaliyoko sokoni? Naiomba Serikali ianze kununua, wawatumie fedha wale maafisa wanaofanya utafiti huko Ngara waanze kununua mahindi hayo ili tuweze kuwaokoa wakulima ambao wanauza mahindi kwa bei ya chini. Eneo lingine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti kulikuwa na upendeleo mwingine kwa Mheshimiwa Samwel, Mheshimiwa Kunti kwanza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia wasaa na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza naomba nianze na ukurasa wa 59 wa Hotuba ya Waziri Mkuu kwenye suala zima la upatikanaji wa maji na hapa naomba kwenda kwenye suala zima la ujenzi wa mabwawa ya kimkakati, mabwawa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Farkwa limekuwa ni wimbo wa Taifa ndani ya Bunge hili. Bwawa hili limekuwa likisemwa na kuandikwa kila mwaka wa bajeti, tangu Bunge lililopita lakini kabla hata mimi sijaingia humu ndani ya Bunge. Leo tena naona hapa kwamba watu wanaenda kwenye upembuzi, wanaenda sijui kwenye nini, hatuoni mwendelezo wa dhamira ya dhati ya kwenda kujenga bwawa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Waziri mwenye sekta pamoja na Waziri Mkuu ambaye ndiye Msimamizi wa Shughuli za Serikali watuambie Bwawa la Farkwa hatima yake ni nini? Ni lini bwawa hili linakwenda kujengwa na hizi stori za upembuzi, stori sijui za nini…*(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti kuna taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli bwawa hili limekuwepo muda mrefu sana kwenye vitabu, lakini kwa mara ya kwanza utekelezaji umeanza na

tunavyozungumza mkandarasi yupo *site*. Kwa hiyo, ni habari ambayo ni halisi, ni habari ambayo siyo tena mradi wa kwenye makaratasi au mpango. Mradi unatekelezwa, tunavyozungumza tunauweka kwenye maendeleo kwa ajili ya kufanya tunaita *conveyors* kuchukua maji kutoka Farkwa kuleta Dodoma. Kwa hiyo mradi unaendelea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Unaendelea na mchango, umemaliza? *(Kicheko)*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema hivi, Bwawa la Kidunda mpaka sasa hivi, kwanza gharama yake imetajwa ni shilingi bilioni 329, limeshafikia asilimia 17. Bwawa la Farkwa tunaambiwa maandalizi ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa wako wataalam washauri kufanyia mapitio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hiki kitu ndicho ninachosema bado ni *story*. Angalau Kidunda tumeambiwa imefikia asilimia 17 na fedha zimetajwa… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti aliyekujibu ni Waziri wa Mipango na hujui mambo yanakwenda vizuri.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mambo kwenda vizuri ningemkuta mkandarasi yuko pale. Ma-*bulldozer* yako hapo na mokorokoro yote yako pale, ningejua mipango inaenda vizuri, lakini kwa mipango ya kwenye maandishi hatutaweza kufika huko tunapopategemea. Shida yangu huyo Waziri wa Mipango angeniambia ni wakandarasi wangapi mpaka sasa na shilingi ngapi wameshatoa kwa mkandarasi na nini kinachoendelea na si kuniambia kwamba wako kwenye michakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hicho ndicho tunachokizungumzia. Hatuzungumzii suala la maandishi, kwenye karatasi. Tunataka kuona vitendo vikitendeka na watu wanapata maji na si vinginevyo. Kwa hiyo, nataka waje waniambie ni lini hii michakato yao inakwenda kuisha na wakandarasi wanaenda *site* na wanaanza kazi ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwenda eneo lingine ambalo nataka kuchangia. Suala zima la tawala za sheria, suala la ujenzi wa mahakama zetu, uwepo wa ukarabati pamoja na watumishi, kwa maana ya mahakimu na watumishi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ni muhimu sana. Watu wetu wengi wanakutana na kadhia mbalimbali na mahali pekee ambapo wanaweza kupata haki zao ni mahakamani. Mahakama zetu nyingi ni chakavu, lakini maeneo mengine hakuna mahakama kabisa lakini tatu watumishi hawajitoshelezi. Mahakimu leo hawapo wa kutosha, kwenye maeneo mengi mahakimu inabidi wafanye kazi na hatimaye unakuta wanafanya kazi na kuamua kesi kinyume kwa sababu kichwa kimejawa na msongo, kwa hiyo mwisho wa siku wanaamua kesi pasipokuwa na haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutolea mfano kwenye eneo hili la mahakama. Wilaya ya Chemba tuna mahakama kumi, katika hizi mahakama kumi zinazofanya kazi ni mahakama tatu tu. Mahakama ya Chemba, Mahakama ya Mrijo pamoja na ya Kwamtoro. Mahakama nne zilishakufa, majengo yalishaanguka, hakuna watumishi, hakuna chochote kinachoendelea. Kwa hiyo hawa watu wa ukanda wa Usandawe kule wanategemea mahakama moja, hakimu aliyepo ni hakimu mmoja na msaidizi mmoja. Hakimu huyo akiugua hakuna kesi zinazoendelea pale. Ndiyo maana tunaona hata wananchi wetu kwenda kuitafuta haki yao wanaona ni kheri tumalizane mtaani kuliko kuhangaika kutembea umbali mrefu, natumia gharama kubwa na akifika kesi zote zinaahirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo bado tuna changamoto kubwa sana. Serikali waone ni namna gani sasa wanakwenda kuboresha mazingira rafiki kwa kuongeza mahakimu na kuboresha haya majengo ambayo yanatoa huduma hizi za haki ili kutoa fursa kwa Watanzania kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo natamani kulisemea ni suala zima la kilimo. Nasema humu ndani tangu Bunge lililopita na Bunge hili. Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania

kwa ujumla tunafahamu kwamba Taifa letu linatumia gharama kubwa sana ya kuagiza mafuta ya kula kutoka nje. Tukaja na mkakati hapa wa kuhakikisha tunaondokana na changamoto hiyo kama si kuipunguza. Tukahamasisha wakulima wetu walime zao la alizeti, lakini sasa Serikali imekwenda kuondoa tozo kwenye mafuta ya kula ya kutoka nje. Hivi ni kweli tuna dhamira ya dhati ya kuondoa gharama kubwa zinazoingiwa na Serikali kwa kuleta mafuta kutoka nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wamelima alizeti, bei imeporomoka, hakuna mfanyabiashara wala mwenye kiwanda anayeweza tena kununua zao la alizeti wamebaki kufukuzana wanapishana na vibali kwenye maofisi. Wanaagiza mafuta kutoka nje kwa sababu Serikali mmetoa kodi kwenye mafuta ya kula. Kwa hiyo, leo tumeamua kulizika tena zao la alizeti, hakuna tena mwananchi atakayeenda kuwa na *morale* ya kwenda kulima zao la alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo viwanda vya ndani ambavyo tunasema tuviimarishe, viweze kuhimili ili tujenge uchumi wetu bado yatakuja kuwa magofu tu kama magofu mengine ambayo yalikuwa miaka ya huko nyuma. Naiomba Serikali, mara hii Waziri wa Fedha akija tunaomba suala la kodi kwenye mafuta iongezwe na ikiwezekana iwe ni asilimia 50 isiwe tena ile 35 ambayo aliiweka mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la nishati mbadala. Serikali inafanya kazi kubwa sana ya kusambaza mitungi ya gesi. Hata sisi Waheshimiwa Wabunge tulipewa hiyo mitungi. Hata hivyo mimi nikawa najiuliza kwamba hii mitungi ya gesi tunayopewa 100 unaenda unaigawa kule, hivi huyu mwananchi nikishamgawia huu mtungi wa gesi akimaliza ile gesi iliyokuwemo mle huo mtungi anaenda kuujaza wapi tena? Kwa sababu mpaka sasa bado Serikali haijafika wilayani, kwenye kata na maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuweza kutengeneza mazingira rafiki, kwamba mwananchi huyu akishamaliza ule mtungi aweze kupata fursa ya mahali pa kujazia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hivyo tu, gesi hii bado gharama yake ni kubwa. Leo mafuta ya *diesel*, *petrol*, mafuta ya taa tuna bei elekezi, ni kwa nini suala la gesi hatuna bei elekezi? Leo gesi kilo sita ni shilingi 35,000, hivi mwananchi wa kijijini kwa uchumi uliopo wa leo ni mwananchi gani anaweza kumudu shilingi 35,000?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala hili pia Serikali nia yake ni njema…

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba tayari Serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha wananchi wote wanapata gesi kwa bei rahisi. Tumeanza na ule mtungi wa kilo 52, tumeenda kwenye mtungi wa kilo tisa na sasa hivi tuna mitungi ya kilo tatu. Kwa hiyo, tunahakikisha mikakati yetu iko vizuri kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kupata mitungi ya gesi kwa bei rahisi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, hiyo inaitwa jaza ujazwe. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Sijauliza mipango na mikakati, nimeuliza gharama ambazo ziko kwenye gesi. Mtungi wa kilo sita ni shilingi 35,000, mtungi wa kilo tisa ni shilingi 58,000 hicho ndiyo tunachokiuliza, kwa nini gesi ni bei ya ghali? Tunachotaka Serikali waje hapa watuambie, kwamba gesi mtungi wa kilo sita kwa sasa kutoka shilingi 35,000 ni shilingi 10,000. Hicho ndicho tunachokitaka, ambayo ni bei rafiki na Watanzania wote wana uwezo wa kumudu kwa hiyo shilingi 10,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine wametangaza kwamba leo taasisi ambazo zinatumia kuni nyingi wanakwenda kupiga marufuku, wanataka waingie kwenye mfumo wa gesi. Bado hicho kitu hakitawezekana kutokana na gharama kubwa iliyopo kwenye

upande wa gesi. Nataka kujua, Serikali imewawekea mkakati gani madhubuti na rafiki utakaosababisha taasisi hizi ziweze kumudu matumizi ya gesi kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia suala zima la upande wa Polisi. Polisi wamekuwa wakikamata magari ambayo yana ving'ora na vile vimulimuli. Sasa nikawa najaribu kujiuliza, hivi ving'ora na vimulimuli Serikali imeruhusu viingie sokoni. Vinatoka huko vitokako vinaingia ndani ya nchi, vinalipa kodi, wanataka nani avitumie? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizidi sana, dakika moja tu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Samweli. *(Makofi)*

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na jioni ya leo naanza kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniruzuku uhai, afya njema na nguvu ili niweze kuchangia kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Hanang.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba tarehe 3 Desemba, 2023 Jimbo la Hanang tulipata changamoto kubwa sana ya maporomoko ya Mlima Hanang na kwenye hayo maporomoko madhara mengi yalitokea. Narudia tena kuishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo ilifanyika. Mji wa Hanang ambao ni Makao Makuu ya Wilaya pale Katesh palijaa tope ambalo kwa kweli tungetakiwa tutoe sisi wenyewe ingetuchukua labda miaka mitatu ili tuweze kulimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa angalau wananchi wanapita kwa sababu Serikali yetu sikivu ya Chama Cha Mapinduzi chini ya usimamizi makini wa Dkt. Samia Suluhu Hassan waliacha kila kitu ili kuhakikisha kwamba wanatusaidia na kwa sasa mambo mengi yanaenda sawasawa. Mambo mengi yalifanyika ili angalau zile huduma za msingi ziweze kurudi kwenye hali ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kipindi kile kila mtu alikuwa amechanganyikiwa. Tumepoteza ndugu zetu 89, wengi waliathirika lakini na biashara za watu ziliathirika. Miundombinu mingi ambayo tulikuwa tumeitengeneza kwa gharama kubwa yote ilienda na yale maporomoko. Tunasema tunaishukuru sana Serikali kwa nguvu ambayo iliitoa, tulishinda usiku na mchana na Mheshimiwa Jenista Mhagama na timu nzima ya Serikali, tunasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingi zimekwishafanyika. Madhara yale ni makubwa sana, ukiangalia kwa miundombinu ambayo iliathirika, kwa maana ya barabara, mpaka sasa Barabara ya kutoka Endasak – Gitting – Gendabi - Dawar hiyo haipitiki kabisa. Ukishuka upande wa mjini barabara zote za mjini maeneo mengine ni maporomoko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fedha tulizoziomba kwa upande wa barabara. Upande wa miundombinu ya maji, mlima Hanang ndicho chanzo kikuu cha maji kwa Wilaya ya Hanang. Tuna kata karibu saba, tunaanza Kata yenyewe ya Gendabi, Kata ya Dawar, Gitting, Measkron, unakuja Kata ya Nangwa. Ukija kwenye mamlaka yote ya mji, Kata ya Katesh, Kata ya Ganana, Kata ya Dumbeta na Kata ya Jorodom wote hao miundombinu ya maji iliathirika, tulijaribu kurudishia kwa kipindi kile kwa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatamani na sisi turudi kwenye hali ya kawaida ya maendeleo ambayo tuliyatamani na ile Hanang ambayo ni ya maziwa na asali ili tuweze kuirudia. Kuna fedha ambazo tuliziomba, tunaomba zile fedha zitoke kwa wakati ili miundombinu hiyo yote iweze kurudishwa kwenye hali yake ya kawaida ili Hanang iweze kwenda sawasawa na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, fedha kwenye upande wa maji na upande wa miundombinu ya barabara zitoke kwa wakati ili kazi ile iweze kukamilika na sisi tuweze kurudi kwenye hali ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kipindi kile kuna biashara ambazo ziliathirika moja kwa moja kwa sababu lilipigwa eneo la soko ambalo lilikuwa linategemewa na wananchi wote wa Mji wa Katesh. Kwa sasa tunaishukuru sana Serikali, imejenga soko kwa ajili ya kurudishia. Hata hivyo lile soko liko pembeni kidogo ilhali wananchi wameshazoea kuishi mazingira ya mjini. Kuna changamoto ya kukubali yale mazingira kwamba sasa tukitoka kule nani atatufuata, kwa sababu utaratibu wa binadamu pale ambapo umezoea kila siku kwenda ndiyo akili yako muda wote iko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ukitembea Mji wa Katesh kila sehemu kila mtu ametegesha sehemu ya kushikilia na wale wafanyabiashara wengi waliathirika. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Jenista Mhagama. Tuliwaita watu wa benki na taasisi za mikopo, tukaongea nao ili waangalie namna ambavyo wanaweza kuangalia kupata unafuu kwa wale wafanyabiashara kwa sababu athari zile ni kubwa na biashara nyingine zilikuwa ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kuangalia namna ya kusaidia zile biashara zilizoathirika moja kwa moja. Tuwalee wale ili waweze kurudi kwenye hali yao ya kawaida, wale wanahitaji kulelewa. Tunafahamu kazi kubwa imefanyika, tunaomba, kwa sababu kweli changamoto ilikuwa ni kubwa, lakini ukiangalia biashara 713 zilizoathirika moja kwa moja kila mtu alikuwa na hali tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wale ambao wanaweza kujimudu baada ya kuwaombea zile nafuu ambazo tuliziomba na wakazipata, lakini kuna wale ambao hawana namna, hawa tuendelee kuwalea, tuendelee kuwawezesha ili kuhakikisha kwamba wanarudi kwenye hali yao ya kawaida ya maisha. Naomba kwenye eneo hili tuendelee kushirikiana, kuhakikisha kwamba wale wananchi wanaweza kurudi kwenye hali yao ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kati ya sehemu kubwa ambayo Ofisi ya Waziri Mkuu inaifanyia kazi, ni kuwawezesha wananchi kwa kuhakikisha kwamba wanapata au wanachochea uchumi wa wananchi. Tumekuwa na utaratibu wetu

wa kuwapa mikopo isiyokuwa na riba kupitia mapato ya ndani ya halmashauri zetu, ile 4:4:2. Kwa maana ya kwamba vijana wanapata asilimia nne (4), akinamama wanapata asilimia nne (4) na walemavu asilimia mbili (2). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo hiyo ilitolewa kwa kipindi kirefu, lakini wananchi wengi walinufaika na walikuwa wakiitegemea. Ni kweli changamoto zilijitokeza kwamba fedha zile zilikuwa hazirudi. Tunachoomba sasa ile mikopo iliyosimama maana yake shughuli nyingi za wananchi za kiuchumi zilisimama. Ungefanyika utaratibu wa haraka kuhakikisha kwamba zile fedha zinaanza kutoka tena ili wananchi wetu waweze kufanya shughuli zao za kawaida ambazo wamezoea, za kilimo, biashara, uvuvi na ufugaji. Tukiendelea kushikilia hizo fedha maana yake tumeshikilia uchumi wa wananchi, tumeshikilia uchumi wa nchi yetu. Hizo fedha zianze kutoka mapema inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia mahitaji makubwa ya kupeleka ile elimu ya vitendo kwa wananchi wetu Serikali iliridhia vyuo vya ufundi vijengwe kwenye maeneo mbalimbali ndani ya wilaya yetu. Kulikuwa na ujenzi wa vyuo vya ufundi kila wilaya. Ukipita pale Hanang ambako tulichagua eneo la Nangwa kwa ujenzi wa chuo cha ufundi, ukipita unasikitika kwa jinsi unavyoenda kwa kasi ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iwe inatoa fedha kwa wakati ili ujenzi ukamilike kwa vyuo vile ambavyo tumevilenga ili hatimaye tupate wataalam tunaowahitaji kwenye maeneo yetu. Imekuwa zaidi ya mwaka mmoja sasa hakuna hata sehemu moja kwenye ujenzi wa vyuo vya ufundi ambao unafanyika, nikitolea mfano eneo la Nangwa ambao haukufika hata hatua ya *lintel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kwenye eneo hili iweke fedha za kutosha ili kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika kwa wakati. Ili hatimaye watoto wa Kitanzania wapate ujuzi unaohitajika kwenye eneo la kilimo, uvuvi, mifugo na hatimaye waweze kupambana na mazingira waliyonayo kutumia elimu ambayo itatokana na vyuo vyetu vya ufundi ili kutibu tatizo ambalo lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya wafugaji yalianzisha shule maalum za watoto wa wafugaji. Kwa Jimbo la Hanang sisi tulikuwa na shule mbili maalum kwa ajili ya watoto wa wafugaji. Tulikuwa na shule ya Gendabi na shule ya Bassodesh ambazo zote ni shule za msingi za bweni. Shule hizi zilikuwa zinasaidia kwa sababu maisha yetu ya ufugaji kwa sasa bado hatujayaboresha kiasi cha kwamba tunaweza kutulia sehemu moja na watoto wetu wakapata elimu inayostahiki, tumekuwa na maisha ya kuhamahama. Ili kutibu tatizo hilo la wazazi kuhamahama, watoto walikuwa wanawekwa bweni ili wapate elimu kwa wakati bila kubughudhiwa na tabia ile ya kifugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali chini ya usimamizi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumepata ukarabati mzuri kwenye Shule Maalum ya watoto wa kifugaji ya Gendabi ambako angalau pakikamilishwa kabisa yale mazingira yangekuwa sawasawa. Ukienda Bassodesh kwa sasa hali ni tete, mabweni yamebomoka, madarasa yamebomoka na ile shule ni ya miaka mingi, wamesoma watu ambao mpaka sasa wameshastaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tutengewe fedha ili kuhakikisha yale maeneo maalum tuliyoyatengea na yale ya uangalizi yaweze kupata fedha na kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanatengenezwa vizuri ili watoto ambao wana changamoto ya kupata elimu nao wapate elimu inayopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kutoa salamu kwa ndugu zangu wa Wizara ya Ujenzi. Kumekuwa na taratibu hizi za *EPC+ F*, taratibu hizi za *design and build* lakini taratibu hizi barabara zingine unaanza ule upembuzi wa awali na usanifu wa kina. Barabara ya Haydom- Mogitu imekuwa ya muda mrefu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea hivi hatutaelewana, barabara hii inapaswa kujengwa ni ahadi ya Marais watatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Ushauri wako wa kitaalam unaweza kukaa na Waziri na watu wa *TANROADS* ukawapa elimu zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Samweli ndiye amefunga orodha yetu ya jioni, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 11.19 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 4 Aprili, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*